

**CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION  
(CKRC)**

**VERBATIM REPORT OF**

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS,**

**WUNDANYI – ST PAUL'S CHURCH, WERUGHA**

**ON**

**30<sup>th</sup> APRIL 2002**

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, WUNDANYI CONSTITUENCY HELD AT ST. PAUL'S CHURCH,  
WERUGHA, ON 30<sup>TH</sup> APRIL 2002.**

**Present:**

1. Com. Prof. A. I. Salim
2. Com. Domiziano Ratanya

**Secretariat Staff In Attendance**

- |                     |   |                           |
|---------------------|---|---------------------------|
| 1. Collins Mukewa   | - | Programme Officer         |
| 2. Fidelis Wangatta | - | Asst. Programme Officer   |
| 3. Lucy Atieno      | - | Sign Language Interpreter |
| 4. Grace Gitu       | - | Verbatim Recorder         |

The meeting was called to start at 9:30 am.

**Mr. Malasi:** Kuhusu ya kumwezesha kukilimu mahitaji yake ya kimsingi kama vile chakula, nguo na malazi. Halafu ya mwisho ni kwamba pato ni gawanyo kwa kutoa asili mia mbili kwa ngazi nyingine kuanzia chini kwenda kitaifa, yaani kwanzia serikali za mitaa ama kwanzia ngazi ya kijijini kwenda ngazi ya kitaifa kuwe kunatolewa asilimia mbili ya lile pato ambalo limepatikana pale ndio tunaenda kwa ngazi ile lingine ya juu kwa hivyo shukrani, nimeshukuru.

**Com Salim:** Asante Bwana Malasi. Na sasa tunamwita Bwana Moses Mugo.

**Mr. Moses Mugo:** Bwana Mwenyekiti wa makao hii, majina yangu ni Moses Mugo mzee kutoka hapa Weruga. Mapendekezo yangu ni kuhusu haki za watoto.

**Interjection:** .....(inaudible)....

**Mr. Mugo:** Mapendekezo yangu kuhusu haki za watoto. Watoto hawapati elimu sawa sawa. Na kutopata elimu huko ni kwa vile elimu ni ya pesa. Elimu inafaa iwe ya bure ili watoto wote wapate elimu.

Jambo la pili, ni watoto wa kike kukosa wajibu wao wa kufanya vizuri ama wote. Wanaponyimwa haki zao wanajisimamia. Vijana: Iwekwe sheria ya kuweza kuwalinda.

Ya tatu, mtoto anayezaliwa wa kike au kiume wanatoka kwa mmoja lakini uridhi unaridhiwa na watoto wa kiume peke yao

ilhali watoto wa kike wananyimwa. Kuwe na haki mtoto wa kike aweze kuridhi naye kama wale wa kiume wanaridhi mali ya babake.

Rasilmali za nchi kama tuseme tuna pesa za wanyama, pesa zile zinatoka kwa wanyama sehemu kubwa itumiwe na wananchi wa pale kwa sababu hata kama kunatokea na madhara yanaingia kwa wao, wanaumizwa, wanaauwa halafu sehemu chache iende kwa serikali ili iweze kuwasaidia wale ambao wanahusika pale pale na kuuwa pale pale na madhara wanaopata pale pale.

Hosipitali ziwe za bure, watu wapate dawa ya bure. Wakati huu tunapoteza watu wengi sana, wengine hawana uwezo wa kutoa pesa ya kununua madawa. Kwa hivyo, watu wote wapate madawa hata wakiwa wanyonge, wakiwa nini ili tuwe na usalama kati ya watu.

Natumaini yangu ni hayo machache.

**Com Salim:** Asante sana mzee Moses Mugo kwa maoni yako. Tutaendelea mbele, tutamwita Bwana Sylvester Mwadime.

**Mr. Mwadime:** Jina langu ni Sylvester Mwadime kutoka Umingu location. Shukrani Bwana chairman na hata wananchi wenzangu wa taifa. Maoni yangu hasa ni kuhusu kutoka nyuma ya katiba hii iliyoko sasa. Wakati mimi nakuwa nazungumza juu ya wavulana na wasichana na mila zetu za kitaita. Nafikiri mila zetu za Kitaita zilikuwa kwanza kabla msichana hajaolewa asipate mimba.

Na kama amepata mimba, ichukuliwe kisheria kama ule bwana atapenda bibi yake amchukue wazungumze na wazazi wa msichana yule apate kumuo.

Basi kulikuwa na sheria ya kimila ambayo ilihusu mvulana aweze kulipa ule msichana ngombe moja dume na kike moja. Hiyo ni kwenye mimi nikikuwa hapa, halafu anaweza kuwa free. Baadaye sheria ilikuwa inasaidia yule mtoto wa miaka kumi na sita, apelekwe kortini na amgharamie yule mtoto, maana yule mtoto haki yake iko kwa baba yake aliyemzaa; haiko tena kwa babu yake.

Tulipoendelea kwenye 656 hii sheria iliondolewa na sijui iliondolewa kivipi. Na hata hivi watoto wengi ama wasichana wengi walio Kenya hata hii namba tulio nao sasa, ambaye ni 30 million au 28 million, inakuwezesha na hawa wasichana waliokuwa hapa free kuwa kubwa namna hiyo.

Mimi naomba wakati huu tunapoenda kufanya katiba hii, kwa sababu mimi ni mzazi na nina mababu zangu wengi ndani ya nyumba; hiyo ichukuliwe maanani iweze kurekebishiwa maanake tunarekebisha hizi sheria kila mara. Badala ya miaka kumi na sita iwekwe pengine 24 years kugharamia yule mtoto mpaka kiwango cha chuo kikuu. Hiyo ni oni langu la kwanza. Kama mzazi yeoyote atapenda sawa lakini haya ni maoni ambayo imesahauliwa sasa na Kenya hii inakwendaisha kwa sababu hiyo, hasa kwa wakati huu kuna magonjwa tofauti ambayo iko hii jogoo wakati huu. Sheria hii ikiundwa nafikiri itazuia mambo mengi kwa vijana. Hiyo ni maoni yangu ya kwanza.

**Com Salim:** Endelea.

**Mr. Mwadime:** Oni langu la pili, nafikiri wakati wa uhuru kupatikana mimi nilikuwepo, na tumejadiwa mambo mengi uhuru ulipopatikana na hayajafanyika vile walivyoahidi. Sasa mimi ningelipendelea siku ile tunaanza na vyama viwili KANU na KADU ilikuwepo, wakati tunapewa uhuru halafu KANU ikachukuwa KADU ikawa bado hajafaulu ni kwa sababu hii watu wengi walikuwa hawaelewi mambo ya KADU ni nini, na serikali za utamaduni zinafanya kazi gani.

Basi mimi naomba wakati huu watu wameshaelewa wote katika Kenya vile serikali ya majimbo inatakikana ifanye. Tumeona saa hii katiba tunayotaka kufanya kama ni ukweli wa mambo iweze kurudisha serikali za kimikoa ama kimajimbo kwa sababu serikali nyingine katika ulimwengu zinatumia ukweli magavana wanapewa nafasi za kupigania urais. Lakini tukiendelea vile tulivyo mimi naona hata katika jimbo lolote katika Kenya hatutashirikisha haki zake. Kwa hivyo, nchi itakapokuwa ikiongozwa na vijana watakaokuja, maana sisi tunaenda hivi, Katiba ingeiusisha kila mkoa kushiriki kupigania kiti cha urais. Hiyo ni maoni yangu binafsi.

Oni lingine la tatu la muhimu; tangu nimeanza kupiga kura 1963, wakati tulianza kupiga kura kama kawaida lakini vile nilivyopiga kwa mara ile ya kwanza 1963, upigaji kura wa miaka iliyofuata sio za halali kwa sababu hizi kura huchukuliwa kutoka kituo cha kupiga na kwenda kuhesab iwa mahali pengine. Nitauliza hii Commission kama itawezekana kura ziwe zinahesabiwa katika kila kituo chake, mahali kule zimepigiwa yaani kuhifadhi haki. Kwa hayo machache asante sana mwenyekiti wangu na wananchi wa Commission kwa kunisikiza.

**Com Salim:** Asante sana bwana Mwadime kwa maoni yako. Labda ningetaja tu kwamba hili pendekezo lako la mwisho kwamba kura zihesabiwe pale pale ambapo zitawekwa yani poll station, jambo hili limeshatangaza na mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi, Bwana Samuel Kivuitu kuwa litayekelezwa. Asante, tukiendelea mbele, Bwana Eric Mugahu Kiwinga.

**Mr. Eric Mugahu:** Kwa majina yangu naitwa Patrick Eric Mugahu Kiwinga. Bwana Chairman, pendekezo langu la kwanza kwa hiki kikao ni juu ya sisi wale watu ambao tumestaafu. Ningependelea katiba iangalie vile tunalipwa malipo ya uzeeni. Unakuta mtu aliystaafu labda miaka ishirini iliyopita na Mungu amempatia nafasi ya kuishi, pension aliyokuwa akipewa haiwezi kwenda juu.

Wakati wa review ya mishahara ya Civil Servants inapochunguzwa, hawa watu hawaangaliwi. Kwa hivyo ningeomba wakati wowote mishahara inapochunguzwa wale watu wanaopokea malipo ya uzeeni waangaliwe.

Jambo langu la pili ni juu ya mgao wa ardhi. Hapa sisi Taita Taveta tumeona ya kwamba mgao wa ardhi umekuwa ka kwamba mashamba makubwa makubwa ambao yamechukuliwa na watu binafsi ama watu wawili watatu na huku sisi Wataita tunaumia kukosa shamba. Hapo ningeomba katiba hii iangalie na ikiwezekana hapa Taita Taveta kila mtu awe na uwezo wa kupata ekari ishirini mwisho na hizo ambazo zinabaki zipatiwe hawa.

Jambo lingine la tatu ni juu ya uhuru wa kuabudu. Tumeona tumepewa uhuru wa kuabudu na serikali yetu ya zamani mpaka ikawa watu wameenda hata kupita kiasi kuabudu mashetani. Hapa ningeomba jambo hii liangaliwe na sheria ipite kwamba hakuna mwenye kuabudu mashetani tunamwabudu Mungu Mola peke yake.

Pia, katika mambo ya utawala tuweze kuangalia wale watu ambao ni wazee wa kijiji tuwafikirie na kuwapea kitu kidogo kama vile naibu wa Chief wanavyofanyiwa wanapopewa mshahara.

Na hapo tukiendelea pia, kuwe na serikali ya majimbo. Naona maoni yangu ni hayo. Asanteni.

**Com Salim:** Asante sana Bwana Kiwinga kwa maoni yako na sasa namwita Bwana Harold Mgeni.

**Mr. Harold Mgeni:** Majina yangu ni Harold Mgeni. Pendekezo langu katika katiba hii ningeomba sana tuwe na serikali ya majimbo ambapo wananchi wa jimbo fulani wawe ndio wenyewe rasilmali; kama kukitokea nafasi ya kuandikwa kazi wafanyi kazi, nafasi zipewe watu wa jimbo hilo. Hayo ndiyo mapendekezo yangu.

**Com Salim:** Naona Bwana Mgeni kwamba unawasamehea wenzako wengine. Ni chama, ni kitu gani, group yako inaitwaje?

**Mr. Mgeni...(Inaudible)**

**Com Salim:** Pamoja. Asante, sasa namwita Bwana Ferdinand Mulamba.

**Mr. Mulamba:** Majina yangu ni Ferdinand Mulamba. Kwa maoni yetu tungependelea tuwe na Kenya huru kiuchumi, kisiasa, kisheria na inayosimamiwa na kanuni na mwongozo wa katiba mpya.

Utawala uwe wa majimbo. Viongozi wachaguliwe na wananchi wenyewe. Bunge lipewe uwezo wa kuteuwa jaji mkuu na mkuu wa sheria.

Rasilimali zilizoko National Park iwe 25% halafu na hiyo nyingine ipatiwe mashamba iwe ya wananchi. Wagombea viti wawe ni wa kutoka eneo hilo wanapotoka. Soko isiwe huru, biashara ndogo ndogo ifanywe na wananchi wale wadogo wadogo. Ndizi zozote ziondolewe na mashamba kuregeshwani wananchi wenyewe.

Haki za watoto zirudishwe na ajira kwa watoto iondolowe na baada ya masomo yao waajiriwe kazi.

Asante sana.

**Com Salim:** ...**(inaudible)** memorandum tafadhali pita hapa kwa wenzetu hapo na ujisajili au uregister hapo.

Sasa namwita Bwana Sospeter Shake...**(inaudible)**...Tutaendelea mbele Bwana Kariuki yupo...**(inaudible)**...Bwana Masharu Maworia au Marora.

**Mr. Masharu:** Mimi kwa majina naitwa Masharu Mawora...**(inaudible)**.... nafikiria ni memorandum lakini siwezi kukiuka mkataba wetu na wale tulikuwa tukichangia katika mtandao huu; kwa hivyo waliniambia lazima nisome kwa hivyo nitajaribu

kadiri ya uwezo wangu kwenda haraka haraka na iwapo kutakuwa na nafasi...

**Interjection:** Kurasa ngapi?

**Mr. Masharu:** Kidogo tu

**Com Salim:** Haya dakika tano.

**Mr. Masharu:** Haya nitajaribu kadiri ya uwezo wangu. Katiba inapasa iwe ikishirikisha wananchi kikamilifu, iwe inafundishwa shulenii ili watoto waweze kujua kizao na majivuno zao. Katiba isiwe ni siri kwa hivyo jina la ‘serikali’ tunataka liondolewe kwa vile kama katiba inashirikisha shulenii ina maana ya kwamba hakuna siri tena kwani hiyo siri ilitungwa na wabeberu kunyanyasa sisi na pia ndio ilitumiwa na kiongozi wetu wa kwanza kuongoza taifa hili kutunyanyasa sisi kama vile shamba la mkongwe la Mwatate ambaa lilimilikiwa na Beth Mugo na Keria Shamba la Taveta ambaa limemilikiwa na Muholo na Basili Criticos-ikiwa ni jamii moja hiyo ya huyo mtawala.

Na tungependelea pia kulease, leaving ya mashamba kama hii ya makonge wananchi wawe wakifahamishwa na muda ule utatakikana isiwe kwamba leasing inafanywa na wananchi waelewi hiyo, hawajui.

Tajiriba tunazoweza kuandika kwenye utangulizi hizi ni kama zifuatazo. Uchumi unaendelea kuzorota baadala ya kustawi. Kwa hivyo, katiba itoe nguvu na uwezo wa kuchunguza kwa nini uchumi unazorota na kama kuna mtu, mashirika, makampuni au hiyo serikali ambayo imechangia uzorotaji wa uchumi ni sharti washtakiwe. Kwa mfano, tulikuwa katika mshororo mmoja na nchi kama China na Japan lakini hivi leo hatuonani kamwe. Isitoshe, tunakaa chini tukiomba msaada kwao. Aibu ilioje?

Bunge lisiwe na mamlaka ya kubadilisha katiba kama vile linavyotaka. Hii ni kwa mujibu tunavyoona vile wanavyofanya kwa hiari yao wenyewe sio kwa masilahi ya wananchi waliowapeleka kule. Mfano, hivi majuzi wabunge walitaka kupandishiwa mishahara yao, wananchi ndio wanaofaa kutoa pendekero kama hilo kulingana na kuridhishwa kwao na vile kazi wanavyoitekeleza.

Uraia utakuwa ni mzaliwa yejote amezaliwa Kenya. Katiba ikuuhusu mtu kuwa na uraia. Vile katiba isiruhusu raia wake kuweka pesa nje ya nchi yake; mtu ambaye si raia wa Kenya asiruhusiwe kumiliki ardhi ya nchi hii.

Katiba isiruhusu ununuvi wa uraia. Katiba iruhusu raia wao wasomi kufanya kazi nje ya nchi yao kisha 10% ya mapato yao irudishwe kusaidia pahali raia huyo alipozaliwa yaani kwao, ili maendeleo yaweze kuafikiwa hata vijijini na sio majiji peke yao. Iwapo haya yote yatajumuishwa kwa katiba basi ina maana ya kuondoa umasikini.

Ulinzi, rais asiwe juu ya sheria ama mkuu wa amiri jeshi na pia asipewe wadhifa wowote licha ya uongozi kama ni rais awe ni rais tu. Bunge iwe na uwezo wa kuchagua rais na pia uwezo wa kumuondoa wakati wowote iwapo atapatikana na hatia.

Kuwe na serikali ya mseto yaami vyama vyote vishirikiane kwa upande wa kupewa kwa waziri kulingana na taaluma zao.

Katiba isiruhusu utumiaji wa pesa katika kampeni na iwapo yejote yule atafanya hivyo ni kuvunja sheria na adhabu hiyo itakuwa ni kuondolewa kwake kugombania kiti kwa muda wa miaka isiyopungua ishirini. Wagombeaji wote yaani wapinzani na wale wako katika chama tawala wawe kitu kimoja; kama ni kampeni, watakuwa wakizifanya pamoja na kujieleza kwa wananchi kinaga ubaga. Kwa mfano, kama ni mukutano, wote wanahudhuria siku hiyo moja kwa pamoja na kujieleza kwa wananchi vile watakavyoshirikiana.

Tunataka serikali ya majimbo, wazalendo wakasema tunataka kodi zile wananchi wanazolipa ziwe zikirudishwa kufanya maendeleo pale walipozaliwa na pia pesa inayoingia kutokana na rasilmali ya eneo hilo itumike kufanya maendeleo katika eneo hilo.

Serikali za mitaa ziwe na mamlaka za kusimamia pesa zinazoingia kutokana na rasilmali hiyo na pia kuwe na kamati kuu tekelezi ya maendeleo ambayo imechaguliwa na wananchi kikamilifu ili ziweze kutumiwa kuimarisha maendeleo eneo hilo.

Haki za kimsingi, mtoto yejote awe na haki ya kupata elimu bila kujali uwezo ya kupata elimu au dini. Kila mzalendo ana haki ya kupata matibabu bure. Kila mzalendo awe ana haki ya kutetewa kisheria bila kujali mambo ya pesa. Ni haki mwananchi aliyedhulumiwa mali yake kortini kuregeshewa dhamani ya mali yake. Kwa mfano, sasa kama mali yangu imeibiwa na mwizi akapatikana ametumia basi mwizi hufungwa lakini mlalamishi huwa hafaidi kitu maana pesa yote ya faini huenda na serikali. Ni haki serikali ichukuliwe hatua za kisheria iwapo itamdhulumu mwananchi wake. Kwa mfano, hivi majuzi mndopomoni ndovu walivamia shamba la Bwana James Wanjala na Bwana Mwanganga na kula nafaka zao zote na kuharibu mazingira yao lakini mpaka sasa masikini wa Mungu watu wao wameachwa katika janga la njaa na hawajui fidia yoyote ahadi ni ya uwongo kama kawaida. Maana ndovu ndio tunaambiwa ni serikali mwananchi si serikali.

Mwananchi awe anashirikishwa katika mfumo wa elimu ili waweze kuchangia kwa kutoa maoni yao.

Vyombo vyote vya habari viwe huru na viwe na lugha ya kuelewaka na kila mwananchi kuwa na uhuru wa biashara. Mfano, pombe za kienyeji Nairobi Laini Saba hapo karibu na Moi Kabarnet gardens zinatengenezwa kuuzwa na kulewa na watu hawashiriki lakini ukija hapa mashambani unaambiwa na kushtakiwa na hatimaye kufainiwa au kufungwa iwapo hana uwezo wa kutoa faini.

Haki ya ardhi, katiba iwe na mamlaka ya kumpatia mwananchi yejote ardhi ambaye amefikisha miaka kumi na nane. Haki za wanajami na tofauti ya kitamaduni. Kila jamii irusiwe kuhudumisha mila zake mradi isikiuke haki za mtu binafsi. Tuwe na lugha moja ya kitaifa ambao ni lugha ya Kiswahili kwa vile kiswahili haki ya Agikuyu isiya kikabila. Mazingira na mali asili yatumiwe kwa manufaa ya mwananchi wa eneo hilo. Uhusiano wa kimataifa katiba isikubali iwekewe masharti na nchi au mashirika ya nje.

Tume za kikatiba, taasisi na afisi kuwe na tume ya kuhakikisha kwamba katiba hakiuki. Mkuu wa sheria awe anahidhirishwa na bunge na sio kuchaguliwa na rais.

**Interjection:** .....(inaudible).

**Mr. Masharu:** Mawaziri wawe wakichaguliwa na bunge kulingana na taaluma zao na pia bunge iwe na mamlaka kunyanganya watu wadhifa huo kama atashindwa kutekeleza jukumu zake. Wananchi pia wawe na uwezo wa kumwondoa mbunge ambaye alishindwa kutekeleza majukumu yake.

Kurisi na upokezanaji wa uwezo, mkuu wa sheria ndiye atakayekuwa na mamlaka ya nchi wakati huo. Rais ataanza kazi yake mara moja anapotangazwa mshindi na kuapishwa mkuu wa sheria baada ya wiki moja yaani siku saba ya kupewa pongezi na marafiki zake. Na mwisho hatuna la ziada ila tu Mwenyezi Mungu agiuse mioyo za hawa wanaochangia ujisadi na kufanya Kenya taifa la umasikini. Waliochangia katika mtandao huu wa katiba ni wengi wote kutoka Mwalampishi.

Asanteni sana kwa kusikia maoni yetu.

**Com Salim:** Asante sana bwana Marora kwa maoni yako.....(inaudible)..... na sasa tunamwita bwana Demeritus Mwasi karibu.

**Mr.Mwasi:** Yangu ni machache tu. Nashukuru Mungu kwa nafasi hii ya kuweza kuzungumza machache. Jina langu ni Demeritus Mwasi nataka kuzungumza machache. Kumbuka ya kwamba, sisi Wataita ni nchi yenye milima na nafasi ya kulima ni kidogo, na mashamba ni madogo na katiba ya nchi iheshimu nchi yetu na kila mwananchi. Na pili, hali ya kuabudu iweze kuva vile ilivyokuwa huru na kuzuia kabisa wale wanayoingilia kuabaudu mashetani wasiweko ili kutesa wananchi na kuzuia maendeleo.

Nataka hali au mila za kiafrika desturi ya nchi iheshimiwe na watu wasiwe na ubaguzi na tena wawe wakipendana. Na tunaomba serikali yetu iwe ya majimbo yenye kupendana yaani kuangaliwa na mtu mmoja na hao majimbo waweze kutumia mali zao wenyewe na pia kila mwananchi ambaye yuko na shamba yake atakayepatikana na mali ya asili asiondolowe bali awe naye wale wenenipa bali hiyo mali yake mwenyewe na kama wanapatikana watu wa kuitoa, waweze kushirikiana na huyo mwenyewe shamba hiyo.

Na pia katika hii ngazi iangaliwe ya kwamba kutoka msingi watoto wafunzwe lugha yao wenyewe mpaka waweze kufahamu na wanapoendelea katika class cha kwanza na cha pili na cha tatu, wajue lugha yao kulisoma na kuiandika na pia wafundishwe lugha nyingine kama inavyowezekana. Na pia kusiwe na ubaguzi wowote katika majimbo.

Serikali yetu tunataka iwe ya democracy, yaani majimbo yote yawe hakuna ukabila, iwe Kenya moja. Na hapo nazidi kupendelea ya kwamba, maoni yangu ni kwamba watu waheshimiane, na wakati wanapochagua mtawala achaguliwe na raia, ama kama ni mwenyekiti wa kijiji, achaguliwe na raia, kama ni chifu achaguliwe na raia, hata kama ni mbunge aweze kuchaguliwa na raia wakimjua tabia yake.

Na pia ningelipendelea ya kwamba, elimu ya msingi hata ikiwezekana mpaka ile ya sekondari iwe bure maana mwananchi anapotozwa kodi, hata kama kodi za VAT, wale wanaonunua magari huwa imekwishatozwa tayari ile VAT wasiulize tena mambo ya VAT na kutoa kodi, maana kodi huwa imeshatolewa kwa ile kodi ya VAT au material unayetumia asiitishwe tena au

kulipisha kodi nyingine.

Maoni yangu ingine ni ya kwamba hizi isiwe ya kufanywa kidogo kidogo, licence hii ndogo, na hii nyingine kama licence ya soda, licence ya sukari, licence ya nguo, iwe mtu akishakata licence iwe ina-cover kila biashara anayetaka kufanya iweze kuwa anafanya kwa njia nzuri. Na hapo pia ile ningelipendelea ile biashara ndogo ndogo kama zile za akina mama wanavyofanya wasiwe wanatozwa pesa nyingi, iwe ni kama pengine shillingi tano tu, akishinda mahali kiasi yake aweze kuangalia watoto wake. Kwa hivyo sio wananchi wasihangaishwe katika miji yao, yaani kwa nini nakaa hapa nakaa pale wawe wakiangaliwa tu kwa njia ya heshima.

Tunataka heshima idumu kwa wakubwa na wadogo. Na pia ningelisema tuheshimiane, pawe baraza na mkutano, katiba yetu itengenezwe wao wakikutana viongozi wote wa kidini watakwenda kupanga mambo wakaabudu kwa njia inayohitajika kama maandiko inavyotuongoza.

Hayo ndio maoni yangu ambayo ningependelea katiba yetu iwe yenyehaki, yenyekujali mtu yule wa chini na mambo ya bei iwe ikiangaliwa kila wakati; ya kwamba mara nyingine sasa ilikuwa ni soko huru na watu walibandika bei vile wanavyotaka mpaka inatatiza watu wa chini.

Na hali ya mshahara isiwe mishahara ya wakubwa kunyanyasa wale wadogo, na wale wanaopata nafasi kubwa wasijaribu kunyanyasa wadogo. Kuwe na uhuru wa kuandikwa mahali popote, mtu anaweza kutafuta kazi kule anayejua, na pia kuwe na heshima kati ya wasichana na wavulana na mahali popote wanapokwenda kuandikwa kazi waseme wakinyanyaswa, yaani kutaka hiki na kile ndio wapate kazi. Hilo kazi ikitolewa imetolewa kwa kila mmoja kwa njia halali. Tena hii serikali yetu ya majimbo isitoke kwenda kwa jimbo lingine.

Na pia watu wanapoandikwa wasiletwe kwa jimbo lingine ama district ingine kuje kuandikwa kwa district lingine maana pia sisi tumepangiwa watu wake wale watakaoandikwa. Jaribu kuioletewa watu kama kiongozi tuko pale wa jimbo lingine ama district nyingine alete watu wa kwoa na kuweza kuwaweka hapa, na pia mashamba iweze kuwa isipeanwe au kuuzwa bila watu, waridhi wale wanavyo bila idhini yao na pia mali kama shamba itunzwe bali iwekwe kama rehani tu na ikitaka kukombolewe, ikombolewe.

Na pia isiuze nje ya jamii ijaribu kuuzwa ama kupeanwa kwa jamii ile ya wale wanaohusikana na uridhi huo. Kwa hivyo pia ningegusia kidogo kati mengi mhesabu wasichana wawe wakipata urithi kutoka kwa wazazi wao, ikiwa ni sehemu ndogo au ni sehemu gani akiwa hajapata nafasi ya kuenda kuolewa basi awe na mahali anaweza kujenga na kustawisha maisha yake. Nafikiri sitakuwa na mengi zaidi, hayo ndiyo ambayo nilikuwa nayo na Mungu awabariki.

**Com Salim:** Asante sana bwana Demeritus Mwasi kwa maoni yako, sasa namwita bwa Nicodemus Kududi.

**Mr. Nicodemus Kududi:** Asante mwenyekiti, kwa majina naitwa Nicodemus Mgeni Kududi kutoka Ugazi location. Nimefika

kuform hii memorandum na kwa hivyo nitaeleza tu kwa muhtasari kwa sababu nimeandika kwa kingereza na kiswahili kwa niaba ya mwenzangu. Kwanza nigelisema ningependa kusema hivi, katiba mpya ningetaka iweze kuwa na azma ya kusema itaongozwa na kikundi gani. Ningependekeza kwamba iendelee kuongozwa kwenye kipindi ya kidemokrasia iweze ikasema kwamba tatu liko na nia ya vyama vyote na siwazi kwamba itakuwa ni demokrasia inahakikisha hakuna watu.

Pili, filosofia ya nchi hii iendelee kuwa ni filosofia ya msingi ya kiujamaa yaani communalism kama ilivyopendekezwa katika Sessional Paper namba 10 ya 1965. Na ikiwa ni hivyo basi, ni kwamba filosofia hii iendelee kutilia mkazo filosofia ya harambee. Kwa hivyo, basi harambee ambazo ni kuungana kijamii tuijendelee maanake tusiendelee kama vilivyo sasa. Kwa hivyo basi serikali isitumie harambee kama chombo ya kupata pesa kutoka kwa wananchi bali harambee ziweze kusaidia katika mambo mengine katika kusomesha ama kutoa matibabu, sivyo. Umuhimu wa katiba hii kwamba katiba mpya itakavyotengenezwa kwa vyovyote viwayo hivyo isiweze kugeuza na yeote yule isipokuwa na wananchi wenyewe. Yaani pawe na national referendum ikiwa hii katiba itataka kubadilishwa.

Haya pili, je tuwe na bunge aina gani? Ninapendekeza kwamba tuwe bunge aina mbili. Tuwe na house of representatives na tuwe na senators wao wawe wamechaguliwa na wananchi.

Pili, napendekeza kwamba aina ya serikali tutakayokuwa nayo isikuwe ya majimbo. Iwe ni serikali ya umoja tu, siyo ya majimbo. Maanake, serikali za wilaya ziweze kupewa uhuru na mamlaka zaidi ya kujitawala. Hivyo basi ikiwa tutakuwa na serikali moja napendekeza kuwe na makao ya rais wanaishi na waziri mkuu. Pili, wanaweza kugawana mamlaka, kama ilivyokuwa katika katiba ya 1965.

Pia, napendekeza kwamba wizara ziweze kuwekwa idadi yake na katiba, sio tunaambiwa kila siku wizara hii wizara ile, sasa kuna wizara 18 sita zikae.

Pia ninapendekeza ya kwamba rais atakayechaguliwa awe ametawala kwa vyama viwili basi. Asipitishe na rais aliyomo sasa katiba hii mpya rais aliyoko sasa isimruhusu asimame kisha napendekeza kwamba mali ya umma ama natural resources ambazo tunazo hapa ni kwamba ikiwa tutakuwa na serikali yenye mamlaka, serikali za mkoa zenye mamlaka ama Local Government zenye mamlaka tosha basi mali zake zote zisimamiwe na serikali hiyo. Na ikiwa serikali kuu itasimama basi asilimia 35 ya ushuru kunaotokana na mali gamu iweze kujenga eneo hilo.

**Mr. Kududu:** Thelathini na tano. Kisha pia napendekeza kwamba serikali hizi za mkoa ama provincial administration zitupiliwe mbali kwa sababu hazina maana, zinanyanya watu. Kwa hivyo baasi ikiwa tutakuwa na serikali ya wilaya ambazo zina mamlaka tosha baraza za wilaya zinaweza kufanya kazi viongozi pana na Provincial Administration.

Haki za watoto ni sovereign. Watoto wawe wanaenda shule bure kuanzia class ya kwanza hadi cha saba, wapate matibabu bure, watoto mashulenji wasitukanwe na walimu, ya pili, wasiwe physically, emotionally and sexually abused by teachers. Hiyo itiliwe mkazo kabisa.

Pia, ningependekeza ya kwamba maafisa watakaoteuliwa kama Permanent Secretaries, Attorney General na wengine wengi,

wakishateuliwa baada ya kufanya voting, basi waziri mkuu ama rais asiweze kuwatoa.

Pia napendekeza kwamba uchaguzi wa rais wa nchi pamoja na makamu wake ufanywe wakati mmoja lakini utenganishwe na uchaguzi wa bunge. Kwa hivyo tunaweza kuwa na rais ambaye ni wa chama kingine ama ikawa ni serikali ya mseto.

Ningependekeza mambo mengi lakini kwa sababu nataka niwapatie wenzangu pia nafasi waweze wakatoa maoni yao nipatie nafasi nikakome hapa. Asanteni.

**Com Salim:** Tafadhali bwana Kudundu, mwenzangu ana maswali matatu kukuuliza kupata kufahamu zaidi mapendekezo yako.

**Com Ratanya:** Yes, Bwana Nicodemus kuna kitu moja ningetaka ujaribu kufafanua. Najua tunaposema Provincial Administration tunaweka hata machifu wapangane hapa na assistant chief. Unafahamu hivyo Nicodemus sasa unaposema provincial administration iondolewe kabisa unamaanisha hata machifu na manaibu wao?

**Mr. Kudundu:** Ninamaanisha hivi, ikiwa tutakuwa na serikali zenye mamlaka za wilaya maafisa kutoka baraza za wilaya watakuwa waweza kufanya kazi ile ya chifu na assistant chief.

Pia napendekeza kwamba utamaduni, desturi na mila zetu ziweze kuhifadhiwa. Kwa hivyo basi, kuna mambo mengine ambayo hayatakikani kwenda kortini, tuwe na korti za wazee ambazo pengine zingekuwa chini ya baraza la wilaya. Pia nigependekeza hapo kwamba ikiwa kuna ubaguzi wa aina yejote ama unyanyasaji wa aina yoyote basi tuwe na ofisi ya ombudsman iwe ikisiliza malalamishi ya wananchi. Asanteni.

**Com Ratanya:** Asante bwana Kudundu , sasa nitamwita Bwana Sospeter Shake, nafikiri amefika, headteacher Nangawa High school. Karibu.

Procedure is very simple; utakaa hapo utatupatia jina lako ili tunase jina na maoni yako pamoja na utaendelea kutupa maoni na ikiwa huna memorandum, itakuwa ni dakika tano tu kutoa maoni.

**Mr.Shake:** Asante sana mimi naitwa Sospeter Shake, headteacher Nangawa Secondary School. Nina mengi ya kusema lakini nitaji-limit kwa mambo ya education tu kwa vile mimi ni mwalimu.

Nina pointi tano ambazo nitaeleza kwa haraka. Point ya kwanza, district ya Kenya tunasema kwamba zote tuko sawa katika Kenya; tuna rights sawa as Kenyans but I think huu ni uwongo, especially in Coast Province tunadanganywa mara nyingi kwa upande wa education.

Policy Council: Politicians wanazungumza wanataka University Coast Province but the Coast Province by then, we were treated na lile Mbagathi College.

Ningetaka kusema this subject kuhusu haki ya kuzungumza in public. Secondary schools zinatangazwa in part with secondary schools zinagawanya za district, Provincial and National, kwa nini our politicians are talking about a university when we do not have a national school in Coast Province? Because there is no National School in Coast Province- why are we pretending to talk about a University tunataka tufike hapo juu wakati hapa mbele chini hatujatembea? Asante.

Tunasema kwamba tupatiwe national school na tupatiwe university; every province in Kenya should get a university (**clapping**)

hiyo ni pendekezo la kwanza.

Number two, nafikiri nikitoa mfano labda nitaenda kando against modification. Kuna bomb pale pale naitwa T.T.C. tulidanganywa ati tutapatiwa Teachers Training College. I am saying that it is criminal for a government to be saying that it is giving us TTC while in actual fact there is nothing that it has given us.

**Mr. Shake:** They cheated us that they are giving us the T.T.C. in Taita but actually it is supposed to be starting. I recommend that it is criminal to start a white elephant project. Kenya should not waste money on projects that are not viable.

Number three is Natural Resources: A friend of mine said use what you have to get what yo don't have. Sasa kama 62% of Taita ni wanyama tupu na wazungu wanakuja huku from abroad, napendekeza kwamba ile pesa inatokana na tourism isaidie katika bursary to poor students in Taita Taveta. Nakaza jembe maanake nitaambiwa oh! we paid those people oh! sijui nini. Such kind of language ni ya watoto.

Number four, tunasema kwamba elimu ya bure kwa watoto wenu tutasaidia wavulana na wasichana kupata elimu equally. For example, watasema ya kwamba we are equal then university cut off points tunataka kureduce za wasichana. What is that? Let them be equal with the entry of points. Kwani nini tunasema mtoto msichana aende na for example, sixty six points university na mvulana aende na sixty nine? Tunawaambia hakika ya kwamba nyinyi mambo bado. Tunawaasia mambo bado (laughing). So the cut off point should not be there. It is a wrong decision by the government.

**Mr. Shake:** Entry points for university entrants should be equal for both girls and boys. The Kenya National Examination Council Act is independent just as the Education Act. Lakini kuna marking scheme kwa syllabus na kuna haki mwalimu anaweza kumaliza syllabus akiwa tu mtoto ameketi kwa sababu hawajui subject hizo ni nini. Kwa mfano, English composition unaweza kuandika; wanasema English composition wanasema 350 mpaka 450 words but they accept even 150 words in English, Kiswahili ukiandika 250 tayari ni 25/50 total percent; but now imagine a teacher does not know that he is just going on with the syllabus and the K.N.E.C Act wanasema kitu kama marking scheme.

The Ministry of Education should come out with a booklet for every subject being taught. In fact, just like now this is a syllabus. Vile tunajua hii ni syllabus basi but tunataka kujua vile hii subject ina-mark-iwa hivi because watoto wana-fail because teachers don't know how to go about teaching the subject and the marking scheme.

**Interjection:** .....(inaudible).

**Mr. Shake:** Marking scheme for every subject is different. Asanteni sana.

**Com Ratanya:** Thank you very much (**clapping**). Asante sana Bwana Sospeter Shake kwa maoni yako. Akiwa ni headteacher waona ya kwamba maoni yake yote yanahuu elimu na jinsi ambavyo elimu yaweza kustawishwa zaidi. Na sasa namwita mwenzake bali ni Deputy wake, Bwana Kariuki. Yuko? Sijui kama maoni ni hayo hayo mengine tutayasikia. Haya asante.

**Mr. Kariuki:** Asante sana, Bwana Commissioner. Mimi ni Patrick Kariuki, Deputy wa Shake na Shake ameongea mambo ya elimu kwa hivyo sitarudia. Kwanza ningetaka kukosoa hii tume kwa sababu tukipatiana maoni hapa kama common man sababu katiba inatakikana itengenezwe na common man. Tunasoma katika magazeti kwamba whenever wanaandika mambo ya vile mnaendelea, mambo ya constitution the points of the common man are not being highlighted. We are just getting Mister so and so, mbunge so and so amesema hivi kuhusu katiba.

Kwa hivyo, we are wondering, will the common man have a true ownership of the final product because saa hii hatusikiki; kwa magazeti ya keshoitakuwa amesema hivi serikali yake inatakiwa kuwa hivi, anataka kuwa hivi. Tunaona tu kama vile nimesema mbunge fulani amesema hivi, mbunge mwininge fulani amesema hivi. Kwa hivyo tunataka hii tume ikienda pale ipeleke yale maoni ya common man. Nikija kwa maoni na mependekezo yangu kwenye katiba, I would say the constitution's amendment should be a continuous process, because like now they are talking of 'we will not have elections before we finish the making of a new constitution. I am wondering because we are a dynamic society, tunabadilika, the environment is changing.

The year 2003 might not be the same year now because we are in the process of development and may be the way we would want to be governed in the year 2003 is not the same as we would like now. So we would like constitution making to be a continuous process. Serikali iunde commission ambayo itakuwa permanent. Tukipata jambo fulani tunabadilisha hiyo katiba, kwa hivyo isiwe static.

Halafu ningependekeza kwamba uchaguzi, kwa sababu nimesema constitution making should be a continuous process, so the elections should be held as scheduled. The elections should not be changed because it will be postponing problems. I mean tutakuwa tunapeleka matatizo mbele.

I would also like to say that we should have a Parliamentary system of government, where MPs have the full authority of the government thus they should themselves elect or appoint a Prime Minister who should come from the party with the majority members of Parliament.

So MPs should also serve for 4-year terms, not 5 years so that they should not stick in that seat in particular because we are giving them some work and mandate wafanye miaka minne tuone vile wanafanya. Lakini Prime Minister afanye miaka mitano ili wale ambao tumewaondoa kulingana na vile anaofanya kazi yake waone kama watamrudisha ama hawatamrudisha. Na hawa MPs lazima wapate consent from the common man. The President should be there but ceremonial. He/she should act as a unifying factor who should come or rather should not be biased along tribal lines.

The Provincial Administration and Local Authority should stay. This is in order to devolve power to the local level because tukiwa na MPs, Prime Minister, President huko juu hapa chini hatutakuwa na kiongozi kwa hivyo ningependekeza kwamba provincial administration and local authority should stay so that we have that power brought back to the people.

Parliament should be given powers to appoint senior government officers like the Permanent Secretary, Controller and Auditor

General and Chief Justice because MPs have been elected by the people. So if they elect themselves they should also elect also senior government officers.

The government officers, because they are answerable to the people who are taxed and are financing the government, will then be said to have been appointed by the people themselves.

Tukija upande wa elimu tunasema kwamba elimu katika primary level iwe free. Hiyo ningetaka kusisiIza kwamba it should be like that and once you talk of education you should also talk of medical attention for the school children.

So I would say, ningetaka kupendekeza kwamba watoto wote kutoka mwenye amezaliwa, day-old infant to six years, wawe wanaenda hospitali bure wasilipishwe pesa yoyote; wawe wanaenda pale bure.

Halafu tungetaka mambo ya family planning, kila mzazi awe anasaidiwa na serikali kuwasomesha mtoto wake wa wa kwanza na wa pili mpaka university level or mpaka mahali anataka kufika; wa kwanza na wa pili, kwa sababu hawa wazazi ndio wanafanya kazi huko chini wanakuwa taxed, the money is going there but they are not getting this money coming back to develop the common man (clapping).

**Com Ratanya:** Thank you Bwana Kariuki. Samahani Bwana Kariuki jina lako la kwanza ni?

**Mr. Kariuki:** Patrick.

**Com Ratanya:** Patrick, asante. Sasa tunamwita Bwana Vermont Lubindi. Vermont Nyamu Lubindi.

**Mr. Lubindi:** Asante sana Bwana Commissioner. Kwa jina naitwa Vermont Nyamu Lubindi. Nimeandika memorandum, kwa hivyo nitasema yale ambayo ni ya muhimu kwa vile mmesema kweli.

Niaanza na amri ya katiba tunayoitaka na majibu ambayo mmepewa mawili ambayo mmeuliza ya kwanza kwa mfano mambo ya preamble. Mnasema ya kwamba the constitution of Kenya should have a preamble indicating that Kenya is an independent, multi-ethnic, multiparty and multi-religious republic.

In trying a constitutional supremacy of the people and the rule of law in which all the citizens are equal and in state policy, I have said that the constitution should clearly state that the people of Kenya have the right to choose and to participate individually and collectively in the planning and implementation at all levels of their governance.

Kumaliza hapo nitaenda kwa constitution. Katiba ya 1963 ya uhuru ilikuwa ni katiba ya majimbo. Haukupewa nafasi ya kufanya kazi kwa sababu kulikuwa na sababu, chama ambacho kilikuwa kinatawala wakati huo hawakutaka majimbo. Mimi napendekeza kwamba nafasi itolewe kwamba system ya serikali isiwe ile ya majimbo, federal government, na tuwe na system zote za kidemokrasia kutoka juu mpaka sub-locational level. Tuwe na bunge mbili, Senate na House of Representatives. Tuwe na local authorities ambazo zina nguvu zao, na zipatiwe usaidizi kutoka kwa serikali kuu.

System zote za Kenya ziwe ni za kidemokrasia na hapa tunamaanisha ya kwamba vyombo vyote vya utawala viwe ni vya kusiwa na wananchi. Sasa mkoloni alipokuja Kenya aliunda vyombo ambavyo vilikuwa ni vya upingamizi. Chombo cha kwanza ambacho mkoloni alileta ni Provincial Administration. Chombo hicho hakijui kwenda hand in hand na demokrasia. Kwa hivyo kama hatutakuwa na demokrasia kutoka juu mpaka village level, system ya provincial administration iondolewe. Wawe watu wa kuchaguliwa na kama hata watakuwa na wajibu wawe ni watu wa kuchaguliwa na wawe na muda karne amba watahudumia sehemu zao, wasiwe ni watu wa civil service .Ili kuondoa utatanishi katika serikali, napendekeza kuwe na afisi ya ombudsman.

Parliament iwe na time schedule itakayojulikana kabisa, tarehe ya uchaguzi itakuwa lini, uchaguzi usiwe ni siri ya mtu binafsi; na Parliament iwe huru kutoka kwa executive. Napendekeza pia kuwe na President ambaye anataka mamlaka yagawanywe kati ya President na Prime Minister. Na Parliament iwe na power of impeachment.

Civil service should be independent of political patronage, vyama vya kisiasa, vile na mwandishi maalum ambaye amepewa uwezo wa katiba- registrar of political parties- kwa sababu hivi sasa vyama vya kisiasa vinaandikishwa kwa sheria ya society Act. Hiyo ni sheria ambayo inatawaliwa na serikali. Kwani kukiwa na mwandishi ambaye anatokana na katiba yenewe, Registrar of political parties, basi vyama vyote vya kisiasa vitakuwa hapo viwe vinatawala viwe havitawali itakuwa sawa na nyingine. Huyo Registrar of political parties awe uhuru kwa sababu hivi sasa tume hili inafanya civic education lakini ikiondoka civic education itakuwa ni kazi ya nani? Napendekeza kwamba hiyo ofisi ya Registrar of political parties iwe responsible kwa civic education.

Wakenya wote wanafaa wawe sawa mbele ya sheria. All Kenyans should be equal before the law. Na all party office holders should declare their assets before they are appointed.

Ardhi, land ownership should be categorised. Mtu binafsi asiwe na zaidi ya acre 30, halafu ziwe ardhi za families, ardhi za kampuni na kadhalika, lakini zote ziwe categorised na acreage should be fixed. Na ardhi ambayo haidumiki mtu anachukua ardhi nyingi, kubwa na haitumii, that land should be taxed. The President should be non-partisan. Mtu akishachaguliwa kuwa President basi asiwe ni wa chama fulani and he should not be a representative of any constituency, awe member wa senate by virtue of his office.

Judiciary, kwa sasa watu hawapati haki ya kutosha kwa sababu korti ya vikosi. Na ninapendekeza kwamba kurudishwe kama vile korti za zamani, the elders court, ili watu waweze kupata haki right down to community level. Mwanachi asikose haki kwa sababu hana pesa za kulipia wakili, serikali imsaidie.

Security, the police should organise and provide security right down to community level.

Sasa tumefika haki za wanawake. Wangaliwe so that they can die in dignity. Mara nyingi nashangaa kufika mahali ambapo kunazungumzwa habari sana za haki za wanawake. When we extend that it appears kuwa kuzaliwa mwanamke ni kuwa disabled. Now, I think it is too much. Lakini mwanamke ni mwanadamu kama vile mwanaume. Mimi napendekeza ule usawa.

Si maajabu tuwe sawa. Sio ati mwanamke awe hivi kila siku aongozwe vile. Kwa nini hawawezi kuwa encouraged wafanye mambo kama wanaume? Siku hizi wanaenda skuli sawa sawa wanapita masomo sawa sawa, ardhi wanapewa sawa sawa. Kwa hivyo, they should only be encouraged to work hard like men sababu najua wanawake kama Margaret Thatcher I have known them to be dependent. They have always competed like anybody else. Kwa hivyo, wanawake wapewe nafasi ya ku-compete na wanaume.

### **Interjection...(inaudible)**

**Mr. Vermont:** Na ya mwisho ni kwamba kazi ziwe one man one woman one job. Kuna mara nyingi watu wengine wanapewa kazi nyingi na wengine hawana. So there should be one man, one woman job and such (**clapping and laughing**)

**Com Salim:** Huenda mwenzangu akawa na swali la kuuliza.

**Com. Ratanya:** Hapo ulipoongea mambo ya mashamba, ukasema ya kwamba kuwe na ceiling ya 30 acres, unamaanisha hiyo iwe general kwa sababu kuna pahali watu wana mashamba mengi, wengine wangesema ceiling iwe 100, iwe 1000 na kuna pahali kuna mashamba madogo. Sasa ile 30 acres yako ni ya kila pahali katika Kenya ama sehemu mbali mbali au sehemu fulani?

**Mr. Vermont:** Mimi nasema kama ni individual mtu mmoja iwe ni 30 acres kila mahali.

**Com Ratanya:** Asante sana na sasa tutamwita Bwana Peterson Mburu.

**Mr. Mburu:** Asante Bwana commissioner. Jina langu ni Peterson Mburu si subaru. Nimeandika memorandum na nitaisoma. Nimesema kwamba katiba isibadilishwe tu na watu wachache bali ibadilishwe kwa memorandum, watu wote wahusike wakati mabadiliko inafanywa. Badala ya wananchi kugawa vitambulisho hivi I.D. card tuwe tunapatiwa, serikali iwe inatupatia passport sababu imekuwa kila wakati mtu akitaka passport mwingine amemaliza miaka miwili, miaka mitatu asipate hiyo passort na hali alitafuta kihalali. Hii ni kibali anastahili kuwa nacho.

Katika serikali yetu ya Kenya usikuwe ngumu kwa mfano ina mamlaka zaidi kuliko zote. Mashirika ambayo si ya kiserikali yaye yakichunguzwa wakati haya jaandikishwa sababu tuna mengine ya kidini na mengine ni ya kitofauti kitofauti yameandikishwa na tena yanalettea watu mambo kwa mfano, sasa hivi tunasikia kuna devil worshippers. Tunashangaa ni nani aliwaandikisha waendelee kufanya kazi kama hiyo. Rais akue chini ya miaka hamsini sababu yeye ni kama mzazi. Sasa akiwa chini ya miaka hamsini watu wengi watakuwa wako zaidi ya umri wake atawezza kuzungumza kama rais.

Pia mawaziri wasiwe chini ya miaka arobaini. Kuna watu ambao wanazaa watoto halafu wakishazaa watoto hao wanaume wengine hupotea. Huenda pahali amehamia Tanzania ama Uganda halafu wanakaa tu na hawajui vile watoto wako wanaendelea

halafu wakizeeka wanarudi Kenya wanakuja kutunzwa na hao watoto wake. Iwe ni lazima kwa mtu akiwa na watoto kuwalea na kuwafundisha.

Halafu pia kuna tabia ingine ya wazazi, wengine hawana mahali pa kwenda hata wakihama hiyo nyumba. Kuwe na sheria ya kulazimisha wazazi kuwachunga na kuwapa watoto haki zao. Nafikiri hata hapa nime-suggest kuwe na mavazi ikiwezekana ya kitaifa.

Kuwe na chombo maalum cha kuangalia masilahi ya wabunge. Wabunge hao wasiwe wajiangalie masilahi yao wenyewe kwa mfano majuzi wabunge walijiongeza mshahara kupindukia kiasi. Wakati wafanyi kazi wengine na serikali wanakosa mishahara ukiangalia wengine watu ambapo wanashughulikia watoto-walimu-wakipiga makelele wakitaka waongezewe mishahara amba ni halali walikuwa wameahidiwa. Lakini wanakosa kwa sababu serikali haina pesa lakini wabunge wakajiongezea. Sasa unashangaa hii ni Kenya gani? Ningalipenda kuwe na chombo maalum ambacho kinachunguza mishahara ya wabunge wasijiongezee wenyewe.

Kila mwananchi atoe kodi asiweke udhaifu. Watoe kodi hii itasadie kila mtu kulinda mali ya umma. Badala ya mwenyekiti wa kijiji tuwe na wenye vijiji wa nyumba ishirini. Hii itasaidia sana kuangalia na kujua usalama wa wananchi zaidi kwa undani. Kwa sababu mwenyekiti wa kijiji anaangalia watu wengi sana. Nyumba ni nyingi sana zinamficha hata hawezi kujua ni wageni wangapi wako hapa ndani, nyumba ziko na matatizo mangapi. Ukumuuliza hawezi akajibu lakini tukiwa na wenye vijiji wa nyumba ishirini nao wanaweza kuwa na uwezo wa kujua zaidi na pia wawe wakilipwa na serikali ya mitaa. Lakini hao wachaguliwe na wananchi. Asante bwana mwenyekiti.

**Com Ratanya:** Asante sana Bwana Peterson na sasa namwita bwana Gamalil Mwamidi.

**Mr. Mwamide:** Mimi naitwa Gamalil M. Mwamidi kutoka Weruga. Naanza na tatizo sugu sana ambalo limeharibu nchi hii. Rais asiwe mbunge, achaguliwe na wananchi wote kutoka jamhuri ya Kenya. Akuwe na mamlaka kama ipasavyo, asiwe na mamlaka ya kuchagua mkuu wa sheria maanake haki huwa haitendeki maanake mkuu wa sheria lazima afuate rais. Jambo lolote akitaka hata kwa uamuzi lazima angalie mtu ambaye amemteuwa kwa hivyo hatakuwa na independent mind. Asiwe na jukumu la kubuni tume. Kwa mfano, Rais Moi amebuni tume nyingi; wage report, tume ya clashes, ya mwabudu wa shetani, lakini akiona imetoa maamuzi na ikague wao that is it. Mwishowe inaenda katika dustbin na inawekwa huko na haitumiki. Kwa hivyo, bunge iwe ina uwezo na mamlaka ya kuteuwa tume kama hizo. Na pia rais asiwe na mamlaka ya kuteuwa kama amri jeshi na asiwe mkubwa wa jeshi na polisi maanake kwa muda mrefu tumeona wezi wanaachiliwa, wale watu wanapora nchi wanaachiliwa lakini mtu ambaye anavita vya mdomo kuunda kufanya mkutano tu. Mkutano unaenda unazimwa baada ya dakika tano. Lakini wale waporaji nchi wanaachiliwa. Kwa hivyo asiwe na hayo mamlaka. Halafu pia asiwe akiendesha nchi na maazimio ama decrees. Anaweza amka asubuhi aseme kitu fulani ifanyike hivi, kwa mfano kama kujenga Eldoret Airport hii ni pesa haikupitishwa na bunge. Yeye anaamka tu asubuhi anasema kuwe na kitu fulani kwa hivyo ziwe recorded hizo decrees. Halafu kuwe na kura ya maoni. Pakiwa na jambo lolote ambalo linahitaji national referendum wananchi waulizwe maoni na

watoe.

Halafu ma-County Council yapatiwe ama serikali zipatiwe mamlaka kama vile ilikuwa kabla tume ile hajabuniwa ya kamli. Maanake wakati ule kulikuwa na barabara, kulikuwa na ma-ambulance, kulikuwa na trailor ya kutengeneza barabara; kwa hivyo zirudishwe.

Halafu pia kuwe na office ya ombudsman kama nchi zingine kama Sweden na Uganda maanake kuna shida polisi akikufanya kosa leo akienda huko unaenda unaogopa. Anatetewa na mkubwa, kukiwa na ofisi kama hiyo ama chief akikufanya makosa anaenda anatetewa na D.O. ama D.C. kwa hivyo hakuna pahali pa kwenda. Kila pahali ni kitu kingine kukiwa na hiyo ofisi ya mlizo au ya ombudsman hiyo itatetea.

Halafu kusiwe na Provincial Administration; machief, ma-assistant chief na wote kuendelea huko juu, maanake hiyo sheria ilibuniwa Uingereza na hata wao hawana hiyo provincial administration ilikuwa hiyo tu njia ya kutugandamiza. Halafu wananchi wapatiwe uhuru; mbunge kama hafanyi kazi sawasa wamtoe na wachague mwengine. Asiwe na nguvu... (**clapping**)...na pia awe anauliza wananchi maswali asiamke asubuhi anaenda kusoma tu; wananchi wamemtuma na hajatumwa. Anafaa aketi na sisi wananchi tumpatie kazi ambayo ataenda kutufanya.

Halafu pia mbunge asiwe waziri na mawaziri pia wawe na taaluma maalum sio kama wakati mwengine tunasikia Moi anaamka asubuhi anasema tunataka, nimemchagua waziri fulani. Mtu wa ujuzi wa askari unamweka kuwa waziri wa afya! Kama ni elimu waziri awe ni educationist (**clapping**).

Na wakati wa kubadilisha mamlaka ama wakati wa uchaguzi tunataka tuwe na national Calendar. Mtu mmoja asiwe na siri ya siku ya uchaguzi. Kuwe na national calendar kama nchi zingine kama America. Ni sawa sawa na kwenda kucheza mpira iwe uko tayari, wewe ndiye referee na unapiga firimbi hatujavaa kanzu unapiga firimbi tuenze mpira; hiyo unayo hatutaki. Iwe inawekwa kwa calendar.

Halafu pia legal tender, pesa ziwe na kichwa ya founding father kama America; pesa iwekwe kichwa ya founding father tuwe kama nchi zingine.

Halafu kuwe na sera ya kilimo, National Policy ya kilimo maanake kwa wakati huu tutoe mfano, ukambani magunia sasa la mahindi ni shillingi mia mbili na Watanzania watanunua. Wanakuja kununua saa hii na mwezi wa tisa tutaanza kuuziwa Taita Taveta. Na huko North Eastern watu wengine wanalala njaa; ikiwa hivyo tuwe na hali kama hiyo ya kutetea wakulima na pia tuwe na mikopo mashirika kama A.F.C na mengine yakupatia wananchi mikopo.

Na pia vile vile serikali iwe na pesa ya kununua mahindi, kama ni mahindi; vifaa vyote vya kilimo hata kama mali imefirika wanunue. Kama ni maziwa yawe powdered. Kama ni tomato halafu mali ukifurika mwananchi anakufa moyo kama vile Trans Nzoia saa hii wananchi hatulimi mahindi. Maanake hakuna watu wakununua. Na huko North Eastern watu wanakufa njaa kwa hivyo kuwe na uhuru pale.

Halafu katika katiba yetu kuwe na specific economic policy, tujue kama ni ya capitalism ama socialism na maana yake. Hapa Kenya utakuta mtu mwengine anaweka let us say plots, unakuta ana plots hata mia moja na kitu na mwengine, ukienda hata

Mathare, hana plot hata nyumba ya kulala kwenyewe ni ya box akilala akijinyorosha mguu, mguu inafika kwa jirani. Hali kama hiyo hatutaki.

Halafu ingine ambayo ninaona ni ya muhimu sana japo sijui watu wataichukulaje, katika pato la taifa, annual budget, tuwe na fungu la kumi, 10%, iwe inafanya kazi ya Mungu ndio nchi yainuka. Haiinuliwi na Mungu.

Halafu katika uchaguzi usiwe unaunganishwa; ule wa wabunge na wa urais utengwe. Maanake watu wengine wanabebwa tu kama upepo. Mgomea kiti wa urais awe ametimiza asilimia hamsini; sio kama wakati ule wa 1997 wakati alipata 35% na the rest walikuwa wanaongozwa na mtu ambaye alipata 34%.

Halafu kuhusu ardhi, Commissioner wa ardhi apatiwe mamlaka ya kugawa ardhi huko Nairobi; asitupangie mambo huko juu. County Council zipatiwe huo uamuzi wa kugawa na wananchi maanake wao ndio wako na wananchi.

Halafu kuna hizi District Development Committees. Mimi naona ziondolewe kabisa maanake DDC si mwananchi ambaye anaketi hata Councillor akichaguliwa mwisho yake ni sub-DDC; hana sauti huko; ni mwenyekiti peke yake huenda. Kwa hivyo watu ambao wanaenda kuketi huko pengine mtu ametoka Meru huko, si sehemu za hapa, yeye ndiye anaenda kuitisha mambo. Kwa hivyo, hizo zote ziondolewe.

Halafu mkaguzi mkuu ama mhasibu mkuu, Auditor General, asiwe anachaguliwa na rais bali achaguliwe na bunge. Maanake ndiyo atafanya kazi vizuri.

Halafu wale watu ambao wameharibu misitu unakuta kama Moi na watu wake wameharibu misitu yote hizo zote zirudishwe mwananchi.

Halafu pia kuhusu hali ya usafiri, matatu, I think we should borrow a leaf from Uganda, matatu ikijaa, basi hauwezi kuingia. Ikijaa basi hata uisimamishe njiani haiwezi kusimama ili kuzuia ajali. Pia kuwe na mbinu maalum za kuwacharge watu kodi. I mean kama nauli, maanake Kenya kuna tofauti pahali pengine kwa shilingi ishirini unaweza enda mpaka uchoke na pahali pengine hapo pahali ambapo utaenda pa shilingi ishirini ortalipa sabini. Kwa hivyo tuwe na mpango maalum Kenya nzima.

Na mwisho ni kuhusu mahakama na majudge wawe wanateuliwa na mbunge sio rais maanake hawatafanya kazi. Siku ya uchaguzi anapigiwa simu anaambiwa ‘wewe amua hii kesi sisi tunataka hivi’ sasa anaogopa. Kusiwe na mwingiliano.

Nafikiri sina mengine isipokuwa nyinyi watu wa tume mimi kitu ambacho nitasema, siombi, mimi nadai haki yetu. Mkimaliza hii hatutaki mwende State House mwende mle sima halafu mharibu hii maoni yetu maanake huo ndio umekuwa mtindo.

**Com Ratanya :** Asante bwana Mwamidi kwa maoni yako. Nafikiri hayo ni maoni kwa niaba ya chama chako binafsi.

**Mr. Mwamidi:** Binafsi.

**Com Ratanya:** Nafikiri mwenzangu ana swalii moja ama mawili; Bwana Mwamidi ungejaribu? Okay. Bwana Gamalil Mwanamidi is it? Kuna swalii moja tu lakini ni ya kufafanua na hii ni kuhusu annual budget. Ulisema kwamba annual budget iwe 10%. Sasa unaweza kufafanua hiyo 10% ni ya kwenda wapi? Kwa wananchi ama wapi?

**Mr. Mwanamidi:** Nilisema 10% katika annual budget wawe wanatenga 10% ya kufanya kazi yoyote ya Mungu au ya makanisa. Watakuwa na mpangilio iwe inafanya kazi gani ya Mungu maanake pesa ni za dhahabu na ni za Mungu. Malaki mbili naninasema namna hivi fedha ni dhahabu na ni za Mungu. Kwa hivyo, taifa letu kama tunataka liinuke ni lazima tuhusishe Mungu hata kwa pesa zetu ndio taifa litainuka.

**Com Ratanya:** Asante Bwana Mwamide na sasa namwita Irene Risambio. Risambio ni dada wa kwanza kutoa maoni yake; tungependa kina mama wengi zaidi waje mbele ili tupate maoni yaliyo na balance kina mama na kina baba. Karibu.

**Ms. Irene Risambio:** Jina langu ni Irene Risambio. . Nitasoma kulingana na vile tuliani tukiwa wanawake wa group. Kwanza, tunahitaji katiba iwe na mipangilio kamili ya demokrasia.

Elimu iwe ni ya bure kuanzia nursery hadi darasa la nane. Mambo ya kutoa gharama yaondolewe.

Haki kwa wanawake, wanawake wajipangilie kwa njia yoyote na wapewe idhini sawa na wanaume, awe ameolewa ama bado. Maana, anayefanya kazi akipata maternity leave ajibu. Mama anapoitenga na bwana, yapaswa wagawanye mali sawa. Mali yeoyote itakayotafutwa na bibi na bwana kwa kila kitu ya mama na bwana yuko karibu, kama school fees.

Kwa mfano, kunyima watoto school fees ni kama hata title deed kwa sababu ingekuwa na shida hapo nitatoa mfano kwa sababu imekuwa na shida mbali mbali. Labda huyo bwana ameachana na girlfriend yake akioa bibi mwingine itakuwa kama ilikuwa ni Mr. and Mrs bibi mwingine na muhuri na itakuwa ni mahali ambapo hatuna mwelekeo mzuri.

Halafu, watu ambao wanasantaza ukimwi makusudi wafungiwe mahali pao na kuishi kwa hospitali. Halafu kuna baba ambao wanafanya mapenzi na watoto wao. Baba anayefanya mapenzi na mtoto wake kifungo haswa anapaswa akatwe sehemu zake za kisiri. Halafu muda wa msichana wa kuolewa. Baba akioa msichana mwenye umri wa miaka chini ya miaka kumi na tisa ahukumiwe. Halafu kuna wasichana wanaowekwa mimba wa shule. Msichana wa shule akiwekwa mimba na mwanafunzi wa shule wanafunzi hao wote wawili wafukuzwe shulen halafu wazazi wa msichana au marafiki wachukue gharama ya yule mtoto na elimu yake hadi atakapofikisha miaka kumi na nane.

Halafu kuna mapenzi ya nguvu baina ya baba na mama. Baba akifanya mapenzi na mama kwa nguvu kwa njia isiyo halali yafaa ashtakiwe kunajisi. Mtu anajisiye mwenzake, awe mwanaume awe mwanamke, ahukumiwe na nchi kifungo cha maisha. Kunajisi sio ati mwanaume ananajisi mwanamke peke yake; hata wanawake hunajisi wanaume.

Halafu haki za watoto, mtu akiajiri mtoto chini ya umri wa miaka 16 serikali iangalie sababu gani mtoto huyu anaajiriwa maana yake ingekuwa mtoto hana wazazi ama yule mtoto ako na wazazi lakini wazazi wake hawajiwezi inabidi huyo mtoto aajiriwe ili asaidie familia yake sawasawa.

Halafu uongozi wa Councils, wanawake wawe na usawa na wanaume sehemu moja kwa kazi.

Machifu wachaguliwe na wananchi pamoja na wafanyakazi wa mitaa kwa vipindi vyta miaka miwili na mayor na mwenyekiti nisawa tu.

Halafu kwa mbuga, misitu na madini. Pesa ambazo zinaletwa na watalii, mbuga za wanyama na misitu pamoja na uuzaaji wa

madini ziletwe na serikali za wilaya baadaye zipelekwe shulen i kama bursary ya kusomesha watoto. Wabunge wasitoke katika familia moja kwani imekuwa kwa mfano atoke katika kabilia fulani.

Rais awe akichaguliwa kutoka kabilia tofauti tofauti si weny kabilia moja inayotawala kila wakati. Halafu upokeaji malalamishi, afisi ikuwepo ya mpokeaji malalamiko na uhusiano na kujua vile makao yanavyoendelea. Kwa mfano kuwe na tume ya ardhi. Hasa kwa upande wa Taita Taveta, sisi tumekuwa hatuna mpokeaji mlalamishi hapa. Kwa hivyo asanteni kwa hayo machache.

**Com Ratanya:** Asante Irene Risambio kwa maoni yako na tutapokea memorandum yako. Sasa namwita Mary Njumwa.

**Ms. Mary Njumwa:** Kwa jina mimi ni Mary Njumwa. Maoni yangu kwa katiba: Jambo la kwanza, ningependelea wakati wote wa kufanya marekebisho katiba mwananchi aweze kujihusisha.

La pili, kutokana na ile katiba tulionayo sasa, kama wananchi wa Kenya inawaruhusu kwishi mahali popote nchini Kenya. Mimi nasema kuwa kila mtu aishi mahali kwao. Nikimaanisha kuwa kuweko na serikali ya majimbo na serikali hizo ziwe za kidemokrasia ya haki kwa wote.

Fungu la tatu, mpunga zetu za wanyama wa pori zibadilishwe ziwe Game Reserve ya wataita baadala za national park, na pesa hizo za national park au Game Reserve ziingizwe katika County Council zetu za taifa ili zifaidi taifa kwa mambo kama bursary za shule, utengenezaji wa barabara zetu za Taita Taveta, kupata maji ya kunyunyizia mashamba yetu kwani mvua hapa Taita ni haba sana.

Mashamba hayo ya mbuga ya wanyama ipatiwe wananchi wa Taita Taveta na robo moja itakayobaki iwe ni Game Reserve na mashamba hayo yatolewe pamoja na title deed.

Ningependelea kuongea juu ya masomo ama elimu. Huu mfumo wa elimu tulionao sasa uondolewe na kurudishwa ule wa zamani, standard seven, form four, five and six na miaka miwili ya university.

Pia shule zote za private zifungwe, zibaki shule za umma. Shule zote za umma zifanyiwe marekebisho ili zihudumie mtoto ye yote yule wa Kenya. Kuendelea kuwa na shule za private ni kusema kutakuwa na shule za matajiri na za masikini. Elimu yote iwe bure.

Hospitali zote za private zifungwe zibaki za umma. Hospitali za private zinasaidia sana ujisadi na kugawanya watu k

wa makundi mawili yaani matajiri na maskini. Ningependa kuwe na serikali ya Africanism na tuwe na ya Capitalism. Matibabu yawe bure kabisa.

Haki za akina mama, kwa mfano kunajisiwa kwa watoto, mama naye mtu akinajisi mtoto wa chini ya miaka kumi na nne basi ahukumiwe kifo, kama ni mtoto yule wa miaka kumi na nne kuendelea basi kifungo chake afungwe kulingana na madhara

amesababisha kwa huyo mtoto. Kuachana kwa bwana na bibi; kama kutatokea kutoelewana kati ya watu hao wawili yaani bwana na bibi, basi malipo tu ikiwa mali ipo wakiwa pamoja igawanywe katikati kwao, pia watoto waende na mama yao na baba watoto awe akiwapatia mahitaji yote kama uhuru bora na elimu hadi watoto hao watakapokuwa wakirudi kwa baba yao kumlinda.

Ulinzi wa miji kati ya bwana na bibi, bibi akiolewa ni lazima ahakikishe mahari kama mfano, ilipwe kama ni title deed liwe likiandika majina yote ya bibi na bwana. Mahakama irudishiwe jukumu la uamuzi wa vita za nyumbani kwani bibi au bwana wanapopigana wanachukulia hatua za kisheria sawa na mtu ye yote aliyejunja sheria yoyote ile ya Kenya.

Lugha zitakazotumika kwa katiba yetu ningependelea ziwe za Kingereza, Kiswahili na hata lugha zote za Kenya ili mwananchi ye yote aweze kusoma na kuelewa vizuri.

Haki za vijana, Mkenya akifanya kazi na ku-retire lazima aondoke na kuachia vijana nafasi.

Asanteni kwa kunisikiliza.

**Com Ratanya:** Asante Mary Njumwa. Yeye ni member wa ile kamati iliyochaguliwa kuwausisha wananchi katika mambo ya katiba na tukiendelea mbele tunamwita Bwana Nathaniel Mukombola.

**Mr. Mukombola:** Kwa jina naitwa Nathaniel Mukombola kutoka Weruga location na niko na memorandum yangu ya binafsi kuhusu katiba iliyoko.

Jambo la kwanza ningependa kugusia ni kuhusu uraia. Raia lazima awe ni mzaliwa wa Kenya na sio mtu kutoka nje. Pia mwanaume awe ni mkenya. Mke akizaa na mtu kutoka nje huyo mtoto asipewe uraia wa Kenya.

Kuwe na idadi ya vyama kama vinne kulingana na matokeo ya uchaguzi. Kuwe na muundo wa majimbo ambapo tutakuwa na bunge katika mikoa, ili isiwe rahisi katiba kubadilishwa kwa minajili ya masilahi ya watu binafsi.

Wabunge wakishachaguliwa wasiteuliwe yyeo vya waziri maana idara zinapewa mawaziri wasio na ujuzi. Hii inasababisha kuanguka kwa uchumi, na maoni yangu muhimu ni kuwa mawaziri wateuliwe wenye taaluma au professionals.

**Com Ratanya:** Samahani bwana Mukombola, naona wasoma memorandum na wakati ni mfupi sana. Huwezi kutupa points zilizomo tu kwa ufupi tafadhali?

**Mr. Mukombola:** Kuwe na wabunge wa kuteuliwa na taratibu za mishahara zilinganishwe. Kuna pango kubwa zaidi kati ya wakubwa na wadogo. Mwenyekiti au mayor achaguliwe na waakilishi kama mia maanake wakichaguliwa na watu wote itakuwa kazi sana. Baraza ziwe bure na zisiwe chini ya serikali kuu. Madiwani lazima wawe wamehitimu kidato cha nne. Baraza iwe na uwezo, haki, maji, national parks na pia uwezo kugharamia karo la malipo yote ya watoto wa primary. Hii ni kuondoa mzozo kwa wazazi.

Watu walioiba pesa au mali ilio zaidi ya shilingi elfu hamsini wasipewe dhamana; matajiri wanaweza kuilipa ilhali maskini wanawekwa ndani.

**Com Ratanya:** Asante Bwana Mukombola kwa maoni yako. Sasa namwita Elizabeth Mwatela.

**Mr. Mwatela:** Jina langu ni Elizabeth Mwatela. Ninatoa maoni kwa niaba ya akina mama wote. Ikiwa msichana wa shule ametoa mimba akiwa shulenii asifukuzwe. Ikiwa mimba ni ya mwalimu basi mwalimu huyo achague kama amuoee msichana huyo ama sivyo akikataa msichana afutwe kazi. Kama hataki mojawapo ya hayo mawili atoe kulingana na mila ng'ombe moja ya kiume na ya kike kwa mamake nyumbani.

Mama akilipiwa mali zote za nyumbani na wakiachana na bwana basi mali hizo lazima zigawanywe kati ya bwana na bibi na ikiwa mama ameachwa na bwana yaani mjane, basi aachiwe mali zote za bwanake. Wanawake kurithiwa hatutaki; wanawake kuridhiwa siku hizi ni vibaya sana. Mama ameachwa na yeye hana ukimwi ataolewa na huyo bwana mwingine ambaye ana ukimwi na huyu bwana pia amuambukize. Mwanaume akimtaka afunge ndoa na atambuliwe wazi na ikiwezekana pia apimwe akiwa na hamu katika jamii yake.

Mwanaume akilala na mtoto wake wa kike basi afungwe kifungo cha maisha na apewe kazi ngumu gerezani.

Maoni ya uongozi baina ya wanaume na wanawake: Wanawake wawe uhuru kuchaguliwa mahali popote. Kuwe na uchaguzi sawa na chochote kila mwanamke awe huru kuchaguliwa. Maoni yangu ni hayo tu, asanteni.

**Com Salim:** Asante sana Elizabeth Mwatela kwa maoni kwa niaba ya Kishushe Women's group. Sasa namwita Bwana Granvile Chawana.

**Mr. Granvile Chawana:** Majina yangu ni Granvile Chawana na ninatoka Mlondi Sublocation, Werugha Location, Taita Taveta.

Yale ambayo nilikuwa nayo ni juu ya National Parks na imaguswa na mtindo huo huo kwa upande wa education umeguswa. Lakini kwa upande wa elimu nafikiri ya kwamba elimu iwe huru kutoka nursery hata kwa standard one mpaka form four.

Nitaongea kwamba wale wanaume au wanawake ambaa wanapachikwa mimba na watoto wanatambatambaa hapa nje ya kwamba, ile Affiliation Act irudishwe ndio wanaume nao wajue ya kwamba ile kazi wanafanya si nzuri sana.

Kuna ingine kwa upande wa local brews. Hii mambo ya watu wa pombe imezidi sana kwa sababu hakuna a regulated period; hamna njia ya kuzuia. Nilikuwa nafikiria ya kwamba pengine ingekuwa regulated kama vile pombe zinazouzwa kwa bars kama Tusker na nini na nini na iwe regulated kwa njia moja; kuweko na clubs at several places ya kwamba wale ambaa wametengeneza vitu vyao wavipeleke mahali pamoja iuzwe huko kama vile soko ya kuuza vitunguu na mboga. Viwe mahali pamoja hili ye yeyote apeleke mali yake pale na auzie pale pale. Serikali inaweza kuwa na njia moja ya kuzuia maafa kama hayo.

Jambo lingine ni kwa upande wa local Council; ziwe local vile neno lenyewe linavyosema.

Inginge ni upande wa mashamba. Vile nilisema ya kwamba hizi mbuga Taita Taveta iko ¾ iko kwa National Parks na hiyo ingekuwa ni vizuri ipunguzwe ikiwezekana nusu, nusu ipewe kwa wananchi wenyewe ambao ni Wataita wapeleke maendeleo huko. Ndio nilisema kwamba mapato yote ambayo yanapatikana yatumiwe hapo hapo.

Wale wanaofanya kazi ingekuwa ni muhima katiba hii iwafanye wao pia waandike watu ili kupunguza unemployment. Kwa hayo, nimefikia hapo. Asante.

**Com Salim:** Asante Bwana Chawana. Bwana George M. Mwanyungu.

**Mr. George Mwanyungu:** Asante Bwana commissioner na watu ambao wamefanya kikao hiki ili tuweze kutoa maoni yetu. Nina maoni hapa ya kibinagsi na mimi ni George Mwajungu.

Pendekezo langu la kwanza ni kuhusu maeneo ya uchaguzi yaani constituencies. Zinfaaa zibuniwe na bunge na sio rais maana maeneo haya yamekuwa ya lengo la kujinufaisha kisiasa na sio kueneza maendeleo kama inavyodaiwa.

Uchaguzi wa mawaziri uwe sawa kwa nchi nzima na sio ati majimbo au wa kikabila. Makamu wa rais achaguliwe na ajulikane wakati wa kupiga kura. Pendekezo langu lingine, wahusika wa ujisadi kwa wakati uliopita na wakati ujao wachukuliwe hatua baada ya uchunguzi wa mambo ya ujisadi pamoja na mkaguzi mkuu wa mapato za pesa za serikali.

Pendekezo langu lingine ni kuwa sheria za kulinda haki na uhuru wa vyama vya kisiasa zigusiwe na unyanyasaji wa chama cha kutawala.

Tume ya uchaguzi ipewe uwezo wa kushtaki wahusika wowote wale watakaopatikana wakitoa hongo au wakitoa vurugu wakati wa uchaguzi.

Pendekezo langu lingine ni kuwa mapato na mali za wabunge, mawaziri, rais na wakuu wa taasisi mbalimbali za serikali zichunguzwe na tume ya kulinda ujisadi na matumizi mabaya yanayotokana na ujisadi huo yajulikane kwa uma.

Pendekezo langu lingine ni kuwa vikao lazima wabunge wawe wakihudhuria vikao vya bunge na iwapo mbunge atakosa vikao vitatu kwa mwezi mmoja mfululizo basi apoteze kiti chake cha ubunge kwa maana wabunge wamekuwa sasa wakihepa hepa vikao vya bunge.

**Mr. Mwanyungu:** Vikao vitatu mfulilizo kwa mwezi moja. Mambo ya elimu ni kuwa rais asiwe chancellor wa vioo vikuu wala tahasisi yoyote ya elimu. Pendekezo langu lingine ni kuwa judge mkuu na mkuu wa sheria wachaguliwe na bunge na kuajibikia wakiwa na mamlaka chini ya bunge.

Pendekezo langu lingine ni kuwa tume ya uchaguzi wa mambo ya ujisadi iwe ikitembelea taarafa hadi mipaka zote za nchi kuelimisha umma juu ya mambo ya matumizi ya pesa za serikali kulingana na mipango iliyoko kwa matumizi. Asanteni.

**Com Salim:** Asante sana Bwana George Mwanyungu kwa maoni yako na sasa namwita Bwana Benson Malugha.

**Mr. Benson Mwalugha:** Asante sana Bwana Mwenyekiti mimi ni Benson Patrick Mwalugha, mzaliwa wa Taita Taveta district sub-location ya Matuu. Hapa nawakilisha memorandum ambayo watu waliketi na wakaandika na naomba niisome vile walivyoandika maana nisiposoma watanilaumu.

**Com Ratanya:** Lakini kwa dakika mbili tu Mwalugha. Dakika mbili na nusu na nitajaribu.

**Mr. Mwalugha:** Asante nitajaribu. Kufuatana na marekebisho ya katiba tulionelea ya kwamba ile katiba ambayo iliyoko ilikuwa inatugandamisha hasa wataita wa Taita Taveta na tukapendekeza mambo yafuatayo:

Kitu cha kwanza ni kuhusu hii mbuga ya wanyama wa pori Tsavo National Park. Tulionelea robo tatu ipatiwe wananchi wailime na ile robo itakayobaki isiiitwe national park iitwe Davida Game Reserve.

Halafu hapo tukapendekeza kuhusu mambo ya serikali tasisi. Tukaonelea ya kwamba kuwe na muungano wa vijiji halafu kuwe na kata, wilaya na jimbo na taifa.

Katika kata, tunaolea ya kwamba tuwe na diwani, wilaya tuwe na serikali za mitaa, jimbo tuwe na wabunge halafu taifa tuwe na rais. Na hapo tukapendekeza kuwa tuwe na Waziri mkuu yaani Prime Minister ambaye ataunda serikali.

Halafu tukapendekeza mipaka ya wilaya irudishwe vile ilikuwa zamani maana tukiangalia, kwa mfano hapa majirani wetu wametusonga sana upande wa juu na upande wa chini.

]Tunapendekeza mawaziri wachaguliwe nje ya wale wabunge amba wamechaguliwa na wananchi.Nitaeleza kifupi hapo. Maana ile katiba iliyoko tunaona ya kwamba kwa mfano, kama hapa Prime kama tumechagua mbunge na akienda pale apatiwe kazi ya uwaziri hawezi kutetea masilahi ya watu wale amba hawako katika upande wa serikali.

Halafu napendekeza utawala wa mikoa uondolewe kabisa.

Halafu hapo kulingana na rasilmali ikawa tunapendekeza ya kwamba kuna mashamba ambayo yamepatiwa lease, nasikia mbeleni ilikuwa miaka mia tisa tisaini na tisa ikakwisha ikawa miaka tisaini na tisa ambayo sasa yule ambaye anayepatiwa hiyo lease anapata manufaa yeye peke yake. Tukapendekeza ya kwamba hayo mambo ya lease ikomeshwe kabisa.

Upande wa elimu, tulipendekeza ya kwamba elimu iwe ya bure kuanzia darasa la kwanza hadi kidato cha nne. Pia hapo tukapendekeza mfumo wa elimu urudi kama wa zamani yaani 7-4-2-2.

Ugawanyaji wa mamlaka, hapo tulionelea kwamba kuna watu amba wamejibiza mamlaka. Kwa mfano, tulikuwa tunaangalia upande wa shule kuna board of governors unakuta mtu mmoja anakuwa member wa zaidi ya shule mbili, tatu na kadhalika, tena hiyo iwe kama anakuta Board of Governors member awe wa shule moja na pia awe na mtoto katika hiyo shule.

Na pia tunapendekeza na watu amba wanastaafu tunajua kabisa kulingana na katiba iliyoko miaka hamsini na tano ukimaliza wewe hufai kwa serikali. Hawa tunapendekeza ya kwamba akishastaafu asipatiwe nafasi ya kusimamia shirika lolote lile. Maana hapa anawanyima wale vijana amba ni chipukizi nafasi ya kazi. Halafu kuwe wale amba walilazimika kustaafishwa na serikali tunaonolea ya kwamba wale watu wengi amba walistaafishwa na serikali walikuwa ni vijana wetu wale wadogo wadogo na wazee wakaachwa.

Tunapendekeza ya kwamba kama utakuwa unastaafishwa na serikali basi iwe ni wazee amba wamefanya kazi zaidi ya miaka ishirini, sio vijana amba wamefanya miaka miwili, minne wanastaafishwa.

Halafu mawaziri tukapendekeza ya kwamba mawaziri wapewe kazi kulingana na taaluma zao. Ile katiba iliyoko nafikiri unakuta mtu ambaye amesomea Engineering anapatiwa waziri ya kusimamia mambo ya afya na mambo hayataenda sawasawa.

Halafu hapo tukapendekeza ya kwamba mkenya yeyote yule awe chini ya mamlaka, no one should be above the law. Pia, mbunge akikosana katika vikao vya bunge basi waliomchagua wapitishie kura ya kutokuwa na imani, maanake kwenye maredio tunasikia mjadala haiendi kwa sababu wale wabunge hawatoshi na hao wabunge wametumwa na wananchi kuwakilisha huko.

Halafu hapo hapo tena tunapitisha ya kwamba mbunge aliyechaguliwa kwenda bungeni awe anarudishia wale waliomchagua ripoti ya mijadala yake ya bunge baada ya miezi mitatu. Halafu tukapitisha ya kwamba wakati wa uchaguzi uwe wa kweli, uhuru na haki.

Halafu tuna haki za watoto. Hapo kama wengine wameeleza, kunajisiwa kwa watoto labda wa miaka mitatu, labda kumi adhabu kali ichukuliwe kwa wanaohusika kulingana na yale madhara yale mtoto amepata maana amepata kiu – psychologically, physically and emotionally. Kwa hivyo, mfanya kitendo hicho achukuliwe hatua kali. Halafu tukapitisha kwamba utamaduni, mila, madini, ziheshimiwe za kila kabilia na hapo tukapitisha ya kwamba kama hapa wataita wana mila na tamaduni zao, zamani wazee walikuwa wanaketi nje wanafoka moto wakizungumza na kujadiliana mambo yao vile watayendesha halafu wanakuja nyumbani na pia walikuwako na pombe yao ya kinywaji ambayo ilikuwa inaitwa ndeje. Heri waruhusiwe kuendelea kunywa ndeje bila kutatizwa na mtu yeyote.

**Com Salim:** Asante bwana Benson Malugha kwa maoni yako. Anayefuata ni Bwana Danson Mwakima.

**Mr. Mwakima:** Asante sana. Jina langu ni Danson Mwakima; nimetayarisha mapendekezo yafuatayo: Katiba iwape wananchi uwezo wa kutoa mapendekezo iwapo inarekebishwa yaani ammendment. Iweke rasilmali hizi, kwa mfano Tsavo National Park iliyoko Taita, zifaidi wenyeji, na basi imilikiwe na County Council ya Taita Taveta, katika kiwango cha Game Reserve ikiwa ni robo ya mbuga hiyo na robo tatu igawanyiwe wananchi kwa ajili ya kulima.

Katiba ionyeshe Kenya ni taifa huru kiuchumi, kisiasa na hata kisheria. Mtindo wa kutawala uwe wa demokrasia ya majimbo. Katika ngazi ya vijiji kuwe na muungano wa vijiji. Kazi ya kanda tuwe na diwani, wilaya, serikali za mitaa, mkoa, majimbo, taifa, serikali kuu, ikuunda na serikali kuu, dola na rais.

Mawaziri wote wateuliwa nje ya bunge kulingana na taaluma zao. Kwa mfano, waziri wa Afya awe amesomea udaktari. Dola iwe na bunge iliyo juu, serikali ya kipimo sio amurishi. Mahakama huru, ofisi ya mteteaji wa haki za umma yaani ombudsman atakayeteuliwa na bunge baada ya uchaguzi.

Kuwe na tume ya ufisadi na tume ya ukweli na marudiano yaani peace and reconciliation. Katiba iwe na vyombo vya habari yaani usawa kwa vyama vyote.

Elimu ya uraia iwe ikifundishwa katika mashule kwanzia shule ya msingi. Katika shule za msingi pia watoto wawe wanafundishwa lugha ya mama yaani mother tongue kwa sababu wengine wameshika lugha ya kujitungia kama ile inayoitwa sheng.

Katiba iwe na huduma za bure za afya mahosipitalini na hata kwa watoto kuanzia mwaka moja hadi miaka sita. Pia katiba iruhusu kuweko kwa madaktari wa kienyeji wanaotibu magonjwa tofauti wakitumia jinsi ya kiasili kama vile Makini Clinic.

Tume ya uchaguzi iwe huru na iteuliwe na bunge. Tarehe ya uchaguzi ujao iwe imejulikana wazi baada ya uchaguzi wa awali. Mtu yeoyote awezaye kupiga kura aweze kupigiwa kura. Kuwe na ballot box za kioo yaani transparent, ndio wakati mtu anaweka hiyo kura yake iwe inaonenkana na watu ambao wako pale.

Na pia, ili kupunguza gharama na muda, kitambulisho cha kitaifa kitumiwe kwa kupiga kura. Katiba pia ionyeshe vyoto vyote; wachaguliwe na zaidi ya watu nusu.

Rasilmali na lease zote za mashamba za umma ziondolewe kabisa. Mtu yejote katika nchi ya jimbo asiruhusiwe kumiliki rasilmali na ni lazima kwanza utasaidiwa na mwenyeji.

Bunge: Wabunge wawe wakifanya kazi mfululizo bila kuhepa hapa kikao na ikiwezekana hawafanyi kama vile waakilishi wa umma kwa sababu wote wanalipwa na rais. Kila chama kiwe na chumba cha mikutano bungeni ili wajadiliane kama saa moja kabla ya bunge kukutana.

Tatu, magazeti yawe na vyombo vya fuatilizi na ofisi ya ndani ya bunge.

Vyama vyote vya kisiasa viwe na usawa wa fedha kutoka hazina kuu. Sita, anayeomba kura lazima awe ako katika chama sio private yaani kibinafsi sasa.

Bunge iwe na uwezo wa kumuondoa rais au waziri mkuu kwa hali ya kutisha, ajiuzulu ama kura ya kutokuwa na imani na yeye. Kikao cha bunge kiwe moja kwa moja katika vyombo vyahabari hapana ati reporter anaripoti. Inakuja moja kwa moja kama ni kwa T.V. ama radio na katika hali ya lugha ya kueleweka haswa kiswahili.

Kuwe na kipengele cha kusimamia local liquor kwa sababu hii inatumika kitamaduni, kwa mfano, ngo'mbe za wajomba ambazo hutolewa na pombe. Yangu ni hayo tu nashukuru.

**Com Ratanya:** Asante Bwana Danson Mwakima. Sasa namwita Bwana Nelson Kanda.

**Mr. Nelson Kanda:** Asante sana tume. Mimi niko na mapendekezo yangu machache.

Pendekezo langu la kwanza ni kuhusu forests. Ningependekeza kwamba forests zote ziliko mahali wananchi wanaishi na ziko na labda wanyama wanaharibu mimea yao, pesa hizi zinatokana na ushuru na misitu hiyo zenyewe zitumike kwa kujenga shule za kusaidia watoto ambao hawaijiwezi.

Pia, serikali ya wilaya ipewe mamlaka kama kusimamia; pesa nazo zitumiwe kwa minajili ya maendeleo.

Serikali ziwe za majimbo kwa sababu pesa nyingi zinazotolewa kama misaada zinaishia miradi mingine bila kufikia na kupokewa na wilaya zingine.

Kwa hivyo, serikali zikiwa za majimbo wilaya zote zinaweza kufaidika na misaada hiyo. Asante sana, yangu yalikuwa ni hayo machache.

**Com Ratanya:** Asante na sasa namwita Bwana Benson Mwaboganda.

**Mr. Benson Mwaboganda:** Kwa jina Mimi ni Benson Mwaboganda. Nimetembea nchi nyingi za Kenya nikiwa diwani na nikawahi kuona ya kwamba watu wa nyanda za juu wana majani, kahawa, pyrethrum, na hata ng'ombe za maziwa. Rasilimali za Taita na Taveta basi hatuna hivyo vyote ambavyo nimetaja ila ni ardhi yao.

Ardhi imechukuliwa na serikali kuu ikapewa jina National Park, ikazuia baraka ya wilaya ya Taita Taveta kuchukua au kukusanya mapatao ambayo yanapatikana kutokana na watalii ambao wanapita hapo kuona wanyama wa pori.

Kwa hivyo, napendekeza ile rasilmali hii itumike kwa watu wa Taita Taveta na hilo neno National Park liondolewe na tuwe na Game Reserve; hili baraza la hawa Taita Taveta liwe na uwezo na mamlaka ya kuchukua mapato ambayo yanapatikana kutokana na watalii wanaokuja. Iweze kusaidia maendeleo na elimu katika wilaya hii.

**Maji:** Katika wilaya hii mwenyezi Mungu ametunukia kuwa na maji mengi sana na maji hayo yanetolewa katika wilaya hii yakapelekwa hadi Mombasa. Baraza la Taita Taveta limewasilisha kwamba wapatiwe angaa senti tano kwa litre moja lakini hawakuweza kukubaliwa kuchukuwa. Napendekeza kuwa rasilmali hiyo ya Taita na Taveta ambayo mwenyezi Mungu ametupa vile wengine wamepewa makahawa na majani tutoze maji ambayo yanaenda Mombasa kuchukuliwa na watu pale, maana ni biashara unaundwa na haki Wataita na Wataveta kupata sesi ya maji hayo.

**Madini:** Utaona katika Kenya hii au baadhi ya Afrika madini mengi na mazuri yanapatikana katika wilaya hii. Tarehe ishirini na sita mwezi huu, tulizungukia wilaya hii ya Taita Taveta tukaenda sehemu ambayo inajulikana Mang'are tukaona madini yakichimbwa na mashini makubwa, makubwa na madini hayo yote yanapotolewa basi yanauziwa watu binafsi wanakuwa millionaires; mTaita na mTaveta ambaye ardhi alipewa na Mungu na rasilmali yote inafaidi watu wengine ilhali wao wanaachwa mikono mitupu. Napendekeza madini yote ambayo yatachimbwa katika wilaya hii basi baraza za wilaya kama county council, municipality na town council ziwe na mamlaka kuona kwamba ni kiasi gani cha madini ambayo yamechimbwa na ambayo yanataka kuuzwa nje watose sesi, ili pesa zipatikane za kutosha za kuendeleza wilaya hii.

**Misitu:** Inaonokeana wazi misitu ya wilaya ya Taita Taveta ina viumbe ambavyo haviwezi kupatikana katika ulimwengu huu na moja uko hapa kilometre mbili ambao unajulikana hapa kama Ngangao forest. Misitu huo na mingineo ilioko katika wilaya hii inaleta watu wengi sana katika dunia hii kuja kuona vile vifaa na viumbe na miti lakini basi pesa ambazo zinapatikana kufuatana na hayo yote ambayo yanapatikana hapo basi baraza la wananchi kwa jumla na wanawake wanapendekeza misitu yote ya wilaya hii ambayo imekuwa gazetted iwe chini ya mamlaka ya baraza ya wilaya ili iwe na nafasi ya kupeana ruhusa mtu kuingia atoe pesa na akitoka awe ameacha ile mali msituni.

**Mazingara:** Kwa jumla, vile Mungu ameumba dunia hii yetu, wilaya hii ya Taita Taveta ni tofauti sana na wilaya zingine. Kuna milima mirefu na mabonde mengi na watu wote ambao wanaishi nyanda za chini wanategemea milima hiyo kwa njia ya kupata maji lakini basi, wazee wetu waliwahi kulinda misitu hiyo sana kwa sababu maji inatokana na misitu. Wazee wengi walilinda

misitu kukawa na maji mengi sana lakini saa hii misitu hiyo imeharibiwa; watu wamelima, wamefyeka kila mahali na maji imeanza kupungua.

Napendekeza kufuatana na mazingara kuwe na kipengele na kisiwe cha hivi hivi bali kitafutiwe lugha kamili ili mwananchi yejote atakayepatikana anaharibu mazingara ya wilaya hii basi achukuliwe hatua kikamilifu maana anahatarisha maisha ya watu wengi.

Mabaraza ya wilaya yapewe mamlaka kuona kwamba misiti imelindwa na kuhifadhiwa kikamilifu.

Bwana mwenyekiti nikiendela kumaliza nitaongea kuhusu mambo ya afya ya mwananchi wa Kenya. Watu wengi katika nchi hii ya Kenya, kwa sababu ya ukosefu wa fedha au mali, wamepoteza maisha yao au hata hawana nafasi ya kupeana kupata matibabu kikamilifu kwa sababu ya hili neno ambalo limeingia cost sharing. Mimi ni mgonjwa sina ndururu; nikienda hospitali basi nkipimwa damu ni shilingi mia moja; nkipimwa malaria ni shilingi hamsini nami nyumbani nalala njaa, sina kitu napendekeza mambo ya afya yawekwe maanani. Mwananchi yejote akienda hospitali apate matibabu bure la sivyo tutaendelea kupoteza watu wengi.

Namalizia mambo ya elimu bwana mwenyekiti. Napendekeza kuwe na elimu ya bure kuanzia shule ya msingi hadi ya upili maana yake tunapoteza talakwe nyingi sana ambazo zimebekwa kwa vichwa vya watoto ambao baba zao ni masikini. Basi yule ambaye ana pesa anapata hiyo nafasi na yule ambaye hana fedha mtoto wake anaishia pale. Kwa hivyo napendekeza elimu ya msingi mpaka ya upili iwe bure ili tuweze kuchukua hizo talanta ambazo Mungu ameziweka kwa wana wetu. Ni hayo tu Bwana mwenyekiti. Nakoma hapo.

**Com Salim:** Asante Bwana Benson Mwaboganda. Kabla haujandoka nikuulize swala moja kama hukufahamu uzuri. Ukisema elimu ni bure tangu msingi mpaka.

**Mr. Mwaboganda:** Elimu ya msingi.

**Com Salim:** Yaani zote mbili ziwe...

**Mr. Mwaboganda:** Ziwe bure.

**Com Salim:** Bure kabisa. Jane Kisocho.

**Ms. Jane Kisocho:** Bwana mwenyekiti na kamati la kuunda hili la kutengeneza katiba. Naanza na elimu. Taasisi za elimu.

**Ms. Kisocho:** Hizi taasisi za elimu, especially secondary schools kuna matatizo katika huu uchaguo wake wa Board of Governors. Unakuta watu wa BOG ni watu ambao wana kazi zao na wamechaguliwa kusaidia ukarabati. Mara kwa mara mkutano ikiitwa utamkuta mtu mara ameenda kwa mkutano fulani mara yuko mahala fulani. Hili limekuwa tatizo kwa

headmaster pia na shule kwa uzima au kwa ujumla pamoja na walimu walioko katika shule hiyo. Pendekezo yangu ni hii BOG members wachaguliwe na wazazi wa shule hizo zinazohusika.

Tena asiwe ni mtu ameritaya ndio anachaguliwa BOG member; akue ni mtu yeoyote yule ambaye anaweza kuendesha shule.

La pili, serikali zetu zikae katika hali ya majimbo; watu wa Mkoa wa Pwani wajue mambo yao na shida zao, tusijimaanishwe shida zetu na wale wa a certain province. In fact, shida ziko tofauti. Natukae na serikali za majimbo.

Pili, barabara za vijijini ninaomba Katiba iingilie kati zizimwe na serikali kwa sababu kule vijiji ndio kuna mazao kama maziwa, mahindi na kila kitu cha kukula. Hizo barabara ziko katika hali mbaya na wananchi wanagharamia. Magari hayafiki. Ikiwezekana, zirudishwe kwa upande wa serikali na zilimwe.

Tatu, ma-Councillors wapewe mamlaka ya kusimamia District Development Committee meetings. Ikiwezekana, Councillor kama amepewa maoni na wananchi wakienda pale akae chairman wa huo mkutano si D.C. D.C ni mtu amekuja hatujui, lakini Councillor akiwa chairman wa huo mkutano nafikiri hayo mapendekezo yetu yanaakilishwa vizuri.

Ya nne, nazungumzia mambo ya watoto wa university. Tunasikitishwa na neno moja, mtoto amepita anaenda university lakini barua yake kuasilia kuja imechelewa na anatakikana mwezi ujao aende. Mzazi ni maskini atoe wapi pesa za kupeleka mtoto huyu? Ikiwezekana, haya mamlaka yapewe ma-headmaster waangilie kazi; barua ziletwe mapema ili mzazi ajitayarische kupeleka mtoto wake university.

La sita, naomba taasisi ya elimu, ikiwezekana, wasimamie walimu kulingana na ahadi waliopewa wataongezwa mshahara na hiyo ahadi itekelezwe. Kuna watu wengi wanaweza kuondolewa kazi na huo mshahara wote ukikusanywa walimu wapewe haki zao ili waendelee kufundishia watoto wetu. Lisiwe tatizo kwa walimu na watoto kwa sababu watoto wanawategemea.

Saba, hawa ombudsman wakae katika wilaya au katika taarafa, sub-location au location kwa kutekeleza mahitaji na kutetea raia waliokaribu nao. Unaweza kuwa na tatizo lako na ukapeleka kwa mzee wa kijiji, mzee wa kijiji anachukulia mzaha unachukua mwenyewe mpaka kwa chief, ukifika kule ametanguliwa tayari anamwambia huyu tumemalizana na yeze kijijini. Ukienda kwa chief tayari subchief yuko pale anakwambia haya maneno wacha tumalize na ni maneno ambayo unataka uende nayo upate mtu maneno. Tukae na watu watakaotetea haki za binadamu na watetee mtu kikamilifu.

Na la mwisho, huu utaratibu wa wabunge wetu tunataka mbunge tumemchagua Taita aende kwa bunge na akae. Mbunge asiwe waziri, kwa sababu anapoapa waziri ametajishwa vyeo viwili anatumikia Kenya nzima na sisi hapa wilaya hapa tunamtaka. Sasa waziri achaguliwe kulingana na elimu yake; kama amesomea hesabu awekwe waziri wa Fedha lakini asiwe mtu ametoka bunge hajui anaenda kuwekwa hesabu. Akikaa hapo hajui ni kitu gani anafanya awe ni mtu amesoma ile kazi hiyo kikamilifu. Nafikiri yangu ni hayo tu. Nimemaliza.

**Com Ratanya:** Na sasa Bwana Vincent Mwazighe.

**Mr. Vincent Mwazighe:** Mimi ni Vincent Mwazighe kwa jina. Nina memorandum lakini nataka kuzungumza kidogo kuhusu kwanza rasilmali zetu za kitaita. Hapa Taita tuna rasilmali nyingi sana kama maji, Mgodi Game park, hotels, misitu na hata mashamba yenyewe. Lakini hizi rasilimali zote ziko chini ya mikono ya watu ambaeo si wataita.

Pendekezo langu ni kwamba ikiwezekana kwa katiba ijayo, rasilimali tunazo zote hizi zimilikiye na waTaita chini ya County Council ya serikali yetu ya wilaya.

Pia, mbuga zetu za wanyama zimechukua sehemu kubwa sana ya nchi yetu ya Taita. Napendekeza ipunguzwe na waTaita wenye we wapewe mashamba watumie kwa kulima na hiyo sehemu kidogo itakayobaki iwe kwa wanyama. Nikija kwa tafrija, yaani starehe kidogo, wazee wetu wa Taita wanapata shida sana kutokana na polisi kwa ajili ya kushikwashikwa ovyo ati wametumia pombe inaitwa mubangara. Pombe hii tunaomba iwe ni halali. Tusker pia ufunjwe.

**Com Ratanya:** Ufunjwe vipi?

**Mr. Mwazighe:** Culture ya utamaduni tunaomba mila na desturi zetu za waTaita zidhihirishwe kama zamani. Na kwa upande wa kazi imekuwa ni tabia mbaya mtu anastaafu anaambiwa arudi nyumbani akalime kesho unaskia ni General Manager wa kampuni fulani. Watu kama hawa wakipewa kazi tena, kazi iwe ni moja kwa mtu moja; yako ikiisha basi imeisha urudi nyumbani. Asante sana.

**Com Salim:** Bwana Edward Mwaigo.

**Mr. Edward Mwaigo:** Asante sana Bwana mwenyekiti. Mimi ni Edward Mwaigo kutoka katika kata ya Pwona. Mimi naanza na ardhi. Hili ndilo linawasha watu wengi sana. Ardhi yetu ilichukuliwa bure na tunaitaka. Asilimia tisini na mbili iko na mbuga za wanyama, kunakuja 11% na sisi waTaita hatutumii nguvu kama makabila mengine. Tunaomba, maana hatutumii nguvu sisi tunatumia kama ng'ombe na makabila mengine na sisi ni watulivu. 50% irudishwe huku pesa zake ziwe zinaingia kwa County Council na zisaidie elimu ya watoto masikini.

Elimu na matibabu zisiwe mpango wa kugawanya gharama, iwe bure. Hazina ya fedha igawanywe kwa kata baadala ya wilaya. Mabarabara ziwachiwe County Council kama zamani. Hakuna malalamiko iliyotheke wakati ule lakini sasa tunayo mengi. Wanaokosea umma wafutwe kazi baadala ya kuhamishwa. Mara wengine wanakosea wanapewa ofisi pahali fulani na kikoa kitu chochote cha kisiasa, cha mradi maana ni wafisadi.

Bunge lisiwe na mamlaka ila wananchi kwa mabadiliko yote; wananchi tuwe tunatoa maoni yetu badala ya wao. Mfano, hawakuangalia mfumo wa nchi unaendela aje. Walijongezea mshahara na zingine na huku mwalimu anapata shilingi elfu kumi au elfu nane. Wanasaidiaaje? Hicho ni kilio kikubwa hatutaacha maishani kulia.

**Urais:** Wananchi wa Kenya na nitanena, ni haki yao kupatiwa uraia. Si uraia wa kununua hata tunashangaa mambo mengine ya

system vile inavyofanywa hapa na hali sisi tuko. Mkenya yejote amezaliwa hakika anasumbuliwa huku na huku. Mambo ya vita imekuwa ni njia ya kutengeneza pesa kwa watu wengine, mfano ma-D.O. na ma-D.C. na ma-subchief, mara imekuwa ni njia ya kupata pesa. Yule asiyetua pesa basi na hali wewe ni mtaita.

Kitambulisho, haiwezekani kuomyesha mzalendo kamili wa Kenya. Wasiwe wanabagua maana kuna watu wengine asili yao si nyeusi, si waafrika lakini tunajua yamkini ni wazaliwa wa Kenya. Hawana mbele wala nyuma.

**Usalama:** Mamlaka ya usalama nafikiri yasiwekwe umri kubwa ya urais. Mamlaka ya usalama na ya majanga yaachiwe President. Hilo ni jambo likigawanya watu wengi wataleta shida Kenya hii.

**Uhuru wa vyama vya kisiasa:** Kila chama kijigharamie na kiwe na muongozi wake.

Muundo wa serikali uwe wa majimbo. Waziri mkuu na rais, uongozi wa serikali na mikoa itupiliwe mbali. Hata waliounda ile katiba ya zamani ni wakoloni na kule kwao hakuna.

**Uwezo wa bunge:** Wabunge wawe wanachagua makatibu, wenyekiti wa umma, mawaziri, mahakimu wa umma na kazi ya mbunge ibakie vile vile.

Umri wa rais uwe ni miaka 45 na kuenda mbele. Mbunge awe na miaka 25; diwani, 25. Wabunge wateule, kwa maoni yangu, waondolewe maana hawasaidii mtu, wanaenda tu kwa serikali kuunga mkono tufinywe.

Rais asiwe na kura tu; awe na uwezo wa kulinda bunge lakini asiwe na mamlaka juu ya bunge.

**Uchaguzi:** Kura zihesabiwe mahali zinapopigiwa, zihesabiwe hapo hapo mbele ya wananchi. Mamlaka ya nchi, rais awe chini ya sheria na awe mbunge kwa muda wa miaka kumi.

**Mahakama:** Tuwe na mahakama ya chungu ndio waislamu nao wawe na sheria zao.

Kukulinda na kuzozana na mambo ya elimu, serikali za mitaa, ma-mayor na wenyekiti wachaguliwe na wananchi. Vipindi kama vya wabunge. Elimu ya madiwani na ya wabunge iwe sawa. Wananchi wana haki ya kuwaregesha nyumbani wakiwa wamekosa umma. Uchaguzi uwe wa siri na kura nyingi ziwe za mshindi. Aachwaye kwa chama chake kwa mchujo asihamie chama kingine.

Haki za kimsingi mahakamani zifanye haki kuhusu case.

Mamlaka ya ardhi ni mali ya mkoa na wanawake wana haki ya kumiliki ardhi na mkuri za Kenya zizimwe na kukaguliwa na bunge ili lisivunje utamaduni wa kitaifa. Msichanganywe na ujenzi wa taifa. Serikali ilinde mazingira, maji, misitu na wanyama. Kimko, NGOs wawe uhuru kusaidia raia au umma bila kuingiliwa na serikali.

Ya mwisho, serikali ikae chini iongezee walimu mishahara kwani wabunge wamejiongezea pesa nyingi pamoja na mahakimu na kusahau walimu. Asante sana.

**Com Salim:** Asante sana Bwana Edward Mwaigo kwa maoni yako na memorandum yako. Sasa namwita Bwana Mutweta Felix.

**Mr. Felix Mutweta:** Bwana mwenyekiti, mimi nafikiri nilikuwa nimetumwa na wenzangu kutoka kwa vijana. Mambo mengi

yameandikwa ambayo nimesikia yakinjwa na wenzangu kwa hivyo basi ningependa tu nigosie jambo moja ama mbili ndio nijaribu kufafanua sehemu moja ya haki ya wanadamu.

Lakini kwanza ningependa nigosie haki za wakenya, hasa ile haki ya uhai kwa sababu hatuwezi kuumba binadamu. Wenzetu wale walioketi walisema hukumu ya kifo itupiliwe mbali na badala yake aliyefanya kosa kubwa kabisa aweze kufungwa kifungo cha maisha lakini si kutoa uhai wake.

Halafu nitagusia umri wa rais. Umeguswa na wenzangu kutokea mbeleni lakini tulikuwa na kiwango cha juu ambacho tulifikiria umri wa rais usipitishe. Nacho ni miaka 75. Rais asiwe ambaye amefikisha miaka 75.

**Elimu:** Tukirudi kwa elimu imetajwa kwamba elimu iwe ya bure kutoka shule ya msingi hadi ya upili. Sisi hapa tulipendekeza kuwe na mandatory universal primary and secondary education na iwe bure. Iwe ni lazima elimu hii ipatiwe watoto wote na isichaguwe mtoto ana ulemavu ama hana. Iwe ni lazima mtoto yejote awe shule kama hajaondolewa na kuanguka mtihani. Akipita kidato cha nne kuenda chuo kikuu aweze kupata mkopo ama aweze kupewa usaidizi na serikali kisha baada ya kumaliza masomo yake akiajiriwa aweze kulipa mikopo ile alisaidiwa nayo.

Tunaporudi katika haki za kimsingi, tuliangalia na mara nyingi tumesikia haki za akina mama, haki za wanawake lakini tuenze kuondoa malalamishi haya na kuangalia watoto wetu wote ni sawa hivyo basi wasichana wetu wavezeshwe kuhusishwa katika kuridhi mali ya wazazi wao.

Halafu ndio tuje kwa walemavu. Bwana mwenyekiti, ni bahati mbaya kwa sisi wakenya kwa sababu tunapenda sana documentation ya curriculum but implementation is new, kwa mfano tunaporudi mwaka wa themanini na tano tulikuwa na Eucharistic Congress na mambo ya akina mama. Mabasi Nairobi yalikuwa yamejaa nafasi za walemavu walikuwa hata wamenunua viti pengine viwili, vitatu ili waweze kuingia kwa mabasi hayo wakitumia magari yao ya kusafiria- wheelchair. Lakini baada ya hivyo vikao mabasi hayo na hivyo viti viliregeshw. Kwa hivyo mara nyingi walemavu wetu hawawezi kutumia magari yetu ya umma na hata manyumba yetu ambayo hata ni ya umma. Kwa mfano, hata tukiangalia kanisa hili pengine mlemavu akikuja na kiti cha wheelchair atahitaji msaada kuingia. Ni kwa sababu pengine katiba yetu haijaingiza mlemavu katika mambo haya; haijaingiza masilahi ya mlemavu. Hata tunapoangalia katika runinga zetu, mtoto au binadamu ambaye hasikii hawezi kupata habari zinazoendelea. Wakati mwingine tunapata katika runinga, yule msomaji anasoma na kuna mtu hapa ambaye anajaribu kuonyesha kwa vitendo, sign language. Kwa nini lisiwe ni jambo ambalo litaendelea kila wakati ili yule ambaye hasikii naye haweze kujumuika kwa kupata habari?

Tunaporudi kwa huyo huyo mlemavu, huduma za afya katika hospitali zetu za wilaya hatupati hizo huduma bure na kwa urahisi kama physiotherapy, occupational therapy, palmic attention na petharapy. Kwanza wengi wetu ambao waemefanya kazi hii wanatoka kwa sababu nafasi hizi hazijapewa katika katiba pia umuhimu wake haujatumiwa na katiba yetu. Hivyo basi naomba katiba iweze kulinda watu hawa na watoto kwa jumla na hasa haki kwa huduma ya afya, elimu, na kuangalia vikundi ama wengi wetu ambao wanatengwa ama kunyanyaswa.

Kwa hayo machache ningependa kuachia hapo na mtawezu kungualiwa yale muhimu yaapishwe na yale pengine hayatakuwa

kwa sababu sehemu zote zinafaa kueleweka na sote. Asanteni.

**Com Salim:** Asante Bwana Felix Mutueta kwa maoni yako. Nilisahau jambo moja hapo asubuhi tulipoanza mkutano kusema kwamba tunaye officer hapa moja wetu ambaye anaweza kutafsiri yote yanayosemwa hapa kwa wale amba wanataabu ya kusikia vizuri. Sasa yuko hapa Lucy. Sijui kama yuko kati yetu jamaa yejote ambaye ana taabu ya kusikia vizuri kufuata hayo yanayosemwa, yuko? Haya twamjua yejote aliyoko hapa. Sawa, sasa namwita Bwana Herman Mwaila.

**Mr. Herman Mwaila:** Kwa majina ni Herman Mwaila. Mimi nitagusia tu kwanzia na post ya rais. Rais mwenyewe asiwe juu ya sheria; awe kama mkenya yejote. Tukirudi kwa afisi ya rais, mamlaka yagawanywe. Kuwe na waziri mkuu na ma-department yaani yako pale yawe chini ya Commissioners. Kwa mfano, kama Director of Personnel Management apewe mamlaka; asiwe chini ya rais, ili wakati anatekeleza wajibu wake asiwe anaamrishwa.

**Watumishi wote wa umma:** Kama ni ujuzi kusiwe na provision kama ile yao Public Service Commission. Kwa maoni yangu, napendekeza hii Public Service Commision itupiliwe mbali na Director of Personnel Management apewe uwezo wa kuajiri na kupandisha vyeo.

Tukirudia kwa upande wa kama polisi Commissioner, apewe uwezo asiwe anaamrishwa ama anapata maagizo kutoka kwa rais.

Upande wa defence pia hivyo hivyo, au apewe uwezo asiwe anapata maagizo kutoka kwa rais. Mashirika yote ya serikali yawe na kwa mfano, Commissioner wa kusimamia na awe na uwezo sio rais ndiyo anateuwa ma-directors.

Tuseme tume iwe inatuewa madirectors na ukija pengine kwa afya hii mambo ya cost sharing hiyo ni mbaya. Haina maana sababu hata pesa zinazokusanywa hapo hazijulikani kamwe zinawekwa ama haziweki kwa account. Cost-sharing itupiliwe mbali; huduma zote za afya ziwe huru kwa mKenya yejote.

Nitagusia Mathare kidogo. Kwa barabara, hapa kwetu taifa tulisahaulika. Nimetembea sehemu nyingi ambazo nikijaribu kulinganisha na hapa kwetu ama mkoa wa Pwani kwa jumla tumesahaulika.

Kama ni rasilmali za nchi zigawanywe sawa sawa; ikiwa ni barabara, afya na kazi zikitangazwa kila mkoa uwe na haki yake.

Lakini si labda mkoa fulani utasikia inaadikishwa ilhali mkoaa mingine hapana. Kwa hivo napendekeza kama wakenya wote, ikiwa ni upande wa kazi, kila mkoa update wake na ninapendekeza kwamba kurudishwa kama ile ilikuwa ni labour office kama ni kazi itangazwe katika district level kulingana na ujuzi wa mtu. Isiwe siku hizi tunaona mpaka upewe kitu kidogo. Hiyo kitu kidogo itolewe kabisa.

Tukirudi kwa upande wa elimu, napendekeza ile system ya zamani ile ya 7-4-2-3 na kuanzia seven mpaka hii form four iwe free; serikali igharamie kwanzia primary. Hii mambo ya cost sharing itupiliwe mbali sababu serikali inafaa igharamie kama vile ilikuwa inafanya zamani.

Mijengo mzazi aachiwe vijenzi, na kwa upande wa ardhi napendekeza kwamba Taita ina ardhi kubwa sana ambayo iko chini ya

wizara ya wanyama wa porini. kwa hivyo napendekeza ya kwamba hii County Council ipewe uwezo kama vile ilikuwa zamani, Game Reserve. County Council iwe na uwezo wa kugawanya kama ni rasilmali ya madini. Watalii wanaokuja hapa mapato tuseme kama 60% iweze kuingia katika County Council kuhudumia wanafunzi wale wanaokosa school fees. Juu ya serikali na huduma za barabara na zinginezo kwa vile wenzangu wamegusia mengine nafikiri nitamaliza hapo. Asanteni sana.

**Com Ratanya:** Asante Bwana Herman Mwaila. Sasa namwita bwana Harrison Mwaighe

**Mr. Mwazighe:** Mimi napenda kuwakaribisha. Kwa jina naitwa Harrison Mwazighe na nina maswala kama matatu. Swala la kwanza ni kuhusu haki za kimsingi. Wafanyi kazi wananyanyaswa sana.

Kwa mfano, kuna mbinu ambayo inatumika kwa sasa, wafanyakazi walioajiriwa na mwajiri mmoja wawe na vyama viwili nya kuwatetea. Mfano mzuri ni chama cha walimu, KNUT na chama kingine ambacho kimeruhusiwa, Kenya Union of Post-Primary Education Teachers, KUPPET. Hii imefanya nguvu za walimu kupigania haki zao kupungua na hii inafanya mfungiwe. Kwa Kiingereza tunasema, “Divided We Fall and United We Stand.”

Kwa hivyo, hii ni njia ya kuwapunguzia walimu nguvu wasipate haki zao. Ningependekeza, katika katiba mpya watu wote walioajiriwa na muajiri mmoja wawe na chama kimoja.

La pili, inaonekana kwa sasa kuna mambo ambayo yanatanisha kwa hali ya wafanyakazi kwa kuwa hakuna uangavu na uwajibikaji yaani transparency and accountability. Hii nikisema hivyo namaanisha kwamba unasiakia uchumi wa taifa letu umezoroteka sana lakini punde si punde unasiakia katika section fulani watu wengine wameongezewa kitu fulani. Kama wengine wanapigana na ukiwa na uchumi umeharibika. Kile kinachoelewaka ni kuwa kuna wakati hata wanaweza kwenda bila hata mshahara kwa miezi kadha pengine ni wakati wa shida pengine wakati wa vita na kadhalika. Lakini hapa inaonekana hakuna uangavu (transparency). Kwa hivyo, ile gap ya mishahara lazima katika katiba ijaayo iaangaliwe. Hilo ni pendeleko langu la kwanza.

La pili, nikigusia tena juu ya wafanyi kazi ningependekeza mara moja, mimi ni mwalimu, tunafundisha watoto nao baadaye wajivunie elimu. Tunashikilia nyadhifa zetu pengine miaka hamsini, hamsini na tano na watoto wetu wanaenda vyuo nya walimu, vyuo nya afya, vyuo vikuu wanazunguka na hakuna kazi. Je, shida hii tutaipunguza kivipi?

Ni pendeleko langu kuwa umri wa kustaafu upunguzwe ili kila mtu apate ile national cake. Hii inafaa kuanzia miaka arobaini na tano hadi hamsini ili wale wengine nao walioelimika wapate nafasi ya kula hii national cake; isiwe ni ya watu fulani tu.

Hapo vile vite nimegusia swala la wazee waliostaifu. Mtu tuseme wa miaka hamsini na tano ambaye anafanya kwa serikali akili uanza kupungua. Unakuta mtu kama huyu anachukuliwa anapelekwa shirika fulani, pengine refinery na kadhalika kizingizio ikiwa ana ujuzi. Je, ningeuliza ni mtu gani anayezaliwa bila ujuzi? Kilele ninachoelewa ni kwamba unapofanya kazi ndio unapata ujuzi.

Pendeleko langu ni kwamba mfanya kazi yejote wa serikali akistaafu asipewe uenyekiti, peana watu walioelimika kutoka vyoo vikuu na wao wapate ujuzi baadala ya kupatia wazee hawa nyadhifa kama hizo. Badala yake wawekwe katika baraza la

ushauri wawe wakishauri vijana hao kwa muda wa miaka fulani kisha vijana hao wanaendelea. Hilo ni pendekezo langu la pili. La tatu, tumesikia katika nchi fulani mtu mwenye mamlaka, waziri au mfanyakazi yeoyote akitajwa tu katika kashfa inadhahirisha kisheira hilo ni kosa inamlazimu ama ni lazima ajiuzulu. Ningependekeza katika katiba mpya ijaayo, yeoyote atakayetajwa katika kashfa yoyote, iwe ni ufisadi ama nini, ajiuzulu mamlake yake mara moja, achukuliwe hatua za kisheria.

Halafu pendekezo langu la mwisho ni kwamba tunaelewa ya kwamba kama ni mbunge mgombezi wa kiti cha ubunge au Councillor tunasikia akitangazwa amefilisika anatakikana achukuliwe wadhifu wake.

Vile vile tumerudi upande mwagine inatakikana kabla haruhusiwe kugombea ubunge au Councillor anatangaze mali aliyonayo na amepata vipi ili apatiwe nafasi ya kugombea wadhifa huo. Kwa hayo, asanteni.

**Com Ratanya:** Bwana Harrison Mwazighe, sasa namwita Bwana John Mwazala.

**Mr. John Mwazala:** Mimi ni John Mwazala. Mimi ningependekeza kwamba katiba ambayo itakayotungwa hivi sasa iwe na demokrasia, yaani iwe na kipengele kitakachomruhusu mwananchi awe na sauti. Kwa maana tunaona sheria iliyokuweko mbeleni ni ya kuweka mawazo mazuri ya mwananchi katika kaburi la sahau. Yaani tunaweza kuona ya kwamba demokrasia was just there in the papers but was not being practised.

Pia ningependekeza natural resources zilizopo karibu na mwananchi ziruhusiwe kutumiwa kikamilifu na mwananchi wa sehemu hiyo katika sheria ya umiliki wa mashamba na ardhi.

Sheria iliyoko hivi sasa ni ya kuazimu mwananchi kwa kuwa madini ama minerals zigunduliwe shambani mwako mwenye shamba hupatiwa notice aondoke mara moja. Hii humfanya mwenye shamba kuwa squatter au mtu ambaye hana shamba na mahali pa kukaa.

Jambo hili linataka libadilishwe na mwananchi apewe uwezo wa kumiliki mali hata kama ni ya dhamani gani iliyopatikana shambani mwake. Kupiga darubini tutaona ya kwamba nchi ya Taita Taveta iko na madini mengi lakini wakaaji wa sehemu hivyo ni maskini sana. Sheria iliyoko hivi sasa imewekwa mawazo ya wenyeji sehemu hizo katika kaburi la sahau naningependekeza sheria hii pia iangaliwe.

Ukirudi upande wa mbuga za wanyama sehemu inayokaliwa na wanyama ni  $\frac{3}{4}$  na ilhali  $\frac{1}{4}$  ndio inayokaliwa na watu. Mimi ningelipendekeza watu wafikiriwe zaidi kuliko wanyama na watu hawa pia waongezewe sehemu zaidi ya kukaa kuliko ile ambayo inayokabiliwa na wanyama. Kiasi kile cha pesa ambacho hupatikana kutokana na wanyama ambao unaletwa na wanyama hawa wanaovugwa ifikiriwe kuinua hali za wakaaji wa sehemu hiyo kama vile wale wamaasai wa Maasai Mara wanavyofikiriwa.

Ningependekeza kwamba pesa hizi zikiwa zinapitia katika County Council zisaidie sector ya idhara ya elimu na idara ya matibabu na pia kuinua hali za wakaaji wa eneo hili la Taita Taveta. Asanteni.

**Com Ratanya:** Asante Bwana John Mwazala kwa maoni yako. Bwana Solomo Kilambo

**Mr. Solomon Kilambo:** Asante sana Bwana mwenyekiti. Maoni yangu ni kama ifuatayo:

- Mtu yejote ambaye si Mtaita asiruhusiwe kumiliki ardhi Taita.
- Tsavo National Park igeuzwe kuwa Game Reserve na isimamiwe na Taita Taveta County Council.
- Rais asiwe juu ya sheria.
- Mtu yejote atakayepora pesa za serikali mali yake inajiwe kisha afungwe.
- Land lease ziondolewe wilayani Taita Taveta ili mashamba yafaidi wenyeji.
- Maji ya Mzima Springs yagawanyiwe wenyeji ili waendelee na kilimo.
- Madini yachimbwe na kuwa na wenyeji ili yawafaidi wenywewe.
- Serikali ijayo iwe ya majimbo na iwe na rais na waziri mkuu.
- Mtu yejote atakayeua kwa kusudia naye auwawe bila kuwachiliwa.
- Pombe za kienyeji ambazo hazidhuru wanywaji zihalalishwe na zisimamiwe na baraza la Taita Taveta.
- Elimu ya shule za msingi, shule za upili hadi vyuo vikuu iwe ya bure na pia matibabu yawe ya bure.
- Wanawake washirikishwe katika uongozi au utawala.
- Mwanaume akifariki mali yake ichukuliwe na mjane na watoto wake na sio mtu wa marehemu kwa sababu kama nyinyi mmestawi na mtu akifariki bibi anafukuzwa halafu mtu anaridhi hizo mali.
- Uajiri wa kazi usiwe wa kuhongana.
- Pesa za serikali zijulikane wazi wazi kwa Wananchi na vile zimetumiwa.
- Chief achaguliwe na wananchi na sio serikali.
- Ndoa za lazima zipigiwe marufuku na zikitokea wenywewe wachukuliwe hatua.
- Mkopo na misaada ifaidii waliochukuliwa na sio walio na vyeo.
- Wazee wa miaka sitini na zaidi wawe wakipata shilingi elfu mbili kwa mwezi kwa sababu hawa ni watu ambao hawezikufanya kibarua.
- Wabunge wasipewe uwezo wa kushambulia masomo mengine kama mishahara.
- Mwisho, kusiwe na mwiningiliano wa kazi. Kwa mfano, mtu akivunja sheria hatua ichukuliwe ipasavyo isiwe kwa sababu mimi ni waziri fulani ndugu yangu hata ameua ni kupiga simu tu atolewe mara moja. Hayo ndiyo nilikuwa nasema.

**Com Ratanya:** Asante Bwana Solomon Kilambo na sasa Sylvester Mwandami.

**Mr. Mwandami:** Jina langu ni Mwandani na nina maoni ya group ambayo tuliketi na wakanituma niyalete. Tulikuwa

tunachangia juu ya serikali za mitaa kulingana na maswali yaliyoulizwa wale ambao tulikuwa tunajadili. Walisema ya kwamba mayor ama diwani wasichaguliwe moja kwa moja na wananchi.

Jambo la pili, miaka miwili kwa mayor na wenyeviti wa County Council inatosha lakini ikiwa kazi yao ni nzuri wataendelea kugombea.

Mabaraza yawe chini ya serikali za wilaya. Kiwango cha elimu kiwe kidato cha nne. Halafu mtihani wanaofanyiwa madiwani iwe inatosha hicho kiwango cha elimu .

Halafu, jambo la sita, kuwe na masharti ya kunadili kwa wanaochaguliwa kuwa madiwani.

Jambo la saba, wananchi wawe na uwezo wa kumuita diwani ikiwa kazi yake ni mbaya kwa kuwandika barua ya kutokuwa na imani naye.

Mishahara ya madiwani ishuguliwe na meya. Halafu kusiwe na madiwani wateule.

Jambo la mwisho, rais au waziri wa local government asiwe na uwezo wa kuvunja mabaraza. Kwa kuongezea, maafisa wa kilimo katika sehemu wanayohudumu wawe wakitafutia wananchi mahali pa kuuza mapato yao.

Jambo la pili, pesa zinazojengewa mradi wowote katika location wasimamizi wa wakati huo wawe ni watu wa kutoka mahali hapo na tender za kazi au za kufanya kazi zitangazwe kutoka wilaya hiyo kwa sababu hiyo itarahisisha au itasaidia mwananchi kwenda kujua ya kwamba mradi huu ambao unaendelea katika wilaya, katika location hiyo, umefanyika kwa njia inayofaa. Asanteni.

**Com Ratanya:** Asante Bwana Sylvester Mwandami. Nahashon Mseri. Jina ni Msemi au Mseri sawa.

**Mr. Mseri:** Asante sana mwenyekiti. Kwa jina naitwa Nahashon Mseri na nina maoni ama nina majadiliano ya kikundi kwa jumla na kwa niaba ya group.

Kulingana na maoni ama mkataba huu ambapo sheria itakapotenga sasa kimila uzuri inaangaliwa kwa upande wa serikali au mambo zaidi yawe kwa kupitia kwa wananchi kuanzia kwa rais mpaka kushukia kwa wazee wa vijiji na pia kwa malipo waangaliwe.

Kuingilia kwa rasilmali, hata kwa wilaya hii ya Taita Taveta tuko na rasilmali kuanzia madini, maji, misitu na mashamba ama mawe. Hiyo sijui ama hiyo rasilmali ingetumika pahali hapa, hapo mwananchi anayekaa katika hiyo rasilmali kama madini zinatokea kwa shamba yako nisiweze kuondolewa kwa sababu yoyote ama niitwe squatter. ingekuwa hapo inatokezea mwananchi anufaike ama asaidike kwa hiyo hiyo rasilmali na isaidie wananchi wa hapo hapo.

Kwa upande wa forest iwe hivyo hivyo yaani kila mradi unatokaea ambao unaweza kusaidia mwananchi wa sehemu hiyo uwe unachangia kufanya maendeleo katika hiyo wilaya ama hiyo sub-location ama location kulingana na vile wale wanaowakilisha watakavyo panga.

Tukifikia upande wa kazi, kila mtu alipwe kulingana na kazi anayofanya. Kusiwe na malumbukizo ya vyeo ama kazi. Kwa

mfano mtu mmoja awe na kazi tatu ama tano wakati wengine wanakosa. Na kuhusu elimu kwanzia darasa la kwanza ama kuanzia nursery mpaka form four, iwe free kwa sababu ukichunguza sana tumeonelea ya kwamba watoto wale amba wazazi wao hawana uwezo ndio hupita zaidi na undani ukifuata ndio wanatufaa kwa uongozi ama wana maarifa zaidi lakini shida inakuwa ni pesa hakuna za kufanya waendelee mpaka wafike kama kulingana na akili yao vile itafikia.

Na tukifuata kwa upande wa waziri, waziri awe ni waziri na mbunge awe ni mbunge, kwa sababu ya kumtumikia mwananchi kwa njia rahisi ama kwa sababu ya kuchaguliwa kwa ile kazi unahitaji ama amechaguliwa afanye. Na kuhusu uteuzi mtu asiwe kwa mfano amesomea ni kazi ya kushona nguo aende kupewa kazi ya kujenga nyumba, apewe kazi ya zile zile anayojua ndiyo maana ataifanya kwa njia nzuri. Na kuhusu mbuga za wanyama, baadala ya kuitwa National Park iitwe Game Reserve kama ni hapa Taita iitwe Taita Game Reserve. Na Serikali pia iwe ya majimbo kusudi watawala wawe kila moja wanagawana sawa sawa kulingana na mkoa wake na mkoa wake anaotawala. Na pia kuwe na waziri mkuu na iitwe na serikali ya mkoa na serikali kuu. Nafikiri yangu yameishia hapo. Asanteni.

**Com Ratanya:** Asante bwana Nahashon Mseri. Sasa namwita bwana Crispin Mwaisege.

**Mr. Crispin Mwaisege:** Jina langu tena ni Crispin Mwaisege kutoka Ngandu. Langu la kwanza nataka tukiangalia ni vyama vya kisiasa. Hawa watu wanaouna hivi vyama huwa na masilahi yao. Kwa hivyo naona maoni yangu kwamba napendekeza kwamba ndivyo hivyo sasa waendelee kutimia pesa zao zenyewe kwa kuendesha vyama vyao isiwe ya kwamba ni serikali maanake hiyo itakuwa kuencourage watu waendelee kuunda vyama zaidi ili waweze kutumia kama njia ya kupatia pesa. Kwa mbuga za wanyama, hasa tukiangalia hapa Taita ama zimepunguzwe mashamba hayo yarudishwe kwa mwananchi au nusu ya hiso pesa zinazopatikana kutokana na hiso mbuga za wanyama basi zipewe wananchi ambayo watu wa Taita kwa sasa. Watu wengi hawana mashamba hasa tukiangalia hapa Taita ni watu wachache sana walio na zaidi ya acre moja lakini katika nchi yetu kuna watu amba wana hata maelfu ya acres za mashamba ambayo hayatumwi. Naona ni kwa manufaa ya watu wote kwamba nchi hii ni nchi yetu, mali yote iliyohapa ni yetu sisi sote basi tusiwe na mtu ye yeyote ambaye ana zaidi ya acre hamsini na ambazo hazitumii zote zili zinamzidi na zinazozidi hapo hiso zigawanyiwe watu wengine amba hata wakiweza kutumia na wasaidie kuinua uchumi wa Kenya.

Elimu ya nursery sasa ni kama ya lazima. Hasa ni base formation na ni ya muhimu lakini imekuwa ngumu sana kwa wazazi wengi kwa sababu ni mahali ambapo watu wanalipa pesa nyingi sana. Na kuna watu amba hata hawana hiso pesa. Mapendekezo yangu ni kama kwamba elimu hii ya nursery ichukuliwe na serikali na walimu wanaofundisha hizi shule pia wachukuliwe na serkali na hiyo itakuwa ni mzigo umepunguzwa sana kwa wale wazazi na pia itakuwa ina usawa kila mahali.

Wazee wengi amba wamefanya kazi kwa muda wa miaka mingi miaka 30 miaka 35 wanaretire lakini ni wachache sana wanaolipwa kabla hawajamaliza mwaka nje bila pesa ye yeyote. Naomba katika katiba mpya ihakikishe ya kwamba angaa maximum au mwisho kabisa iwe ya kwamba baada ya miezi mitatu baada ya kuretire hao wazee wamelipwa pesa zao na

warudie maisha ya kinyumbani ya kuendelea vizuri na jamaa zao. Pamoja na hilo nakumbuka mzee moja ambaye aliretire miaki mingi iliyopita okay wakati huo pesa zilikuwa mishahara ilikuwa chini lakini anaendelea kulipwa shilingi mia moja na kumi na saba hivi sasa. Hiyo pesa inamsaidia namna gani kwa sasa? Wakati ule ilikuwa ni pesa lakini kwa sasa hakuna chochote.

Naomba ya kwamba au napendekeza kwamba mishahara inapopandishwa juu juu kwa sababu ya hali basi na hizi pension pia ziongezwe ziweze kuwasaidia hawa watu kwa maisha ya wakati huu. Mambo ya hospitali yamesemwa maana lakini narudia ya kwamba haiwezekani watu kuendelea kulipa ndio wapewe madawa, kuweza kusaidia wananchi madawa na mambo ya hospitali yawe ni ya bure. Kuna wazee hapa ambao tunawaita wazee wa kijiji na hao ni watu wa muhimu sana kulingana na mipango yetu ya Kenya. Ndiyo hasa wanaunganisha watu wa kijijini ndio mambo yote ya kutoka serikali yanaingia kwao yakinika kwao yanaenda kwa serikali. Na hawa watu wana kazi ya muhimu sana na wanachaguliwa na watu wenye kwamba ni watu wenye nidhamu nzuri na ni watu wanaofaa. Hawa watu naomba pendeleko langu ni kwamba watambuliwe ama kwa njia ya mishahara au kuna ma allowances sio hata ikiwezekana yawe yanatolewa na County Councils.

Rais asiwe juu ya sheria. Ndio awe na mamlaka kadha ya kwenda kuendesha nchi lakini asiwe chini ajue sheria kama ya kwamba lolote atakalofanya basi yeye hana neno napendekeza pia kwamba mawaziri na permanent secretaries wawe wakipewa hizo kazi kulingana na elimu ya ile kazi. Kama ni mtu ambaye amefanya ukulima basi apewe wizara ya ukulima, kama ni mtu ni permanent secretary pia apewe wizara ya ukulima kwa sababu anao ukulima na anao na anaweza kushauri watu pale. Ni mtu ambaye anatarajiwa kushauri watu lakini ikiwa sasa ni mtu ambaye hata hajafundisha hata sikumoja kama mwalimu anapewa kusimami walimu itakuwa ni vigumu kuendesha hiyo idara. Kumekuwa na ukosefu wa kazi kwa muda mrefu sana, lakini hata kazi zilikuwa zimeanza kukosekana pengine miaka kumi iliyopita na kila mwaka nafasi za kazi zinaendelea kupungua.

Nipendekezo langu kama ya kwamba kukipatikana kazi tuanze kuandika wale watu wa miaka ya tisaini na mbili wakimalizika ili wa tisaini na tatu mpaka tumalizie wa mwisho. Lakini si haki kama kwamba tuache hali ilivyo hivi sasa kama kwamba sababu unajulikana na mtfulani basi ijapokuwa umemaliza mwaka wa elfu mbili na mbili weewe ndio unaandikwa kazi na mtu ambaye aliye sawa na qualification zake ziko sawa na zako na alimaliza mwaka wa tisaini na mbili yeye sasa anaachwa wewe unaandikwa. Kwa hivyo napendekeza kwamba watu wawe wakimaliza wakiandikwa hiyo lot ikimaliza nayo tuanaangalia lot ingine mpaka hivyo hivyo tumalizane. Of course kutegemea elimu na huhitimu kwako.

Pia mambo ya colleges kwa mfano bado kuna watu wanaendelea colleges na colleges zinaendelea lakini bado unakuta kwamba college moja ina watu wengi wa khabila moja kuliko college ingine au kuliko watu wengine. Napendekeza ya kwamba tuwe na ile quota system kama ni watu wa namna hiyo, tribe hii wawekwe number hii yao na wao wapate haki yao hata ikiwamoja amefeli kureport basi tupate mwingine kwa ile ile khabila, kwa ajili hiyo tutakuwa na usawa na namna hiyo napendekeza nikitambua kazi ya madiwani kama ya kwamba baada ya miaka kumi sawa na MPs wasiweze kupewa pension. Kazi yao kwanza ni very taxing kama ya kwamba si haki wenzao MPs baada ya miaka kumi wanapewa pension na wao baada ya miaka kumi hata ishirini wengine. Benson Mabwange alikuwa hapa na wanataka hivi hivi na hawana njia ya kupata shukrani. Hilo ndilo

pendekezo langu kwamba na wao baada ya miaka kumi wapewe pension.

**Com Ratanya:** Asante sana bwana Crispin Mwaisege kwa maoni yako na nafikiri atakayefuata bwana Gibson Mwasongo atakuwa ni mwisho kwa sasa nafikiri baada ya bwana Mwasango kutoa maoni yake tutapumzika kidogo na tatarudi baada ya nusu saa hivi kuendelea.

**Mr. Gibson Mwasongo:** Asante mwenyekiti majina kamili ni Gibson Mwasongo kutoka Maundo sublocation. Nina memorandum hapa nitasoma tu kwa muda mfupi. Rasilmali, wanyama, pori, ardhi, maji, utalii na misitu zirudishiwe wenyiji wa Taita Taveta na hiyo mbuga ya wanyama ambayo ni asilimia sitini na mbili ningeomba robo tatu irudishiwe kama mwananchi na hiyo robo moja iwe Game Reserve. Utawala wa mikoa iondolewe kwa hivyo tunataka serikali ya demokrasia ya majimbo. Tukiwa na serikali za mitaa.

Tuwe na rais, waziri mkuu, mbunge, diwani na muungano wa vijiji. Tunadai vyuo vikuu katika mkoa wa pwani. Elimu ya zamani iliofutiliwa 7-4-2-2 turudishiwe. Tunadai mipaka ya wilaya ya Taita Taveta irudishwe wenyewe. Waliostaafu wasiwe wanapewa jukumu ya kusimamia miradi iliyoko wilayani. Zahanati za watu binafsi tungeomba wakati ujao zifunguliwe mbali zibaki za serikali. Kufuatana na mila za Kitaita mahari kwa Wataita yarudishwe yale ya zamani na kodi za wazee ziwekwe.

Tume ya uchaguzi uwe uhuru na haki. Kura itegeme maoni na walio wengi. Tukichagua, wakati tunachagua tukichagua mbunge asiende akapewa kazi ingine huko mbele maana sisi huwa tunapeleka wabunge hatupeleki mawaziri kwa hivyo wangoje wawe wanachaguliwa mbele ya bunge, nje ya bunge. Kwa upande wa uridhi, wa mali kila mtoto achukuliwe kama sawa. Yaani kila moja apewe right yake akiwa ni wa kike akiwa ni wa kiume. Kufuatana na yale mashauri ya shule ningependekeza wawe wanachaguliwa wale amba wako na watoto kwa mashule hayo. Nikimaliza hii landboard ihusishe wanawake kwani huwa tunaona wakichaguliwa wanaume peke yake na mambo yetu ya ardhi yaye yanafuatiiliwa hapa wilayani sio huko Nairobi. Kwa hayo machache asanteni.

**Com Ratanya:** Asante sana bwana Gibson Mwasongo kwa maoni yako. Sasa basi tupatie nafasi ya kupumzika kunyosha miguu na turudi hapa kiasi cha saa tisa kasorobo tafadhalini. Wananchi ni heri tuanze sasa. Wale amba wako nje waingie halafu tuendelee. Sasa tuna Peter Salai, Peter Salai yuko hapa?

**Mr. Peter Salai:** Majina yangu mimi ni Peter Salai katika kata ndogo ya Taita Taveta. Kwa hivyo, Katiba ikiwa kwa kisheria. Sehemu zilizotengwa zifadhiwe sheria kando ya vijito. Kuna viwango ambayvo havitakiwi kulimwa teremko zaidi, wananchi wafanyiwe mpango sehemu za chini sambarare hasa katika pahali palitengwa pakuitwa National Park na mteremko hiyo upandwe miti zaidi ya kiasili hapa inayohusikana na madawa ya kienyeji. Kuhusu elimu ya msingi, wanafunzi wasomeshwe lugha ya mama yao Kitaita kutoka darasa la standard one mpaka standard sita.

Elimu igharamiwe na serikali hadi kidato cha nne pia welfare yao iangaliwe. Taasisi za kidini ziwe zikipatiwa kiasi fulani kutokana na mfuko wa government, kutokana na kodi itokayo kutoka kwa uma. Taasisi za kilimo na ufundu zipanuliwe kifedha na kitaalamu. Rasilmali kutoka Jimbo hili sehemu kubwa igawiwe jimbo zilikotoka. Mashamba yaliyotoka lease, iliyoko kwa lease ya miaka elfu mia tisa na tisaini na tisa ziondolewe kufuatia katiba mpya. Asante.

**Com Ratanya:** Okay asante sana bwana Salai. Sasa tunaendelea kwa Ephraim M. Josiah.

**Mr. Josiah:** Asante sana mwenyekiti na maafisa wetu amabo mmeefika hapa Werugha kanisani. Majina yangu ni Ephraim M. Josiah. Mimi ni kama mzee wa makao. Jambo langu nazungumza hivi ni ya binafsi mwenyewe. Nataka hivi skuli zetu zote zipatiwe nafasi kusije school fees kuondolewe kabisa. Kwa sababu kuna watoto ambao wamezaliwa wengine hawana baba zao hawana ndugu zao wa kuwasaidia kwa hii wakufanya mtihani wakipita wanakosa na hivyo tunawatupa kabisa na ndio ambao watakuwa ma D.C. na ma D.O ama P.C. hapo nimemaliza.

Sasa niende ya pili, ya pili binafsi nataka hivi kama serikali iko na uwezo ituangalie kwa mambo ya matibabu. Watu wengi wanakufa huko nje katika hospitali. Hajaangaliwa hana pesa, au hana kitu chochote anazungushwa zungushwa huku na huku anapimwa anaambiwa dawa utanunua ukuje siku fulani na hakuna hana pesa atoe wapi. Hilo jambo napendekeza serikali ituangalie gharama za madawa ikiwa kwa wingi. Sina pendekozingine, hayo ndiyo mapendekezo yangu mawili ambaye ningetoa. Na ninakomea hapo sitaki kuendelea zaidi.

**Com Ratanya:** Okay asante sana Ephraim Josiah kwa hayo maoni yako sasa tunaendelea kwa mwingine hapa George Sabonja, karibu hapa.

**Mr. George Sabonja:** Honourable Commissioners na wananchi. Niko na machache hapa ningependa kupendekeza lakini ni ajabu mambo mengi nimeandika hapa watu wameshaandikisha katika memorandum zao. Lakini hiyo hata hivyo hawezi kunizua kupeleka mbele mambo yangu niliyo nayo. Jambo la kwanza, kwa jina ni George Sabonja. Jambo la kwanza katika nchi yoyote na katika kimila za kiafrika si vizuri in future, kuwe na maPresident ama President wa baadaye kuwa bila bibi. They are supposed to have wives. Msimamo na utawala wa maisha unaanzia hapo. Ukiwa kama namna hiyo unakuwa kama cowboy sasa mambo haiwezi kuwa mzuri. La pili ni kwamba sisi watu wa pwani kabla sijapendekeza tumetazikika vya kutosha kulingana na mpango ilivyokuwa inaendelea tangu wakati wa uhuru. Utaona matatizo mengi yameonekana hapa pwani, umasikini umezidi ukiwa pwani yenye iko na resources nyingi na watu hata kuna matajiri, lakini utaona ya kwamba mambo imekuwa ngumu hasa sababu ya kuwa na huo uchungu wa aina hiyo.

Mimi napendekeza a federal system of government other than this Presidential one. Na watu wanaanza kuuliza federal system maana yake ni nini? Leo nasema kwa ufupi ni majimbo na ninapendekeza wakati huo huo ya kwamba katika hii nchi ya Kenya tuko na majimbo nane. Isipokuwa moja ambae zimezidi kipimo ya Rift Valley sijui lengo la kuwa na hiyo area kubwa namna hiyo karibu thirteen districts while other provinces ziko na five si vizuri sana kwa macho ya wananchi. Ningependekeza Rift

Valley Province iwe divided into two areas North Rift Valley and South. Nikiwa hapo hapo kwa majimbo ni kwamba sisi watu wa pwani ama sehemu zingine za Kenya kwa hayo majimbo tisa hiyo ingine ikagawanywa kila watu watakuwa na mamlaka yao ya kujitawala na kujimudu na kusimamia mambo yao ya kiuchumi, ya kisiasa hata ya kijamii.

Nanitapendekeza ya kwamba kutakuwa na President huyo central government mpaka ikuweko, tukiwa na hiyo Central Government, hawa wa central government zitagwanywa katika region ambapo itaweza kuwekwa katika kila region iwe pengine ina governor whatever they might call them lakini nafikiri njia nzuri ni kuwa na wale magovernor halafu katika wale magovernor kutakuwa na regional assembly Mombasa kama hapa in case of war na other areas namna hiyo. Tutakuwa na bunge letu hapa, tutakuwa na wote watachaguliwa hapa kwa wabunge kutoka district tano ziko hapa pwani wawe na bunge huko Mombasa. Coast province ina resources nyingi lilo lingine wamelisema.

Tuna wildlife and tourism, tuko na hali ya maforest, minerals ziko nyingi na nitasema ya kwamba katika hii province ya Mombasa ukuwe headed na governor huko Mombasa rasilmali kama kwa mfano, kama ni minerals, natural resources zozote zikipatikana waretain 75% of those resources 25% wapeleke kwa central government. Hiyo 75% kutakuwa hizi local authority kama County Council watoe 25% wapeleke kwa mwananchi hapa the remaining afanye administration ya serikali ya pwani.

Na kabla sijaenda mbele pia ningetaka kupay tribute kubwa kwa R.G. Ngala wakati wa independence day, tukupata uhuru hata ile katiba ilitoka Lancaster ile ya mwisho ilikuja na majimbo. Kile kipengele kilikuwa ndani wale ambao hawajui lakini ilifanya kazi kwa muda wa mwaka moja kidogo wenzetu wa kutoka juu wakaona ya kwamba ah hata hii serikali za namna hii tutaweza kujenga Mombasa kweli, tunaweza kuishi Mombasa kweli? Wakatupilia mbali lakini tulijua ilitupuliwa mbali kwa manufaa ya watu binafsi ambao hatuwezi kuwataja hapa lakini haikuwa vizuri. Kitu kama namna hiyo ninapendekeza nikizingatia juu ya majimbo ni kwamba katika ule utawala wa rais ambao nimesema nitarudia wawe na mabibi the future government powers zio ziwe more ceremonial na kazi yao kubwa ya kiserikali iendeshwe na waziri mkuu. Katika hiyo hiyo Central Government tuwe na Upper and Lower House, Senate and Lower House hii ya House of Representatives amba ni present members of Parliament. Wakilishi Kenya nzima hata hapa tuchaguwe house of representatives ja wabunge wetu tutapeleka huko. Si ati tukiwa na hizi serikali za region hatutakuwa na wabunge huko, watakuwepo, investors bwana commissioner.

### **Com Ratanya:** Hebu jaribu kumaliza

**Mr. Sabonja:** Namaliza nikisema investors, kama serikali za namna hiyo za majimbo itabuniwa watakulaliwa wazungu, wa-Asia kutoka wapi, other regional governments zitakuja ili ziweke rasilimali zao hapa. Wale already ambao wanaproperty si ati watapokonywa watacalculate kwa sababi halipi tax katika hizi manyumba na utakuta mtu mmoja ako na estate kutoka hapa mpaka hapo barabara. Zingine ziko Eldoret, zingine ziko Nyeri, zingine ziko wapi. Sasa utakuta hakina tax hata moja inakuwa kufanya namna hiyo commissioner utakuta ya kwamba rasilimali nyingi zilitengwa. Na tutapunguza hii eradication of poverty katika Kenya. Itaweza kufanya kitu gani kama mambo kama hayo hayafulawi. People don't pay tax hawalipi wanaishia namna

hiyo na kuendesha magari yale makubwa, makubwa na mambo kama hayo. Nafikiri nimepata neno hapa, nafikiri nitafikia hapo.

**Com Ratanya:** Na una memorandum

**Mr. Sabonja:** No.

**Com Ratanya:** Okay asante sana kwa hayo maoni yako George. Sasa tutaendelea kwa mwingine anayefuata Abednego Kitambo

**Mr. Kitambo:** Asante bwana chairman. Niko na mapendekezo hapa na mapendekezo haya ni ya vijana wa kata ndogo ya Sagasa.

**Com Ratanya:** Wambie jina lako kwanza.

**Mr. Kitambo:** Jina langu naitwa Abednego Mwarenge natoka Werugha.

**Com Ratanya:** Mwarenge au Mwarege

**Mr. Kitambo:** Mwarenge

**Interjection:** Zala

**Mr. Kitambo:** Natoka kata ndogo ya Werugha ambayo iko kwa kata ya Werugha yenye. Mapendekezo hapa ni ya vijana wa sagasa waliopata elimu kuhusiana na katiba na basi wanakaa kujadiliana na katiba basi wakasema na wakapendekeza, wakapendekeza kama wapasavyo. Pendekezo la kwanza vijana hawa walipendekeza ya kwamba katiba mpya itungwe na wananchi na iwe ni yetu ileze lengo, ndoto na shabaha za wananchi hii inamaanisha ardhi yetu, na rasilmali zetu zote ambazo tulipokonywa siku za ukoloni mamboleo.

Mwananchi awe na haki ya kuwa na nakala ya katiba ambapo apewe kitambulisho ya katiba kwa wakati huu. Hii inamaanisha kwamba kila mwananchi anapokuwa mtu mzima aweze kupewa nakala ya ile katiba ili aweze kusoma na kujua katiba inasema namna gani. Kitambulisho iwe lazima pia, iwe na kadi za kura. Kitambulisho hicho kitakachokuweko kitaamanisha kitatumika hata kupiga kura na hivyo basi hakutakuwa na kadi za kupiga kura bali kila kitambulisho mwananchi atakachopewa kitatumika hata kupiga kura.

Pendekezo lingine katiba iwe na haki za wananchi za binadamu. Kizazi cha kwanza, cha pili na cha tatu. Hii inamaanisha haki za kimsingi, haki za kiuchumi na haki za kidemokrasia. Pendekezo la nne, utawala wa demokrasia wa majimbo ambapo serikali za

mitaa, County Council ziwe na uwezo zaidi kusimamia rasilmali zote katika wilaya kwa manufaa ya watu. Hii inamaanisha rasilmali ardhi, mashamba, madini, maji, misitu, wanyama wa pori na kadhalika.

Tano, utawala wa amirisha ndani ya administration na afisi zake ziondolewe. Yaani chief, diwani, D.O., D.C., na P.C., ziondolewe kabisa. Ni wa kikoloni na ukoloni mamboleo ambapo hatutaki ukoloni wa wale administrators. Vijana wetu wanapendekezo zaidi kuwa na viongozi wakuchaguliwa nitarudia. Kuwe na viongozi wa kuchaguliwa ambaa watakuwa ni wa viongozi wakilishi, Diwani, Mbunge, Waziri Mkuu na wote wawe na mishahara.

Pendekezeo lingine kuwa na msimamizi wa dola ambaye si msimamizi wa serikali. Msimamizi wa dola ni yule msimamizi wa state kama rais. Lakini sio serikali bandikwe awe anasimamia state na maswala ambayo yanamhusu. Pendekezo lingine kusiwe na uelekezaji wa mamlaka na kuwe na utawala wa sheria ambako watu wote nchini wako chini ya sheria na wanashitakiwa hapo kwa kila mtu chini ya sheria iwe ni rais iwe ni nani. Na yote ambaye ataenda kinyume cha sheria aweze kukabiliwa na sheria ipasavyo kuwe na uwazi na uwabizaji wa kila kiwango kwa kila kiwango ama kila kazi. Maswala yote ambayo yanawahuhsu wananchi yaweze kuelezwu kiwazi na kila mwananchi aweze kuelewa. Kuhusu serikali mawaziri wachaguliwe na waziri mkuu.

Pendekezo lingine mawaziri wachaguliwe nje ya bunge kulingana na taaluma zao, kulingana na taaluma. Na serikali iwe imehitim. Waziri mkuu achaguliwe kwa wengin wa kura. Vijana walipendekeza awe na percentage ya 55 ama asilimia sitini na tano ya kura zote zilizopigwa kutoka majimbo halafu awe na percentage ya kura zote nchini kuwe na bunge, bunge iwe juu ya kila mtu ameteuliwa. Bunge hiyo ichaguwe tume ya kuajiri nchini ambaye itaajiri wabunge katika afisi zote za uma. Pendekezo lingine bunge iwe ya kutoa kauli ya mwisho isipokuwa na maswala yanapatiliwa kwa kura ya watu wote kwa mfano kubadilisha katiba. Hapa inamaanisha ya kwamba bunge haitakuwa na mamlaka, kusiwe na kuchaguliwa kwa watu ofisi. Bunge ikiteuwa imeteuwa na serikali iundwe mara moja na mahakama yawe huru katika kazi.

Waziri wote na watu wote waweze kushitakiwa katika mali kama na uhuru na haki kuondolewa. Either waziri na waziri mkuu pamoja na rais wawe wanashitakiwa wanapokosa. Majudge nao waweze kushitakiwa wakosapo. Rasilmali zote za kumiliki za wenyeji za wilaya zinahusika sehemu hizo, County Council. County Council zote ziwe katika katiba na maelezi yenye chini ya Local Authority, mapato yote yanapatikana kupitia wanyama wa pori yaingia County Council ya Taita Taveta kwa manufaa ya wenyeji. Kuwe na haki ya ajira ya vijana. Vijana wapewe ajira wawe wakipata mshahara ili waendelee kihali ya kiuchumi jinsi ya kupata chakula, pia ya msingi ya kuongoza na kuongeza nafasi za kazi. Katiba iandikiwe kwa lugha ya kiswahili na wenyeji kama lugha ya kitaita, Giriama, Kikuyu, Kiluyha. Vyombo vya habari vyote viwe vya kutoa habari sahihi kusema kweli bila vitisho wala kuungiliwa hii inamaanisha radio, magazeti, runinga na njia zote zile tunapata habari. Bunge iwe inasikiliza moja kwa moja kupitia radio na runinga. Ishirini na nane mbuga za wanyama wa pori na masako ambapo inachukuwa asilimia ishirin na mbili ya ardhi ya Taita Taveta iwe na malipo ya ujenzi wa Taita Taveta.

Game Reserve na iwe na 95% yaani iko percent ya ardhi ya Taita Taveta ambayo iko na national park waweze kukata 25% iwe Game Reserve na 75% or 62% uwezwe kugawanywa na wale wananchi wenyewe itumiwe kwa kazi zitakazowafaa kwa ujenzi wa taifa, sheria za madini zibadilishwe ziwe zikichimbwa na wenyeji. Number three mfumo wa elimu ubadilishwe, kuwe na darasa la saba, kidato cha nne, kidato cha sita na chuo kikuu yaani system ya zamani ya 7-4-2-3. Inaonekana mfumo wa siku hizi una maneno mengi, halafu ninamalizia hapo ndio kumaliza namaliza hapo kwa nina mapendekezo ingine ya individual.

**Com Ratanya:** Tutasoma memorandum

**Mr. Kitambo:** Haya ni mapendekezo ya mtu binafsi

**Com Ratanya:** Okay you have been registered twice here so one is for the group and one is yours.

**Mr. Kitambo:** Individual

**Com Ratanya:** Okay

**Mr. Kitambo:** Mapendekezo hayo nimepatiwa kwa niaba ya mtu binafsi. Sawa nikiweza kuwa na mzee huyu na alikuwa aketi hapa lakini kwa sababu ambazo hazikukamilika kabla hii mkutano akasema mimi nitakutuma wewe ikiwa muhimu nikutume wewe kama vile unaweza kufanya ili kuyafikisha mapendekezo. Mzee huyu amependekeza kwamba

**Com Ratanya:** Sasa jina lake

**Mr. Kitambo:** Jina lake anaitwa Jefferson Mwakio Kisaka ndilo jina lake.

**Com Ratanya:** Si jina yako tu nimeandika.

**Mr. Kitambo:** Ni yangu imeandikwa lakini mapendekezo haya si yangu

**Com Ratanya:** Kwa hivyo unataka jina yako iwe chini tu kwa list yetu iandikwe huyo mwingine.

**Mr. Kitambo:** Fine, fine.

**Com Ratanya:** Kwa hivyo huyu anaitwaje

**Mr. Kitambo:** Jefferson

**Com Ratanya:** Jefferson

**Mr. Kitambo:** Jefferson M. Kisaka

**Com Ratanya:** Kisaka okay, endelea sasa.

**Mr. Kisaka:** Huyu anaweza kunituma hangeweza kufika hapa lakini amenisihi jana chochote kile amependekeza nikiandike hivyo na niweze kusoma hivyo kabisa. Ameomba sana kusikilizwa kwamba chief manaibu wa machief hata ma-DO pamoja na maCouncillors waweze kuunda mamlaka ya kiasi ama kwa kizungu tunasema powers. Sababu wengine wanatumia mamlaka haya yao hata kwenda kudhulumu wengine ambako wanaishi. Pendekezo la pili amesema ya kwamba sheria ya ardhi uweze kusimamiwa na tume unayoihusu na sio wale watawala.

Mambo ya ardhi yapewe watu wa ardhi kama ni watu wa lands or whatever but the other leaders like D.O., chiefs, they should not engage in such affairs. Pendekezo la tatu mwananchi awe na haki ya kujieleza ama ya kujieleza shida yake kusiwe na kitu chochote. Njia yoyote iwezwe kubuniwa ama kutafutiwa ili kwamba mwananchi yejote hata yule ako mashambani kule aweze kusaidiwa, kupendekeza ama kupeleka tabu yake. Kuna wengine wana maswala yao ya taabu lakini akipeleka ifike mahali yanazuiliwa. Pendekezo lingine amesema ni ya kwamba tunajua ya kwamba katika Kenya hii mwananchi yule ana cheo chochote katika serikali pengine ni wa kuijendeleza kabisa na kadhalika. Kuna mahali atakapoingia na akitaka kufanya maendeleo yote zaidi kuna vita hata utapata hata akiingia mahali atabidi pengine aambiwe atoe hongo ama kulingana na mamlaka ya mwininge aweze kuzuia mambo ama mlango yake. Kwa hivyo anapendekeza ya kwamba kutafutiwe namna ama njia ni kama hii ya kwanza ambapo malalamiko ya mwananchi kama hivyo yanawezwa kusikizwa.

Mwananchi ambaye yuko kule interior hata pengine hajawahi kutoka njia ifanywe ana namna hata kama ni tume ibuniwe ya kutumikia mwananchi kama hivyo aulizwe ana taabu gani na aweze kuelezea. Pendekezo lingine amesema ni kwamba swala la rasimali liweze kuangaliwa kuna watu kando na yeye amba wana mashamba yao na yana rasilmali nafikiri wamefikiwa mahali na ikabidi pengine kulingana na mamlaka kama ni machief kama ni ma Councillor ama whoever, ujumbe huu wanatumia mamlaka hayo wakifinya au kupokonywa rasilmali hizo ama kuzuiwa asichimbe mali na hiyo mali au madini yako kwa shamba yake.

Pendekezo, amependekeza ni kwamba njia ziweze kufanya ili waweze kusaidia wananchi kama hao kwa njia yejote mwananchi ambaye ana shamba kubwa ama ana rasilimali yake iweze kuhifadhiwa na yeye mwenyewe aweze kufaidika. Asanteni.

**Com Ratanya:** Okay asante sana Bwana Munau kwa hayo maoni yako ya group pamoja na hayo mengine ya huyo mzee mwininge. Okay sasa tutaenda kwa mwininge anayefuata ni Ronald Mulawi. Ronald yuko?

**Mr. Ronald Mulawi:** Matume ya uchaguzi na wananchi maoni ya Werugha ni maoni yetu Werugha kutoa maoni ya kutokana na tume ya katiba ya Kenya. Majina yangu ni Ronald Mulawi ni maoni yetu ya Werugha kutoa maoni ya tume ya marekebisho ya katiba ya Kenya. Kenya tulipigania uhuru na tulupata uhuru kitambo lakini sasa tunagandamizwa na serikali ilioko sasa mamlakani natulipata uhuru. Kwa hivyo tunadai haki zetu kama vile ardhi, rasilmali turudishwe na tupatiwe title deeds na hii mbuga ya kitaifa ambayo ni national park iwe ni ya Wataita, imilikiwe na Wataita kwa manufaa yao wala si ya kitaifa.

Rasilmali kama vile maji na madini inatakikana iwe huru. Watu wawe na ofisi ambaو unashimamia kiti hiyo, kwa sababu hiyo ya kulemewa wa unyakuzwi wa ardhi na rasilmali kunyakuliwa unaitisha serikali ya majimbo. Kutokana na yayo tunaitisha serikali ya majimbo ambayo itafuatiliwa katiba hii mpya na muongozo mpya. Utawala huuu utakuwa na ngazi kwa tawi. Kijiji wakilishi na divisheni na D.C., mbunge wa zote. Kura zitakuwa kwa uamuzi. Waziri atachaguliwa kulingana na taaluma zake. Awe ni raia wa Kenya kwa usomi, form four leaver, afya nzuri na kipindi cha miaka kumi. Miaka mitano halafu akifanya vizuri iwe ni kumi.

Na mgombania kiti cha bunge au rais awe ni miaka 30. Na mwisho wa kugombania awe miaka sitini, apate kura nusu na awe chini ya sheria, asiwe na mamlaka kama ya hivi sasa serikali ilivyo. Awe chini ya sheria na wananchi.

Aina ya uchaguzi hivi nafikiri huru na ya kidemokrasia na akikosa adhibiwe. Kumtoa kiongozi kwa uongozi kama vile akikosa akipigiwe kura ya kutokuwa na maoni. Utawala wa mikoa viondolowe na kuweka majimbo ili rasilmali zikamilifu kwa dola ya Kenya itakuwa wa mahakama, serikali ya bunge, kuna senate na representative, kuwe na mahakama na sheria naiwe ombudsman.

**Com Ratanya:** Ebu jaribu kumaliza dakika zako ziko karibu kwisha una dakika moja.

**Mr. Mulawi:** Elimu, kielimu tumeachwa nyuma kwa sababu ya unyanyasaji, hatujakuwa na chuo kikuu, na inapaswa tupatiwe huduma za serikali bure na barabara ya jina wa watu kwa sababu ya rasilmali na mfumo wa elimu ubadilike kwanzia standard one mpake seven halafu form four, form six halafu chuo kikuu. Na masomo ya standard one na four ifundishwe zaidi. Na wale wameretire wasikubaliwe kuhudumu tena ofisini wapatie vijana.

**Com Ratanya:** Naona kama masaa yako yamekwisha, peana memorandum yako kama unayo. Na asante sana bwana Ronald sasa nitaenda kwa mwingine. Mwanyanje Nyambu yuko? Mwingine ni, kama huyo hayuko tuna mwingine Ludorick Mwanandime.

**Mr. Ludorick Mwanandime:** Kamati yote kwa jumla hamjambo? Mimi kwa majina ni Ludorick Mwanandime. Langu ni kwamba niko hapa kwa group ya FEP inamaanisha Frier Environmental Project. Kama vile tumesikia kwamba ikitangazwa katika maredio kuwa kuna misitu ya watu binafsi huko kwetu ambako ni Frier kuna msitu ambaو ni msitu wa wazee wetu ambaو waliuhifadhi tangu hapo zamani lakini baadaye ilikuja ingeliwa na wale walioingilia, walichaguliwa sana, wakikata miti yaana bila kujali hivi ndipo sasa tunaomba kwamba wakati huu mashamba hizo au msitu huo ipitishwe katika katiba mpya

kwamba wenyewe msitu huo wausimamie wenyewe. Waendelee kusimamia msitu huo wenyewe kama walivyokuwa wakiusimamia hapo awali. Maana kwa kweli mtu anaposimamia haki yake hawezи kuharibu. Lakini inapoingilia na watu wengine wataharibu na ikiwa kila mahali inasemekana ya kwamba kila mtu ana haki na mwenye haki yake huwa chini yake tunashindwa hapa kwetu kwa nini haki zetu zinataka kunyanyaswa na watu wengine. Zikifanyiwa mpango ili zikapatwe kuchukuliwa na watu wengine, kwa hivyo tunaomba kwamba ikapate kusimamiwa na wenyewe. Tupewe ruhusa ama iandikwe kabisa katika katiba hii mpya.

Mali ya Mwandime iwe ni mali ya Mwandime na mali ya Mwakio iwe mali ya Mwakio bila kuingiliwa. Lingine nililo nalo ni kwamba mambo juu ya imani. Watu wawache kila mtu awachiwe uhuru wa kuabudu kwa sababu utakuta wengine wanaenda kwa waganga. Mtu anapoenda kwa mganga hakuna mtu anyemwingilia ama anayemfuata na kumuliza kwa nini mtu huyu amekuganga kwa muda mrefu. Lakini mtu mwingine anayeamini kama hapa mahali tumekuwa, tumekaa kanisani na humo kanisani hapa hapa kwa Bibilia ya katibu. Bibilia ndiyo kitabu cha Zaburi mia na tatu inasema akusabeba umri yako yote ako pamoja na magonjwa yako yote, sasa katika hiyo utakuta mtu mwingine anawekea anapangia kiwango cha kuabudu. Inabudu kidogo unamwambia hivi wacha hivyo usiendelee sana. Kwa hivyo tungeomba kwa katiba mpya iweke tu uhuru wa kuabudu. Tungali tusiwe ya kwamba ati mtu anaua mtu mwingine pengine kama ni kuamini ni amini na nina siku takatifu. Kwa nini niingiliwe? Kwa hayo machache Mungu awabariki.

**Com Ratanya:** Okay asante sana bwana Mwandime kwa hayo maoni yako na tena tutanenda kwa mwingine. Tumeamaliza. Asante sana, maoni mazuri sasa twende kwa Eleston Mwakio, Malazi Ulura, na sasa mumeona kumekuwa usiku kabisa mjaribu kuleta mapendekezo tu, maoni yako na halafu yachukuliwe si useme mambo mengi yale unaweza kuwa unarudia. Kwa hivyo kama Malasa hayuko, Malazi Uhura yuko? Twende kwa Reuben Mogenga. Kuja utawambie kwa ufupi kama una memorandum utaweka pale na tutakuwa na nafasi ya kuisoma. Kwa hivyo useme kwa ufupi. Just give the highlights.

**Mr. Reuben Mogenga:** Kwa jina ni Reuben Mogenga na ninawakilisha kati ndogo ya Mavunge. Mengi yamekwisha semwa na waliotangulia. Nami nitasema mawili au moja tu. Moja mkazo ambayo ni ya mbuga hizi za wanyama. Tangu hapo ilisemekana kwamba 62% ndiyo inatawaliwa na wanyama kwa hivyo sisi tunatia mkazo ipunguzwe iwe 40% na 22% irudishwe kwa wananchi iongezewe na wananchi wapewe hiyo mahali iyo shamba na ile ingine ichukuliwe na County Council kwa sababu sisi tungelikuwa hata tuweze kupata pesa kutoka huko lakini serikali imekuwa ikipokea hizo sasa tunakaza mkazo kwamba County Council ipewe senti kutoka hapo zaidi ili iweze kusaidia Taita Taveta districts. Nafikiri kwa ufupi.

**Com Ratanya:** Asante sana bwana Reuben peana memorandum yako na sasa tuenda kwa Holiness M. Ndumwa, hayuko? Kama Holiness hayuko twende kwa Luciana wachienye upande wa akina mama sasa, sasa hata kama huyo hayuko tuendelee kwa mwingine. Victoria Lavela, Victoria Lavela hata huyo hayuko, Clement Mwamburi, Nicholas Wandogo. Ni wewe Nicholas uje useme kwa ufupi naona hata mvua inatifuata. Sema kwa ufupi na kama una memorandum yako upeleke pale. Wambie kwa ufupi yale unayo.

**Mr. Wandogo:** Asante bwana mwenyekiti. Maoni yangu ni juu ya urekebishaji katiba.

**Com Ratanya:** Aanza na kusema jina lako.

**Mr. Wandogo:** Jina langu naitwa Nicholas Wandogo.

**Com Ratanya:** Endelea.

**Mr. Wandogo:** Maoni ni urekebishaji katiba ile ya kwanza. Elimu iwekwe juu ya katiba ili kila mtu aweza kupata elimu ya msingi mpaka chuo kikuu bila kutatizwa na mambo ya karo. Kwa sababu watu wengi au watoto wetu wengi wameshindwa kwenda mbele kwa sababu ya ukosefu wa elimu na ninaweza kusema ya kwamba hapa karibu nusu ya watoto wetu hawajapata elimu ya kutosha kwa sababu ya karo. Number two, katiba ihakikishwe ya kwamba wananchi hawakosi madawa au matibabu yoyote yale kwa sababu ya ukosefu wa pesa katika hospitali .

**Com Ratanya:** Kwa hivyo unatakaje?

**Mr. Wandogo:** Nataka wananchi wawe wanapata matibabu ya bure kama vile wakati wa ukoloni. Katika katiba mpya iweke wazi kwamba polisi waheshimu watu ambao wamezaliwa wana makosa kwa sababu wakati mwingine polisi wanawadhani watu wanamakosa wanawachukuwa kama maadui zao. Hawachukui kama watu ambao wanaoishi nao pamoja. Kuhusu mambo ya mashamba, kuna watu walio na mashamba makubwa makubwa na hawayatumii. Mtu yejote asije asiruhusiwe kuwa na zaidi ya acre ishirini maana hiyo haiwezi, itakuwa zaidi kushinda wenzake wengine. Kuhusu uridhi wasichana wawe wakipatiwa uridhi na wazazi wao au na serikali sawa na watoto wa kiume. Asanteni nimefika hapo.

**Com Ratanya:** Okay asante sana bwana Nicholas kwa hayo maoni yako mazuri uende pale upeane maandishi yako na sasa tunaenda kwa Moka Chorongo ni wakati wake sasa. Kama hayuko twende kwa mwingine, Patrick Mwakula.

**Com Ratanya:** Useme tu kwa jina

**Mr. Patrick Mwakula Kinyambura:** Namwamkuwa hamjambo? Kwa jina langu mimi naitwa Patrick Mwakula Kinyambura. Tuseme maoni yangu nasema kwa kuhusu mambo inahusiana na elimu. Tuseme elimu hii ya Kenya mtu yejote amepitia kuptita kwa elimu kutoka kwa daktari, hata kutoka kwa mbunge hata kutoka kwa rais. Mimi napendekeza kama inawezekana elimu iwe msitari wa mbele kutengwa pesa za kutosha hata watu kusoma elimu ya bure kutoka kwanzia standard one au nursery mpaka university kwa sababu hapo ndio tunaanza kupata daktari, tunaweza kupata hata judge, hata rais kwa sababu amepitia kwa elimu. Na wa elimu wenye sababu ndiyo chombo cha kwanza kuendekeza nchi yetu ya Kenya wapatiwe mshahara wa kutosha ambao wapate kutelimisha vizuri.

Yes, jambo la pili kuhusiana na maneno hii ya afya, hii afya inatakikana naye akiwezekana itengewe pesa za kutosha ambapo hizo pesa zinaweza kusaidia mwananchi yeyote katika Kenya apate kupata matibabu ya bure. Sasa iki ja sikia tena jambo lingine la tatu katika Kenya ni wizara hii ya kilimo ni wizara muhimu ambayo nayo inatakikana iangaliwe ipatiwe pesa za kutosha kuangalia masilahi ya mwananchi saa ile sisi tutakuwa tunakosa chakula. Iwe inajua ni ardhi gani ambayo inaweza kupaa kwa kilimo na tupate chakula cha kutosha.

**Com Ratanya:** Jaribu kumaliza

**Mr. Kinyambura:** Halafu sasa tukija tukifikia kama sehemu ya mkoa wa pwani tunaona tena matatizo ya kutosha. Kwa sababu ukiangalia hata kuanzia sehemu za Mombasa, kwanzia sehemu hata Lunga Lunga mpakani na Somalia ukiangalia watu wengi sana ni wasquatter. Hawana ardhi za mwananchi ambaye wanaweza kumlinda hata ukapata Title deed. Na sisi tunaomba, kama inawezekana hiyo mambo ichunguzwe kwa vizuri na wananchi hawa wapatiwe haki zao. Wapatiwe title deed. Na sehemu za wanyama wa pori, Coast nzima wanasema hata sehemu za Tanga mimi najua huko kuna wanyama na wale watu wanaoishi sehemu hizo pia nao wananyanyaswa kama hapa kwetu Taita.

Sehemu hizo nasema zirudishwe kwa wananchi iwe Game Reserve. Ikishakuwa Game resereve iwe chini ya County Council. Kisha ikisha kuwa hivyo, kama ni ardhi inataka kutolewa kwa wananchi wahame ikiwa ni kwa kilimo, ikiwa ni kwa nini hiyo ni manufaa kupitia kwa mkono wa County Council. Yangu ndio hayo.

**Com Ratanya:** Asante sana bwana Patrick unaweza kwenda pale uandikishe. Sasa tuna mwingine anayefuata ni Ahariel Mwandime. Mwandime tuambie point zako kwa ufupi.

**Mr. Ahariel Mwandime:** Nitajaribu, kwa majina yangu naitwa Ahariel Mwandime. Mimi ni Mtaita halisi kutoka sublocation ya Wundanyi. Kwa mpango wa katiba mpya nataka kusema kwanza mipaka yetu ya Taita iangaliwe sana kwa sababu tunasukumwa huku na huku na tunazidi kubali. Jambo la pili, taifa yetu iondolewe kule mkande iloko kule Taveta isitwe Taita Taveta ni Taita moja kwa moja.

Jambo la tatu, ma President watakaochaguliwa watawale miaka kumi bado na ikiwezekana iwe kicity. City hii ikitawala miaka kumi na city ile itawale miaka kumi. Jambo la nne ni huduma kwa vijana, vijana wakati wanaitwa kwa kazi kuduma, wakati mwingine wale wachukuzi wakija wa huchukua vijana kwa kazi za huduma ningependelea kutolewe mwenyeji wa kule awe akiangalia lugha kwa sababu wakati mwingine huduma itakuja, watu watakuja kuchukuliwa kwa kazi ya huduma halafu wawe wenyewe kuchukuuwa Wataita wenzao kutoka kwao halafu watakuja kuandikisha kama Taita halafu wanaitwa Wataita, lakini kumbe si Wataita.

Jambo la mwisho, pia ni la tano, hospitali za district zinataka zikawe heshima kwa sababu zinataka kuwa na ma doctors kamili

ndani ya hospitali ya district. Si Clinical Medical Officers tu awe hata ni doctor kabisa. Jambo la mwisho, wasichana wakiwa na bahati mbaya apate mimba na amzae mtoto na awe bahati hajapata bwana wa kumwoa baba yake amridhishe mali yake. Mambo yangu imefika hapo mwisho.

**Com Ratanya:** Okay asante sana Mwandabime. Sasa tutaneda kwa Anderson Koronge, yuko? Mwingine ni Mwasae Mwarange. Yata hayuko, John Mwandime yuko karibu.

**Mr. Mwarange:** Wakenya wote mimi kwa majina ni Donald Mwasai Mwarange. natoka mjadala, Werugha, Taita Taveta, pwani. Niko na mapendekezo ambaye wanatokana na mjadala kidogo kidogo mmefanya na wananchi hapa na pale. Na katika sehemu ya kwanza kutokana na mambo ya katiba napendekeza kuwa katiba iweke watu juu ya mambo mengine yote.

Madili, mila na desturi zao ziheshimiwe na ndizo zinakuwa msingi wa katiba ya taifa. Katiba hiyo iandikwe kwa lugha za wenyeji, lugha ya kitaifa kiswahili na iwe rahisi kueleweka kwa kila mtu. Pia katika katiba shabaha na lengo la watu zielezwe zikizingatia hali ya kuingia kwa mapambano ya kuondoa ukoloni mamboleo kwa kuondoa utawala wa mkoa wa machief, ma – D.O., ma – P.C., ma – D.C., ambalo twaliona ndilo lilokuwa lengo kuu la wapiganaji uhuru kama ilivyo tangazwa katika sabaha na maongozi ya chama cha Kanu mwaka wa elfu moja mia tisa na sitini.

Tawala zitakazopishwa baada ya kung'oa ukoloni mamboleo ni tawala shirikishi za demokrasia kila ngazi kuanzia nyumbani, vijiji na miradi yote, kata na miungano yote ya kundi katika ngazi hiyo ambapo tutakuwa tukichagua kiongozi wa siasa kwa jina la diwani. Kwa ngazi ya constituency, tuwe na mbunge na tuwe na mkao wa wilaya ambao utakuwa ni mkao wa serikali za mitaa ambao utaunganisha viongozi wote, madiwani wote katika hiyo ngazi ambayo itasimamia rasilimali zote na mkuu wao ambaye atakuwa ni mwenyekiti awe ni mwenyeji wa kuchaguliwa kupitia kwa kura.

**Com Ratanya:** Mwarange kama una memoranudm utatupatia baadaye tutasoma lakini tuambie kwa ufupi yale unayo.

**Mr. Mwarange:** Kwa bahati mbaya memorandum yako haikuwa haiko tayari kwa hivyo nilikuwa nagusia vile nilikuwa nikitayarisha maana haijachapishwa bado.

**Com Ratanya:** Okay tuambie yale unayo kwa ufupi masaa iko kombo.

**Mr. Mwarange:** Kwa hivyo katika kiwango cha taifa tutakuwa, nafikiri nitawatumia memorandum baadaye kupitia either kwa posta ama kupitia kwa District Co-ordinator, kupita kwa District Co-ordinator ni sawa zaidi. Kuzingatia tuwe na rais ambaye atakuwa ni mkuu wa dola tuwe na waziri mkuu ambaye atawateuwa mawaziri kutoka nje ya bunge na zilingane na taaluma halifu tuwe na bunge kuuu ambalo litakuwa na masenator na bunge la wakilishi. Pia katika bunge napendekeza kuwa mambo yote yatakayopitishwa katika bunge yawe yanatiwa sahihi sio na mkuu wa dola wala waziri mkuu bali na speaker wa bunge

kuonyesha ya kuwa yamepitishwa na yamekuwa ya sheria kabisa na kipindi cha kuhudumu cha wabunge kiwe cha miaka mitano.

Jeshi liwe linasimamia chini ya wizara mpya ya ulinzi na likuwe chini ya bunge ya waziri mkuu au ya rais tuwe na tume ya uajiri ambayo itachaguliwa na bunge na wajiriwa au wafanyakazi waajiriwe kulingana na elimu. Katika hali ya uchaguzi tuwe na uchaguzi wa wazi na wa siri halafu ilijo na uhuru na haki. Wagombeaji wote wawe wa eneo hilo kuburudika kama kwa mfano wilaya bunge au jimbo na kwa kulinda makabila madogo, madogo tunazingatia kwamba nyadhifa za kisiasa zisiwe zinagombewa na watu wa nje ya jimbo hilo.

**Com Ratanya:** Okay jaribu kumaliza.

**Mr. Mwarange:** Ardhi, lease ziondolewe na hata nikitoa mfano wa Taita Taveta ambapo tunakuta kwamba asilimia kumi na nane nukta sita zinachukuliwa kwa lease ambazo ziko kwa muundo wa kikoloni. Kama Taveta, ziwani, Voi na hata Kidai zipokonywe wale watu wako nazo na zirudishiwe wenyewe, hiyo ni pamoja na sheria za madini zibadilishwe na muundo yote ya kikoloni iondolewe, legal tender katika sarafu yetu ya Kenya tusiwe na kichwa cha Rais ambaye atakuwa. Vile tunaendelea kubadilisha marais au waziri mkuu tusiwe na kichwa chake kwa tender ya pesa yetu bali kuwe na kichwa cha mpiganiaji uhuru ambaye alikuwa kiongozi mashuhuri Dedan Kimathi kwa heshima yake. Nafikiri mengine yatakuwa kwa hiyo memorandum ambayo nimeahidi nitatumana.

**Com Ratanya:** Okay asante sana bwana Mwasai Mwarange. Sasa ni John Mwandime inaonekana hayuko. Julius Teka na wananchi ningetaka kuwakumbusha kwamba mambo mengine tunarudia yale ambayo yamesemwa. Ukija ni heri uwe na mambo mapya ili tujaribu kufanya haraka. Tusiwe tunarudia yale ambayo yamesemwa uwe na mambo mpya kama inavyowezekana.

**Mr. Teka:** Asante mwenyekiti mimi kwa majina ni Julius Teka nimetoka Kishushe. Naongea kuhusu mauaji ya ndovu kwa wanadamu ambaye mtu ameuwawa shambani au machungani na hataweza kulipwa. Tunaomba kwa maoni yangu mtu akiuawa na ndovu au mnyama ye yeyote ana haki ya kulipwa hapo kwa hapo, kwa hivyo maoni yangu ndiyo hayo. Yaliopo mtasoma.

**Com Ratanya:** Asante sana, Julius ameleta mambo mapya kabisa kwa hivyo inatakikana namna hiyo. Usirudie yale yamesemwa yote (clapping). Amekuwa number one kwa hayo. Okay sasa hebu twende kwa Kefa Kabuta.

**Mr. Kabuta:** Kwa majina yangu ni Keffa Kabuta na maoni yangu ni haya. Tume zote zinochaguliwa kisheria katika Jamhuri letu la kenya liwe linatoa usafiri na kama kutakuwa na allowance zozote siziwe zimepangwa kiusawa. Halafu kulingana na kazi mshahara iwe tofauti lakini allowances kwa mfano night out allowances alfaa na travelling allowances ziwe kiusawa. Maoni yangu ni hayo na asanteni.

**Com Ratanya:** Okey asante sana Bwana Keffa inaonekana kweli tunaleta maoni mpya. Kwa hivyo nenda kama mtindo huo huo ili tumalize haraka tusiwe tutakaa hapa mapaka usiku. Na sasa nengetaka kumwita Luka A.C. Mjala. Mlete mambo mpya si kurudia yale ya zamani, zamani.

**Mr. Lucas Leujama:** Asante sana mwenyekiti mimi jina langu ni Lucas Leujama. Basi jambo la kwanza ni kwamba mimi naomba kumchuja.

**Com Ratanya:** Waambie jina lako

**Mr. Luca Leujama:** Jina langu ni Lucas Leujama. Mimi nilikuwa naomba computer ziondolelwe kwa sababu wizi umezidi Kenya sana lakini kwa sababu kazi yote unayofanyiwa inafanywa na ushupavu. Ni computer tano nazinafanya kazi ya watu mia tano au elfu moja. Na ukilinganisha gharama utakuta wale watu wangefanya kazi ya mikono bila shaka zingelingana. Kwa hivyo computer ziondoke ili uwizi upungue.

Jambo la pili, computer sizitaki nataka sisi wenyewe tufanye kazi kwa sababu they are so many in kenya na wamelala tu mbona wanaimba. Kazi iongeweze kwetu lakini sio computer tunanunua . Halafu cha pili ni kwamba sisi tuna mipaka kwanzia mtito hadi taru wataita tahuna sauti ni shamba zetu. Tunataka watu wale waondolewe mipaka inyoshwe vizuri tuchukuwe sehemu zetu ili tuweze kupata mashamba ya kutosha. Jambo la tatu tuna maji hapa mzima spring haya maji baba yetu amenyang'anywa nguo ambaye ni Council.

Tunasikia mwenyekiti wa Council sikitakazwa hana kitu. Kwa sababu gani mwenyekiti wa Council haokoti chochote maji yanatoka mzima kwa pipe kubwa yanaelekea Mombasa mimi niende tena Mombasa na nilipie maji. Lakini hayo maji imetoka kwa Council yangu. Council yangu haikoti chochote inatoka tupu. Kwa hivyo hakika maji yetu Council ipewe sehemu fulani ili nayo ipande kwa sababu maji yametoka kwake.

Pia kuna jambo lingine hapa sisi hatuna shule. Shule zetu mara tunadanganywa shule ni bure mare ni pesa hatuelewi maanake ni nini. Haya tukienda sasa tunakuta inapouliza sana unaambiwa wewe mbaya hicho kitu kiondolewe. Walimu nao kwa mfano walimu wa nursery mishahara yao ni midogo sana na vile wanafanya kazi kubwa kuondoa watoto mavi. Unamkuta analipwa shilingi mia nane ama elfu moja niambie huu mshahara kweli. Makosa, inafaa wale walimu wa nursery walipwe vizuri kwa sababu wenyewe kutafuta watu wasome. Hivyo mnavyo andika mwalimu wa nursery kama si nursery usingeandika hapo mezani.

Jambo la mwisho kumetokea kitu cha uhuni, uhuni imetuzidi. Wizi kidogo, bangi, chang'aa, pombe. Mimi maoni yangu naona afadhali pombe ya muratina urudishwe na iwe kilabu maallum. Kwa sababu zile nyumba ndogo ndogo zinazouza pombe ndipo vijana wanaunda njia ya kuunda bangi, ndipo itapata njia ya chang'aa askari naye anapata kupewa kitu kidogo kila siku askari

mbaya. Kumbe ni tabu na pombeni the main agenda ni kutoa kitu kidogo haya wacha sinichukuwe. Mwenye kilabu hakuna kitu kama hiyo atapoteza.

Ningependekeza kilabu kiweke kisimamia na Council, kisiwe ni mimi ninacho nyumbani eti niuze. Council isimamie kama zamani maanake sisi tulikuwa tunapata nice Council tangu walikuwa wanalipia hizo pesa kwa Council. Tangu waguze hizo pesa sisi hatuna kitu na Council imekuwa ni Council tu hata magari haina sasa, hata la kubeba takataka haina kwa sababu imenyang' anywa kila kitu na serikali. Sasa Council imebaki ni Council jina tu, imevuliwa nguo.

**Com Ratanya:** Naona kwamba umemaliza bwana Leujama.

**Mr. Leujama:** La mwisho ni kwamba

**Com Ratanya:** Mwisheso

**Mr. Leujama:** La mwisheso kuna wanawake wengi na wasichana waliozaliwa nje ambao hawana nini. Wanawake walioelewa nje, walikuwa ambao hawana ndoa wananyimwa kitambulisho mpaka bwana atoe pesa. Ndipo jina liwekwe la bwana na wakati nikifa mimi amo ukifa yule mwanamke hasumbuliwi na ndugu zake kwamba hana kitambulisho cha bwana. Kwa hivyo majina ya mabibi yaandikwe mabwana, na wasichana wameozaliwa nje wao bila wanaume wangaliwe mtu alimpatia mimba achukuliwe hata kali ili yule mtu amwoe ama amulipe. Si mwalimu mtoto wa mtu kutoka shulenii halafu acae hivyo. Yangu ni hayo asante.

**Com Ratanya:** Okay tunashukuru sana Lucas. Na sasa tunaenda kwa David Nyambu.

**Mr. David Nyambu:** Kwa mabwana commissioner na wananchi hamjambo. Mimi bwana commissioner ingawake ninayosema sigusii kidogo wacha nigosie maanake sikupanga mengine nimeona yamefanana wacha niende speed.

**Com Ratanya:** Okay bwana David naona kwamba una memorandum, kwa hivyo itasema kwa ufupo kabisa na utupatie hiyo memorandum tutasoma.

**Mr. Nyambu:** Okay bwana Commissioner, mimi naonja onja kidogo kulingana na vile nimeandika. Jambo la kwanza ni kutetea hii national park hii ya Taita Taveta. Hii national park ni kubwa zaidi na inaonyesha ni kubwa zaidi na wananchi hapa hawana mashamba kabisa. Kwa hivyo tunaonelea igawanywe  $\frac{3}{4}$  ibaki  $\frac{1}{4}$ , na hii  $\frac{1}{4}$  iitwe Taita Taveta Game Reserve hii ingine imebaki igawanywe wananchi watumiwe kwa kulima mashamba. La pili ni hii hali ya maji, Taita na maji mengi sana hasa kama kuwa spring. Maspring iko na maji mengi sana inaenda Mombasa, Voi lakini Wataita hawatumii hata hapo chini wanakufa na maji. Unaona mtu moja anaanza kumaliza mwezi, wiki mbili bila kujiosha hapo hapo karibu na mfereji unapitia hapo karibu.

Tunataka hawa wajamaa watumie haya maji kwa kunywa. Wapewe maji kwa kunywa, wakipewa maji kwa kunywa na wale wanotumia Mombasa au Voi walipe County Council ya Taita Taveta kulingana na madini. Tuingie madini yalioko hapa pesa zinazoingia katika Kenya tunataka ziingie katika Taita Taveta ambapo ni County Council ya Taita Taveta mzazi. Tulipe hapo si kulipiwa na Nairobi yaani kuwa office kuu. Hili lingine nasema naingia mambo ya kuendeleza mambo ya serikali.

Serikali tunayotaka sasa tunataka serikali ya majimbo. Serikali ya majimbo ambayo itakuwa na mkoa bora ambaye tunaweza kumwita ni rais na waziri mkuu wa majimbo na wa mabaraza na wanavijiji. Wote hawa watakuwa wakichaguliwa na wananchi, na wawe miaka yao iwe thelathini hadi sitini. Na kipindi chao chote cha kihudumu hao wote wanaochaguliwa kuwe miaka mitano, mitano.

Tuingie mpango wa hospitali, hospitali tunataka ziwe bure. Hizi cost-sharing ziondolewe maana watu wanakufa njiani wengine wanakufa kukosa pesa. Madaktari nao tunapendekeza walipwe pesa nyingi. Wasije wakatoroka nje maana wengine wako nje na hawawezi kuhudumi katika hizi hospitalai zetu za hapa nyumbani. Kwa upande ya elimu tunataka elimu kutokea msingi hadi ya upili iwe bure. Na vifaa vyote vya watoto vilipwe na serikali. Huu mfumo wa elimu kuanzia nursery ama standard one iwe ule wa zamani, 7-4-2-2 mpaka university.

Kulingana na kimila wananchi huwa hiona wanajilazimisha ama kuna mila zingine vile unaona mvua inanyesha sasa. Zilikuwa zinafanya na wazee kutoka zamani. Walikuwa wanajiona, wanafundisha ama matandiko fulani. Haya matandiko wanayfanya na pombe zao za kienyeji. Tumeona siku hizi pombe za kienyeji hazipo zile ziko ni za kigeni. Hizo za kigeni hazifanye matekezo kama hayo. Tunaomba hii sasa ingizwe katiba. Mkenya ye yeyote nataka awe chini ya sheria na mkuu wa sheria tunataka na mahakama achaguliwe na wananchi.

**Com Ratanya:** Okay David jaribu kumaliza.

**Mr. Nyambu:** Wacha nikatie shortcut.

**Com Ratanya:** Usirudie yale umesema

**Mr. Nyambu:** Nimegusia mara ulipanga

**Com Ratanya:** Sasa jaribu kumaliza

**Mr. Nyambu:** Sasa namaliza bwana Commissioner. Uchaguzi tunataka uwe wa siri na uwe wa haki. Na tunataka ikiwezekana kutoka area ya udiwani, area ya ubunge watu wachaguliwe wa area ile ile. Ikiwezekana kulinda uporaji na kulinda ufisadi. Yangu ni hayo bwana Commissioner. Nashukuru sana.

**Com Ratanya:** Okay asante sana bwana David Nyambu. Jiandikishe hapo. Tuna Mercy Mushila, inaonekana kwamba hayuko. Samuel Isupirio, Samuel yuko karibu? Okay na tena ningetaka kuwakumbusha wananchi mjaribu kufanya mapendekezo yenu mafupi. Yawe mafupi. Usirudie yale yote tumeambiwa kutoka asubuhi. Tumeambiwa mengi kwa hivyo usirudie tuambie mambo mpya. Ulipeana memorandum unatosheka. Okay asante sana. okay that give a memorandum and he is satisfied. That is Samuel. Now Eda MuchiGame yuko, that one hayuko, this is Albert Mugange. Mugange usirudie na kama uko na memorandum utatuachia lakini sema mafupi tu. Hebert Mugange. Mimi kwa jina ni Hebert Mugange. Kwa hivyo yale ambayo unaongeza nimekupatia dakika moja uongeze mapya.

**Mr.Hebert Mugange:** Nitagusia tu yale ambayo nasikia wenzangu hawajagusia. Na nitaanze na hili la kwanza kulingana na umuhimu katiba inapendekeza uchaguzi wa mwaka elfu mbili na mbili usifanyike kabla katiba haijarekebishwa. Hili la pili ninapendekeza kulingana na haki ya mwananchi katiba ijayo igusie kipengele fulani ambacho kitakachoeleza ya kwamba mgonjwa ye yote anayeugua ugonjwa wa ukimwi ama ye yote yule katika nchi ya Kenya itolewe amri wapimwe na ye yote atakayepatikana na virusi basi jina lake litangazwe ki wazi wazi Kenya nzima.

Nchini Kenya uhuru wa kuabudu imekukwa yaani kuwa abused. Katiba inapasa kuweka mashariti katika kusajili madhehebu kwa sababu baadhi ya viongozi wa madhehebu fulani wanautumia nguvu ilivyowekwa ya kuabudu kwa manufaa yao wenyewe. Watu wasitumie jina la mungu au maandiko matakatifu katika kujinufaisha au katika biashara. Kuhusu wagombea viti. Katiba isiruhusu mtu mgombeaji ye yote kiti awe ni mbunge au madiwani kuahonga wananchi wakati wa campaign. Iwe ni hatia kwa mgombea kiti ye yote kuanunua wananchi wampigie kura.

Kwa sababu hali hii inafanya mwananchi kuwa kama mtumwa na sio mwajiri na hali kama hii Kenya, haki ya mnyonge ni mwenye nguvu apende. Majukumu ya viongozi katika ngazi mbalimbali yaelezwe katika katiba hii ambayo tunairekebisha na zaidi zaidi wabunge na madiwani ili kusiendelee kuwa na kupewanwa ahadi nyingi na hao wagombea viti hata kusieleweke iwapo ahadi hizo ni za kweli au ni zaudanganyifu ndani yake.

**Com Ratanya:** Inaonekana hiyo tutasoma. Fupisha hayo atutayasoma hata ukitaka tena.

**Mr. Mugange:** Yamebaki machache. Lingine ambalo nitakalo ligusia nu kuhusu vitambulisho. Inaonekana kunatokea malalmishi katika vitambulisho ambavyo vimetolewa vipya, picha zilizoko katika vitambulisho hivyo havilingani, ama hazilingani na sura za wenyewe. Hivyo basi tunapendekeza ikiwezekana vitambulisho vyatapo awali virudishwe kwa sababu vienyewe vilikuwa na picha rasmi za wenyewe. Ingine ni kwamba ardhi imilikiwe na wananchi wazalendo. La mwisho kuwe na serekali za majimbo. Lakini majimbo haya yagawanywe kimkoa ili kusije kukawa na ukabila. Yangu ndio hayo. Asanteni.

**Com Ratanya:** Okay asante sana hapa. Twende kwa mwininge anaitwa Sebastian Sogona, Sebastian hayuko? Okay twende

kwa mwingine naitwa Syreton Mwamburi ndie anaingia. Kwa hivyo Mwamburi twambie kwa ufupi yale mapya ili tusipoteze wakati mwingi.

**Mr. Syreton Mwamburi:** Asante sana chairman . Mimi ni Syreton Mwamburi na ninatoka hapa hapa werugha. Yangu ni machache maanake mengi yamezungumzwa na wenzangu. Mimi langu ni kuomba hii tume ambaye tunaipigania sasa iangalie masilahi ya wazee na vikongwe. Maanake mengi yamezungumzwa kwa vijana, watoto na akina mama lakini inaonekana ya kwamba temesahau hao wazee. Maanake mtu akisha kuwa mzee kwa hakika hawezi kufanya kazi hata kama anapenda huwa hawezi. Kwa hivyo napendekeza kwamba iweko ufungo maalum ya kuangalia hao wazee na hao vikongwe ni nino hao viwete. Maanake ni watu wanaishi na wana mahitaji yote lakini hawajiwezi kwa kujipatia mapato ilo ni la kwanza.

La pili hapa sasa kuna hao watu tunaingilia kwa hii retirement benefits. Hii retirement benefits kwa hakika naona pengine huu mtindo uliopo tuseme pengine imepitwa na wakati. Kwa sababu unaona pengine mtu ali-retire pengine mwaka wa sitini ama hamsini inaona bado mpaka sasa mungu amemweka maisha anishi na ukiangalia maisha yake yamekuwa duni sana kwa sababu unaweza kumuona ile retirement benefit haipandi. Zile job groups zinasopandishwa kila wakati huyu mtu ambaye ange-retire zamani anabaki hapo hapo. Na ni ajabu na ni kweli kwamba kuna watu mpaka sasa unaweza kuona wanapata shilingi mia mbili ati ni retirement benefit. Hiyo naomba hii katiba ya sasa iangalie jambo hilo na irekebishe ikiwezekana tafadhali. Maanake hilo watu wanapewa maisha lakini ukimwangalia mtu hana la kuishi maanake pesa kidogo sana. Yangu na fikiria yalikuwa ni hayo machache mengi yamezungumwa. Asanteni sana kwa kunisikiliza.

**Com Ratanya:** Okay asante sana Mwamburi. Twende kwa Chris Nyange.

**Mr. Chris Nyange:** Asante Bwana mwenyekiti. Majina yangu kamili naitwa Chris Nyange na ninaenda kwa mchango kwa sababu nina memorandum nitafupisha fupisha. Katika katiba hii ambayo tunataka iangaliwe ningependekeza katiba yetu sisi wa kenya si chombo kuvunja dola yaani inachukuliwa kihivi kwa maana ya uzito. Na muundo wa dola, kuwe na executive ambapo ni ya kutekeleza. Kuwa na bunge, bunge ziwe mbili,bunge ya kwanza iwe ni bunge waakilishi na bunge tekelezi. Bunge waakilishi iwe ni bunge ya kuchaguliwa na wananchi na katika mbunge wanaochaguliwa na wananchi wasiteuliwe kuwa mawaziri.

Katika zile bunge zingine ambazo nimelitaja kama bunge tekelezi hapo ndio mawaziri watoke ambapo atachaguliwa na bunge baada ya kupitia katika huo ukaguzi ndio wawe appointed. Hao watakua mawaziri. Ma-professionals ambapo watakuwa wanahudumu kwa, watapangiwa mawizara kulingana na taaluma walizonazo. Halafu katika bunge tekelezi liwe linakagua na-officer wote wakuu wa serekali. Wasiwe appointed bila kukaguliwa. Wakaguliwe baada ya mapendekezo wakaguliwe waonekane kwamba wanafaa kinidhamu na kwa hali zote na qualifications halafu ndio sasa wawe appointed au wanawenza kuwe Permanent Secretaries na wengine ma-officer wakuu.

Mahakama yaweko, yawe huru na yasiwe yakuweza kuiwigiliwa. Katika mikono hii ambayo nimesema ya kwamba katika dola.

Ya Ku-form dola mikono hii mitatu yatumike bila migongano wa kuinigiana kushuhuri. Bunge ifanye kazi yake kama bunge hata sana, bunge tutakayo kuwa tunaitegemea sana ni bunge waakilishi. Halafu mahakama yafanye kazi zake bila pia wawe na muda wa kuhudumu amba ni taratiabu. Na katika mahakama wawe wanafanya kazi yao huru na muda waliopewa na pia wawe wakiwa vetted.

Local authority, kuhusiana na hali iliyoko mabaraza ya wilaya na miji yameshindwa na kutekeleza majukumu mbali mbali na muhimu ijapokuwa hao ndio walioko karibu na wananchi kwa sababu hayo mamulaka waliokuwa nayo kuitia mwaka wa nineteen sabwini (1970) yalinyakuliwa yakapelekwa kwa central governement. Hiyo basi wakanyang'anyw'a mapato na kazi zao muhimu zikawa zimeenda wa kiambiwa ya kuwa pesa zitakuwa zikitoka huko zikija lakini pesa hizo zimeendelea haziji. Hivyo basi tunaomba mamlaka yapanuliwe.

**Com Ratanya:** Jaribu kumaliza, try to sum up.

**Mr. Nyange:** Okay sasa kulipa madiwani. Walipwe kutoka kwa mfuko wa mamlaka. Hiyo ni moja, uchaguzi wa ma-mayor na wenye viti kwa sababu ya upango wa gherama vile ninavyopendekeza kwamba wachaguliwe yaani wafanye campaign kana ni district nzima inakuwa kama hilo si jambo la sio kama linawezekana. Ninaona kwamba kama kitakuwa na uwajibikaji na uhaki na kutokuchukua hongo au kuhongana midiwani wanaweza kuendelea kuchaguwana kwa sababu ya kuzuia vyama vingi. Huduma muhimu ambazo zinahitaji ziwe zinalipwa na pesa za kodi ni ya kwanza iwe ni elimu, madawa ya hospitali na yaani elimu iwe ya bure kutokea nursery hadi ukiwezekana chuo chingine kikuu.

Madawa katika hospitali ya uma yawe bure na pia hazina kama nini inakuwa, watu wanakuwa retrenched na baada ya retrenchment inakuwa ni vigumu watu kupatiwa pesa zao za NSSF ati mpaka apite umri wa miaka hamsini na inakua ngumu tu hawezi kuachiliwa. Kipengele hicho ningeeomba kiondolewe. Mtu anapokuwa retrenched aweze kulipa pesa zake ili aweze kuijendeleza. Mila, mila zetu sa wataita ni kama vile hazina tofauti kama na mambo yaliyvo katika bibilia. Hivyo basi ni ombi langu mila hizi zidumishwe ambapo tunaweza kuondoa mambo kama vile ilivokuwa wasichana wetu walikuwa hawawezi kupata mimba kabla hawajaolewa. Lakini mila hizo kufunziwa ziwe open.

Okay recommendation ni kwamba zihifadhiwe na yaani zikubalike na katiba kwamba maanake tu taratibu sisi wenyewe. Kuchukuliwa bila idhini na bila malipo aama compensation. Mashamba yetu makubwa makubwa kama hii yaliyochukuliwa yanayomilikiwa yanapanda makonge ambaye ni ziwani, mwatate hapa na poi. Yenyewe hawasitahili kuwa na title deed badala yake wangekodisha na wawe wanalipa County Council ama kulipa mwananchi kupita kwa County Council. Na ifadhi za wanyama pia ardhi hiyo tunataka irudi. Ni haki yetu yote 100% halafu kama kutakuwa kwa sababu serekali huwa inajiri watu tukuwe na percentage ambapo tutakubaliana.

**Com Ratanya:** Okay jaribu kumaliza national park tumesikia mara nydingi .

**Mr. Nyange:** Naam

**Com Ratanya:** Kwa hivyo jatibu tu kufanya ufupi

**Mr. Nyange:** Madini pia yaregeshwe

**Com Ratanya:** Hata madini tumesikia. Memorandum si tunaweza kuiweka na tusome baadaye.

**Mr. Nyange:** Okay hiyo tunaweza kuiweka. Sasa nipatie nafasi ya moja. Kuhusu umaskini nchini Kenya nafikiri njia ambazo kuweza kuwangalia ya kuondoa kupigana na umaskini ni kwamba kila mtu yaani tuajibike tufanye kazi kwa bidii na tuajibike sana. Ya pili mtu moja afanye kazi moja. Tatu wafanye biashara wa wholesale wasipatiwe nafasi ya kuendesha biashara za reja reja. Ya nne, kuwe na control kwa bei ya vitu vya kawaida, maanake kulingana na haki zetu na tofauti za matajiri na maskini tunakuwa ni vigumu kushindania masoko ya vitu. Hivyo basi ningependekeza kwamba kuwe na control irudi kwa bei vyetu vyakula.

**Com Ratanya:** Bwana Nyange jaribu kumaliza kuna wengine wanangoja.

**Mr. Nyange:** Okay

**Com Ratanya:** Tupatie memorandum yako

**Mr. Nyange:** Na kuhusu mipaka pia ningependa yaadhibitiwe na yaheshimiwe.

**Com Ratanya:** Okay mipaka yes. Namwita Ibrahim Mwaruta, huyo Ibrahim hayuko. Samason Mwawasi. Na ninetaka kuakumbusha ya kwamba kama una mambo mapya tutapitia hayo usiwe ukirudia. Sababu tumesikia mengi na kunaendelea kuwa usiku.

**Mr. Samson Mwawasi:** Kwa majina Samson Mwawasi. Maoni yangu ni kuhusu biashara yetu ndogo ndogo. Kuhusu biashara ndogo watu wengi ambao wanafanya biashara zile ndogo ndogo wanapata shida kwa vibanda vyao kubomolewa huko ndio njia ya kujitafutia familia zao ili zipate kushiba. Kwa hivyo kwa mapendekezo yangu naona vibanda hivyo visibomolewe. Vibanda hivo visibomolewe, County Council isibomowe na County Council.

**Com Ratanya:** Tangu nini ibomolewe?

**Mr.Mwawasi:** Zibomolewe sababu familia nyingi zinategemea hizo vibanda.

**Com Ratanya:** Unasema viondolewe viwanda?

**Mr. Mwawasi:** Visiondolewe

**Com Ratanya:** Visiondelewe, Okay

**Mr. Mwawasi:** Nani ni hayo tu. Asante sana.

**Com Ratanya:** Okay asante sana. Kama ukiwa na jambo hata moja ambalo halikusemwa ukisema hapa itakuwa ni mzuri sana. Kwa hivyo usiwe unarudia rudia. Kama huyu amefanya mzuri. Twende kwa mwingine hapa anaitwa Ebrahim Mwanagachi. Inaonekana hayuko. Na tena tuna Dorothy Mwapili vile vile hayuko, Joyce Mwaruma, Mushila Mwangeka. Okay bwana Mushila tuambie yale mapya mapya na usipoteze wakati kwa yale tumesikia mara nyingi.

**Mr. Mshila Mwangeka:** Asante sana bwana mwenyekiti. Majina yangu ni Mushila Mwangeka. Langu la kwanza ni kuhusu mahakama ama uamuzi wa mahakama ni kwamba ningependekeza mahakama yawekwa uhuru halafu linalofuata polisi ipunguziwe nguvu za kudhuru wananchi pasipo haki ila iwe tayari kusaidia wananchi mahali kokote wakati wowote waitajiapo msaada.

Linalofuata ni kwamba biashara ndogo ndogo zitunzwe na serikali na wachunge kuwakata kodi ya hali ya juu that is overtaxation. Ama ikiwezekana hata kabisa kiosks wasikatwe chochote wasiombe kodi. Biashara zao ziendeleshwe bila kuitishiwa kodi na kodi zitishwe wale watu wako na biashara kubwa kubwa kama supermarkets na kadhalika. Halafu kuna ukeukaji wa haki za wafanyakazi, mishahara midogo, ningeomba katiba mpya itazame kwamba kitu cha kwanza waongeze wafanyi kazi wote mishahara kwa maana wanaishi hivyo duni kwa ajili ya hiyo kitu. Halafu linalofuata ni kwamba wanyonge ambao hawana haki ya kimapeni ama kifedha wanadhuluiwa. Kwa hivyo ni jambo liangiliwe tusije tukadhuluiwa saana ati kwa sababu hatuna pesa na wale wako na haki za pesa wanaenda kotini na wale ambao hawana wanabaki huku wakidhuluiwa kwa maana hawana hata pesa za kushitaki huko kotini. Na ingewezekekana huko kotini serikali ikurudishiwe washitakiwa fidia iwalipe wanapo kutwa kwamba hawana hatia kwa maana ni nyingi sana wanapoteza pesa za na kadhalika.

Tukiendelea hapo kidogo ningeomba kwamba wale wote ambao hawana ardhi na wako nchini ya Kenya serikali ihakikishe ya kwamba kila mwananchi wake anapata sehemu ya ardhi. Tukiongeza kidogo hapo mtapata kwamba uhuru wa kutoa maoni pia uwewewe kwenye kipengele hiki cha katiba mpya kila mtu aweze kuzungumza yale ambayo anayo njia ya uhuru bila kudhuluiwa vibaya na serikali. Halafu pamoja na hivyo tuna mawasiliano mabaya kama barabara hatuna ningeomba serikali iweze katika kipengele kipyga cha katiba iweze kugawanya haki za kimapeni ama pesa kwa kila division ili sote tuwe na haki

sawa kwa maana huwa tunalipa kodi nchini hii.

Halafu ningeomba bunge la katiba mpya iwe ikisomwa moja kwa moja kwa mwananchi badaala ya kusomewa baada ya mambo mengine kuondolewa baadaye. Iwe ikisomwa moja kwa moja tukipata habari iliyotunafuatilisha huko bungeni. Halafu kuendelea hapo

**Com Ratanya:** Karibu ya mwisho sasa

**Mr. Mwangeka:** Mwisho nitaomba kwamba watoto waangaliwe na wasiweze kuajiriwa hiyo iweko ikuwe ni hatia kuajiri mtoto ambaye hajafika miaka kumi na nane. Halafu kwa upande wa kupiga kura ningeomba zipigiwe kisiri. Watoto wakizururazurura mitaani pia watunzwe na serikali naitafute njia ya kuondoa tatizo hilo halafu vyama vya wafanyakazi. Vipewe uhuru wa kutetewa na wafanyakazi wao bila vitisho vyovyote. Tukiendelea ningeomba kwamba universities ziweze kuwekwa kwa kila jambo.

**Com Ratanya:** Hebu jaribu ya mwisho kabisa.

**Mr.Mwangeka:** Ya mwisho kabisa.

**Com Ratanya:** Kwa sababu tuna memorandum yako tuambie ya mwisho sasa.

**Mr.Mwangeka:** Asante sawa basi nitatoa la mwisho kwa kusema kwamba mazingira pia yatunzwe katika kipengele hicho cha katiba mpya. Ukiwezekana kila mwananchi alazimishwe kupanda mti kwenye shamba lake.

**Com Ratanya:** Nashukuru bwana Mushila kwa hivyo twende kwa Jefferson Mchalongo. Na hapo kwa sababu naona Mchalongo ana memorandum tuambie machache halafu utupatitie memorandum yako. Dakika moja na nusu hivi. Kidogo tu kwa sababu kunaendelea kuwa usiku.

**Mr. Jefferson Mchalango:** Asante bwana mwenyekiti katika katiba mpya ningetaka wale ambao hawana mashamba kwa sasa na kuna hizo Game Reserve sehemu nyingine igawanywe hao watu na zigawanywe kulingana na vipimo kwa mfano kila mtu asiwe na zaidi ya acre ishirini.

Kuhusu wasichana wale ambao wanapata mimba nje ningependekeza kwamba mwanaume anayehusika na mimba hiyo aweze kupoteza nusu ya sehemu ya shamba lake ambaye atagawanywa na baba yake ama alilonunua kwa huyo msichana ambaye ana mimba ya huyo bwana. Mtu yejote ambaye anataka kuuza shamba katika hii katiba mpya ningependekeza kwamba ikiwa anauza awe na sababu nzuri na sababu hizo zижilikane kwa familia yake na kwa watu wa ukoo wake. Na watu hawa wawe zaidi

ya watu ishirini. Kuhusiana na mambo ya koti napendekeza kwamba kila taarafu iwe na koti ambayo inaongozwa na magistrate.

**Com Ratanya:** Okay inaonekana kwamba amemaliza. Tupatie memorandum sasa. Okay nashukuru sana na sasa ningetaka kujua ni wangapi ambao tunao hapa ili tuweze kujua tunaendelea namna gani. Francis Mwacholi, yuko? Francis Mwacholi kama yuko inua mkono ili tujue kama yuko hapa okay. Ayo Ondimo, Willy Mwakulomba, Obura Zange, Stanley Kindonyi, hata Stanley yuko, Patrick Shuma, Amos Mutigo, keti tukakwita tena, Elizabeth Chao, Elizabeth yuko, Emmanuel Mwambula, Emmanuel hayuko, Gilbert Mwamburi, yah this one I have read him. Zaphati Maigacho, yuko, Benson Mwakachola, Benson yuko, Peternice Musiko okay, nitamwita mmoja mmoja na mjaribu kufupisha na sasa nawapatie dakika mbili na ukiwa na memorandum nitakupatia dakika moja ili tuondoke hapa twende tukajenge nchi njia ingine.

**Ms. Hogla Zangi:** Jina langu mimi ni Hogla Zangi. Maoni yangu ni yale yamesemwa lakini nitataja yale ambayo hayajasemwa. okay ya kwanza kuzoroteka kwa uchumi wa Kenya. Ningeonelea kama Kenya imepata pesa iwe ikitoa fungu la kumi kwa mwenyezi Mungu ili pesa ibarikiwe kuondoa ndio ziende ziae. Lingine ni kuangaliwa wale ambao hawajiwezi vilema. Na watoto yatima kutolewa elimu bure. Na la pili watoto wale wanazaliwa nje ya ndoa akiwa hata kama amezaliwa ni vizuri lakini awe yule ambaye amemzaa wazazi wawili watumilikiwa na wale mume na mama. Au kama kuna lingine tofauti yaani Kitaita tunasema (translator). Hii maana (translator) ni kulindwa ng'ombe ndume na ng'ombe jike na kywa msichana ambaye aliye shule na kijana wako shule wamewekana mimba. Yule msichana anarudi nyumbani na mvulana anaendelea na shule ningeonelea wote wawe nyumbani. Msichana akiwa anangojea mtoto mvulana awe akifanya kibarua ya kuja kulea ule mtoto au kumuelimisha. Na kuwa na viboko vikali kwa wanaonajisi wanaofanya kazi ya unajisi au wanaotumiwa nguvu kwa kufanya mapenzi. Kuwe na kifunzo kutoka miaka saba na kuendelea na viboko vikali.

**Com Ratanya:** Kwa hivyo ni kama amemaliza wazo hili.

**Ms. Hogla Zangi:** Kuna lingine katika hospitali ambazo halikuguzwa.

**Com Ratanya:** Sema ya mwisho.

**Ms. Zangi:** Katika mahospitali zetu kuwe na kamati ambayo inaweza kuwangalia shida za wagonjwa na hata za wafanyakazi. Na hii kamati inawezwa na ikiongozwa na district kuna sababu hii. Ni vizuri kuwa na kila hospitali ya district iwe na daktari hilo liisemwa. Na ninaguza lingine katika koti au kule, koti zetu. Koti zetu tunaona ziko katika kwa umbali sana hazifikii wananchi kwa mfano hapa tukiwa hapa Wundanyi tunaenda Voi tunataka kila mahali au districts iwe na magistrates hapo ili kusafiri kuwe rahisi. Na ndipo wakati mwingine uhalifu unazidi kwa sababu tunashindwa kuenda Voi. Na kwa mitengo au common land limesemwa lakini sikusikia kwamba hii mitengo usipewe mtu binafsi upewe wananchi wote. Asanteni.

**Com Ratanya:** Okay nashukuru sana madam kwa hayo maoni yao mazuri kabisa. Twende sasa kwa Amos Mtigo. Amos

usirudie kwa sababu una dakika moja.

**Mr. Amos Mtigo:** Mimi naitwa Amos Mtigo. Mengi yamezungumzwa siwezi nikarudia. Langu ni moja. Naona sisi Wataita tumeachwa nyuma kimila. Kwa mfano Wamasai wantumia mikuki.

**Com Ratanya:** Tuambiwe mapendekezo mnataka kutumia mishale ama la. Toa mapendekezo yako.

**Mr. Mtigo:** Hata sisi tunataka tuwe na uhuru wa kutumia uta kwa kujikinga. Kwa mfano yaani kama tuko tumeijiwa na wakora siwezi tembea bila silaha. Mshale kama silaha au baadala ya kutegemea watu kama vile anategemea kutumia kama mawe. Sasa hilo ndiko pendekezo langu kwa vile mengi yamesemwa.

**Com Ratanya:** Kwa hivyo tumeshukuru sana umetuletea pendekezo nzuri kabisa. Tuende kwa Elizabeth Chao. Nawe Elizabeth tupatitie mapendekezo yako kwa dakika moja na nusu.

**Ms. Elizabeth Chao:** Kwa majina naitwa Elizabeth Chao. Kwa mapendekezo yangu ningependa wanawake walitishe haki zao kama wanaume. Shule zetu za zamani zirudishwe za standard seven. Pia kama mwanamke ameolewa na bwana, bibi na bwana kama wamenunua plot kwa mfano wawe wametoa pamoja na yote bwana waandikishe kuhusu majina yao yote wawili . Bibi na bwana kwa maoni yangu watoto wajane pia wasome bure. Yangu ni hayo.

**Com Ratanya:** Okay asante sana Elizabeth maoni ni mazuri kabisa. Twende kwa Gilbert M. Mwamburi.

**Mr. Gilbert Mwamburi:** Jina langu ni Gilbert Mwamburi natoka Mrungi, Werugha location. Maoni yangu ni kwamba masilahi ya Mkenya yatekelezwe kwanza kabla ya mgeni. Pendekezo la pili sheria itekelezwe sawa kwa mgeni na kwa mwenyeji kwa mfano kukiwa msako kama vile town mwaafrika anaposimamishwa na mhindi, mwarabu, au mzungu asimamishwe. Maoni ya tatu sheria itumike sawa kwa maskini na kwa tajiri. Maoni ya nne Mkenya awe tajiri au masikini awekwe kiwango maalum cha ardhi.

**Com Ratanya:** Asante sana Gilbert na mwingine ni Sephat Mwangacho. Hata wewe Mwangacho ufuate huu mtindo. Utuambie mapendekezo tu yale ya muhimu.

**Mr. Sephat Mwangacho:** Mimi kwa majina yangu naitwa Sephat Mwangacho na kwa jumla yale mengi yangu na yale machache niliyonayo ni yale yamezungumzwa lakini kwa uchache naomba niruhusiwe kusema kidogo.

Maoni yangu ya kwanza ni kwamba kuwe na serikali ya majimbo. Ya pili sheria kuhusu madini ichunguzwe na ya tatu ambayo ni ya mwisho ni sheria idumu ya mbinu za upangaji ya uzazi ambazo ni za kisasa ziondolewe na badala yake kutumia mbinu za kizamani.

**Com Ratanya:** Okay ni hayo tu ama? Asante sana bwana Mwangacho. Na tutaenda sasa kwa Benson Mwakacha

**Interjection:** Mwakochola

**Mr. Mwakochola:** Mimi nitaomba mnipatie muda kidogo vile nimetumwa na wenzangu na hawatafurahishia nikipeleka hivi.

**Com Ratanya:** Okay nitakupatia mingi zaidi kwa hivyo ni dakika mbili

**Mr. Mwakochola:** Aha saa hiyo itamaliza hii karatasi mingi. Hio mapendekezo ya katiba imetoka kwa vijana wa Marumange. Na wanataka katiba ya Kenya iwe ni ya Wakenya halisi na wajifiche kwa katiba na sheria walioweka. Mkataba huu wa katiba ukuwe ni wa jamii ya Wakenya. Wahusika wakuu wawe wananchi wa Kenya na mkataba huu ulenge kufanya wananchi Wakenya kuwa na sauti katika nchi yao. Kwa upande wa rasilmali, rasilimali zilizoko kama ardhi.

**Com Ratanya:** Kwa hivyo Benson wewe una dakika mbili. Kwa hivyo jaribu kumaliza kusoma kwa hiyo dakika mbili.

**Mr. Mwakochola:** Na hizi karatasi zitakwisha kwa hiyo dakika mbili kweli. Rasilmali hizo ambazo zimetolewa na Mungu ili watu wazitumie kuhoresha maisha yao tunaweza kuzilinda, tuhifadhi bila msaada kutoka nje. Rasilimali hizi zinatoka Kenya na ni za wakenya na ziko kwa manufaa ya Kenya. Zikisikiwa kuhifadhiwa na wenyewe kama mbuga ya Tsavo iwe Game Reserve baadala ya national park ili ifaidi wenyiji Mtaita.

Mashamba yaliyonyang'anywa mababu zetu na masettler wazungu kwa mfano Taveta, Mwatate, Voi na Kidhai yarudishiwe wenyiji na lease ziondolewe. Sheria za umilikaji na uasidi wa madini zigeuzwe ili wenyiji wao waweze kufaidi na serikali yao wilayani iwe na wakati wa kuendesha ili kuwapa wakazi huduma ya mjini. Sheria za lenga nazo zigeuzwe ili wajiriria waanze kulipa kwa haki kwa maana dhamana kamili ya jasho lao. Mishahara ya wafanyakazi upandishiwe.

Wafanyakazi walioajiriwa wasikubaliwe kuendesha biashara ili uwape nafasi wasiwe na kazi. Wakenya wanalenga wawe na Kenya ya kujitegemea kiuchumi na yenyе kufuata sheria. Kenya inayosimamiwa kulingana na kanuni zilizotungwa na wananchi wenyewe na katiba yetu. Mtindo wa serikali tunataka tuwe na majimbo na dola ya Kenya iwe na ya sauti tatu tu. Ya bunge, serikali halafu na ya mahakama ambapo hakina iliyo juu ya katiba na sheria ya Kenya. Halafu loyalty pledge iondolewe.

Kiongozi wa taifa awe ni rais ambaye atagombea urais peke yake si pamoja na ubunge na achaguliwe pamoja na wananchi cheo na mali ya mtu aliyonayo. Ahakikishe miradi yote inayopitishwa bungeni yatekelezwe na kutembelea kila mahali nchini.

**Com Ratanya:** Naam, yale yamebaki tutayasoma.

**Mr. Mwakochola:** Na hao wengine niwaambie nini?

**Com Ratanya:** Naona unarudia yale yamesomwa, lakini mimi nitasoma. Tume itasoma hiyo vizuri sana.

**Mr. Mwakochola:** Itakuwa ngumu.

**Com Ratanya:** No tutasoma, haitakuwa ngumu tena nyngi.

**Mr. Mwakochola:** Lakini nasoma hili

**Com Ratanya:** Haya sema ya mwisho

**Mr. Mwakochola:** Haya rasilmali zilizopo nchini. Wananchi wa Kenya vitu hivi vimilikiwe na wenyeji kwa manufaa ya wananchi walioko katika sehemu vitu hivo vinapatikna. Taasisi katika kila chombo cha kusimamia rasilimali ardhi, kwa mfano ardhi. Tuwe na ofisi za ardhi katika kila kiwango. Tasisi hizi zichaguliwe na wananchi kwa mfano ofisi ya kama tusema hivi survey, kama Game Reserve tuwe na ofisi yetu ambaye itachaguliwa na Wataita na ndiyo hiyo wataibuni, rekodi za ardhi ziwekwe katika kiwango cha locational kwa sababu zitakuwa zikipatikana kwa njia rahisi na record hizi zitahifadhiwa na watu ambaao watakuwa wakifanya kazi hapo. Uwikizaji wa ardhi usiweko kwa sababu ardhi ni ya wananchi na wenye walikuwa wamepewa miliki hizo mfano wa hawa watu wa Taveta wazirudishe.

**Com Ratanya:** Okay sasa utamalizia yako hapa na twende kwa Peter Misiko, kwa Peter tuambie kwa ufupi usirudie yale yamesemwa na wengine. Dakika moja.

**Mr. Peter Misiko:** Hamjambo. Mimi hapa nakuja kwa officer, nimefika kwa sababu ya kazi yangu. Kazi yangu nafanya kazi ya ufundi.

**Com Ratanya:** Bwana Misiko tungetaka utuambie yale ungetaka yaingie kwa kutengeneza katiba.

**Mr. Misiko:** Kutengeneza katiba

**Com Ratanya:** Mapendekezo yako yale unataka tume itumie kwa kuingiza kwa katiba mpya.

**Mr. Misiko:** Mpya

**Com Ratanya:** Ndiyo mapendekezo

**Mr. Misiko:** Mapendekezo yangu nataka kwa kazi yangu ya ufundi ya kufunga mawe ya kufanya matafari ya Mawa.

**Com Salim:** Ungependa kusema nini hapa matafari yako.

**Mr. Misiko:** Nataka kazi yangu nataka wale watoto wanazurura zurura mnisaidie kwa serekali ile kufundisha kazi ile ya ufundii. Yangu nimefanya. Nimefanya kwa miaka nyingi sasa nataka kuachia kazi yao yakupata pesa.

**Com Ratanya:** Kwa hivyo Bwana Misiko una mengine unayo tuambie ingine moja.

**Mr. Misiko:** Ingine moja. Nikusaidiwa na serekali kuisadiwa na serekali kuletwala kazi yangu.

**Com Ratanya:** Asante sana. Kwa hivyo nenda hapo. Misiko niandikie hapa.

**Com Salim:** Na sasa umefika wakati wa kufunga kikao chetu hiki. Tumemsikia mwananchi wa mwisho. Kuna maoni yake kwa leo iliyobaki kwa hakika ni kuashukuru nyote wale memutoa maoni wakaondoka na wale amba mamebakia kusikia mpaka dakika ya mwisho twawashukuru sana kwa subira yenu uwezekano wenu kikuwa nasi mpaka dakika ya mwisho. Kwa hivyo twashukuru na twawakikishia kwamba maoni yenu tumeandika pia tumeyanasa kwenye tape na tukirudi tutasikiza tapes sote na memoranda zote tulizopewa na kuakikisha kwamba maoni hayo yakuwemo katika katiba. Kwa hivyo namshukuru sana Reverend kwa ukarimu wako wa kutuwezesha kukutana katika kanisa hili na tungependa utumalizie. Kama vile utuanzia kwa maombi . Karibu.

**Reverend Skever Shuma:** Basi tungeomba tungesimama halafu tumshukuru mungu kwa nafasi hii ambayo ametupatia siku wa leo kwa ajili ya kazi hii ambayo ilikuwa mbele zetu. Natuombe. Mungu wetu baba yetu wa mbinguni tunashukuru kwa kuwa bwana ulikubali sisi kutuwezesha kuona siku ya leo na tena mungu tunakushukuru kwa ajili ya siku hii ambayo bwana tuliandaliwa kikao hiki cha kukusanya maoni kwa watu wako wa sehemu hii. Kwa ajili ya katiba mpya ya nchi yetu ya kenya. Tunakushukuru kwa wageni wetu amba bwana uliwaleta mahali hapa na akawenza kufanya kazi hii bwana ambayo waliipangia kuifanya mahali hapa.

Tunakushukuru Mungu wetu hata kwa wananchi wa sehemu hii amba bwana wamekuja mahali hapa na wakatoa maoni yao kuhusu katiba wanayoitarajia ambayo bwana utakua ndiyo mwongozo katika nchiyetu ya kenya katika siku zijazo. Tunashukuru mungu wetu kwa vile umeweza shughuli hii kufanya kwa njia nzuri kama vile bwana ilivyo tarajiwa na hawa wageni amba wamekuja hapa ili kuweza kufanya shughuli hii ya kukusanya maoni ya watu wako.

Mungu tunashukuru kwa yote ambayo umetufanya tangu asubuhi na hata kufikia sasa. Na sasa Mungu imefikia wakati ambapo sisi tutafumuka, tunaomba Mungu wetu tufumukane tukiwa mikononi mwako. Tunaomba wageni wetu wanaposafiri kutumia magari bwana uweze kuwapa safarini njema. Uwalinde mahala popote watakopopitia na tunaomba uwezo wako upate

kuandamana pamoja na wao ili bwana waende kwa njia nzuri hata wafike mahala hapo wataenda kulala usiku wa leo.

Na sisi amba tulikuja mahala hapa bwana tunapoondoka tukitumia miguu tunaomba Mungu wetu uwepo wako uandamane nasi na utulinde na utupe safari njema na kila moja wetu aweze kurudi nyumbani mwake akiwa mkononi mwako Bwana tunakushukuru kwa yote tunaomba sasa baraka zako zindamane pamoja nasi na tuendelee kuziona tunapoondoka mahala hapa na mahali popote tutakapopita tangu sasa Mungu tunaomba tuendelee kuona wewe na baraka zako tuweze kuzishuhudia. Tunaomba kazi hii ambayo tunaendelea kufanyika siku hii ya leo Mungu naomba na mahali popote ambapo kazi inaendelea kufanyika bwana tunaomba wewe mwenyewe usaidie watu wako ili kazi hii ifanyike kwa njia mzuri na mwishoni ituzalie matunda mema ambayo itakuwa ni katiba mpya ambaye itakuwa na katiba ambaye, kila moja wetu anayeishi katika nchi ya Kenya ataikubali na utaweza wa kuishi kulingana na hiyo.

Tunaamini kwamba Mungu wetu umetusikia na unatenda hayo kwa kuwa tunaomba tukiamini katika jina la Yesu Kristo mwokozi wetu. Amen.

Tushikiriane tukisema neema ya bwana wetu Yesu Kristo na mapenzi ya mwenyezi Mungu baba na ushirika wa roho mtakatifu uwe pamoja nasi sote na hata milele. Amen

Asante sana wageni kuwa pamoja nasi tunaomba Mungu amufikishe katika kazi yenu.

Meeting ended at 5.00 p.m.